# Nipashe

Jumanne Mei 21, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579923

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Dk. Mengi atajwa alivyosaidia kusajiliwa kwa benki ya CRDB

UKURASA 11





Nipashe
TESA
Jumanne Mei 21, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ukurasa 15
Wana Suba wapania kuwakwamua wanafunzi 846 waliobaki nyumbani
Ukurasa 18.
JE, WAJUA?
Mambo matano yanayodhihirisha dunia 'si ya wanawake'
Yasiyomalizika kuhusu ubaya katika uhusiano mantiki yake kisaikolojia
Chuo cha Ualimu Vikindu katika mahafali ya 18 ya kutoa walimu

UKURASA 13

# Korosho zawa moto bungeni

• **Wabunge** wataka waliopotosha serikali wachukuliwe hatua, mwingine aeleza hali ilivyo jimboni kwake, waomba CAG achunguze...*Endelea uk.2*



Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele (kushoto), akihojiwa mbele ya Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa tuhuma za utovu wa nidhamu katika kikao kilichofanyika Ofisi za Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## Masele ahojiwa bungeni

UK. 2

## Shamhuna, Ngwilizi wafariki dunia

UKURASA 2


**MICHEZO** **KAMPIRA AITABIRIA YANGA MAKUBWA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akishiriki katika kuusalia mwili wa marehemu Ali Juma Shamhuna, kabla ya mazishi yaliofanyika katika Kijiji cha Donge Imiyani, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Korosho moto bungeni

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

SAKATA la kuchelewa kuuzwa kwa korosho zilizokusanywa na serikali kutoka kwa wakulima, limeendelea kuteka mijadala ya Bunge baada ya jana wabunge mbalimbali kulizungumzia wakitaka wahusika kuwajibika au kuwajibishwa.

Katika mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye (CCM), alisema bungeni jijini Dodoma jana, kuwa wote waliohusika na kile alichokiita hujuma dhidi ya zao la korosho, wajiwajibishe au wachukuliwe hatua.

Alisema kama watu hawatawajibika wenyewe, anakusudia kuwasilisha hoja bungeni ili chombo hicho cha kutunga sheria kichukue hatua kuwawajibisha.

Nnauye ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema zao la korosho liko chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU), akitaka mkakati wa ununuzi wa zao hilo kupitiwa kwa makini.

Alisema kuna haja Bunge kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kukagua kile alichokiita udanganyifu katika malipo ya korosho kwa wakulima.

Alisema baada ya ukaguzi huo wa CAG, taarifa iwasilishwe bungeni na ijadiliwe na wabunge, akieleza kuwa maelezo yanayotolewa kuhusu malipo ya korosho si ya kweli.

"Nia ya Rais ilikuwa njema kabisa, lakini waliokwenda huko wamefanya mazonge na mambo ya ovyo, hapa tukubaliane, siyo serikali yote imeharibu, bali wako waliofanya mambo ya ovyo, ni vema wakawajibika ama kuwajibishwa," Nnauye alisema.

Mbunge huyo alisema Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga na wasaidizi wake hawahusiki katika sakata la korosho, lakini wapo wanaotakiwa kuwajibika. Hata hivyo, hakuwataja.

Nnauye pia alisema uchun

INAENDELEA UK. 8

# Masele: Nimelelewa vyema

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

HATIMAYE Makamu wa Kwanza wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), Stephen Masele, amehojiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka kuhusu tuhuma za utovu wa nidhamu, huku akisisitiza amelelewa vyema na wazazi na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hatua hiyo ya kuhojiwa kwa Masele imetokana na agizo la Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, kuandika barua kwa Rais wa PAP kumtaarifu kusitisha uwakilishi wa mbunge huyo na kumtaka kurejea nchini kuhojiwa kwa tuhuma za utovu wa nidhamu.

Wakati Spika Ndugai akitangaza uamuzi huo Jumatano, Masele ambaye pia ni Mbunge wa Shinyanga Mjini (CCM), alikuwa Afrika Kusini akishiriki vikao vya PAP.

Huku Spika Ndugai akilieleza Bunge kuwa Masele amekaidi mara kadhaa kurejea nchini kuhojiwa, jana saa 3:40 asubuhi, mbunge huyo aliingia bungeni na baadaye saa 5:34 asubuhi aliingia kwenye chumba cha mahojiano na Kamati ya Maadili iliyomhoji hadi saa 9:18 alasiri.

Kabla ya kuhojiwa na kamati hiyo, Masele ambaye mwaka 2010 alitangazwa kushinda kiti cha ubunge kwa tofauti ya kura moja, aliingia kwenye ukumbi wa Bunge kisha akaingia kwenye maktaba ya Bunge na baadaye kuingia kwenye mgahawa wa chombo hicho cha kutunga sheria.

Saa 5:10 asubuhi, Masele alitoka kwenye mgahawa huo na kufanya mazungumzo ya dakika nne na Mbunge wa Bariadi Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Serikali, Andrew Chenge.

### KAULI YA MASELE

Baada ya kuhojiwa na Kamati ya Maadili, Masele aliwaambia waandishi wa habari kuwa ameitikia wito wa Bunge, huku akisisitiza hajawahi kufanya vitendo vya utovu wa nidhamu katika kipindi chote akiwa kiongozi.

Alisema amelelewa vyema na wazazi wake na CCM aliyoitumikia katika ngazi mbalimbali kuanzia akiwa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) hadi kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

"Mimi nimelelewa vizuri na wazazi wangu na chama kuanzia ngazi ya chini hadi juu, nimekuwa kiongozi UVCCM, mjumbe wa baraza kuu la chama, natambua miiko ya kiuongozi na sijawahi kufanya kosa la utovu wa nidhamu," alisema.

Masele aliongeza: "Nilichofanya ni kutetea misingi ya haki za binadamu. Isitafsiriwe kwamba ni utovu wa nidhamu."

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emmanuel Mwakasaka, baada ya kumhoji Masele, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wanaendelea kufanya uchambuzi wa shauri lake na wakimaliza kazi, watakabidhi taarifa kwa Spika.

# Shamhuna, Ngwilizi wafariki dunia

**Na Romana Mallya**

WANASIASA wakongwe nchini, Ali Juma Shamhuna na Brigedia Jenerali mstaafu Hassan Ngwilizi, wamefariki dunia.

Taarifa zilizopatikana jana zilieleza kuwa Ngwilizi alifariki dunia jana katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Dar es Salaam, wakati Shamhuna alifariki dunia juzi visiwani Zanzibar.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alitangaza jana kuwa Ngwilizi, ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alifariki dunia jana katika Hospitali Kuu ya Jeshi ya Lugalo alikokuwa akipatiwa matibabu.

Katika uhai wake, Ngwilizi alitumikia Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kuanzia mwaka 1968 hadi 1993 katika nafasi mbalimbali hadi Brigedia Jenerali.

Pia aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Mbunge wa Kuteuliwa na baadaye Mbunge wa Mlalo, Lushoto mkoani Tanga kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2005 hadi 2015.

Ndani ya Bunge aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Maraka ya Bunge na pia Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Bunge iliyoundwa Julai 2 mwaka huo kuchunguza kashfa iliyomhusisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini na Nishati, Eliakim Maswi, akiwatuhumu baadhi ya wabunge kula rushwa kutoka kwenye kampuni ya mafuta.

Kwa upande wake, Shamhuna ambaye aliwahi kuwa Naibu Waziri Kiongozi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, alizikwa jana Donge Kaskazini Unguja na wakati wa uhai wake alishika nyadhifa tofauti ndani ya serikali.

Shamhuna ambaye pia aliwahi kuwa Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Zanzibar aliwahi kuwa Waziri wa Elimu, Mafunzo ya Amali na Waziri wa Maji, Ardhi, Nyumba na Nishati (Zanzibar).

Mwaka 2010 hadi 2012 alikuwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Zanzibar, mwaka 1981 alikuwa Mwakilishi wa Kwahani mjini Unguja.

Shamhuna alizaliwa Januari 1, mwaka 1944 na alifariki dunia akiwa Fuoni Wilaya ya Magharibi, Unguja.

## HABARI KITAIFA

# Mbunge CCM aitaka serikali ihalalishe kilimo cha bangi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI Jeshi la Polisi likipiga vita kilimo cha bangi na kuharibu mashamba yaliyolimwa kilevi hicho, Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba (CCM), ameishauri serikali kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya utengenezaji wa dawa za binadamu.

Akichangia mjadala bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha, Kishimba alisema nchi tayari nne barani Afrika zimeruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya matumizi ya dawa za binadamu.

"Ni vizuri kama dunia inapopata kitu kizuri ni vyema Watanzania tukawahi. Ninavyoongea kuna gazeti... (alitaja jina la gazeti) la tarehe 15 limesema Uganda imesharuhusu kulima bangi kwa ajili ya dawa za binadamu," Kishimba alisema.

Mbunge huyo aliongeza kuwa asilimia 80 ya dawa za maumivu ya saratani zinatokana na bangi.

"Nashangaa wataalamu wetu wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), wangekuwa wameshachukua sampuli na wangewajulisha kuwa dawa zilizo na bangi ndani yake.

"Wangemuuliza msambazaji hiyo bangi anaitoa wapi? Mheshimiwa Spika, sisi wenyewe tunayo bangi hiyo, tunaona kila siku inakatwa, ukweli nyingi siyo kwa ajili ya kuvuta. Bangi hiyo imekuwa ikienda katika dawa za binadamu," Kishimba alisema.

Aliendelea kujenga hoja yake akieleza kuwa mbali na Uganda, nchi za Lesotho na Zimbabwe pia zimeruhusu kilimo cha bangi na kuna viwanda vya kutengeneza dawa za binadamu kwa kutumia bangi.

Alilieleza Bunge kuwa gunia moja la bangi nchini linanunuliwa kwa bei ya kati ya Sh. milioni nne na Sh. milioni 4.5 na kwa Lesotho na Zimbabwe, gunia moja linauzwa Sh. milioni 20.

"Bangi karibu yote ya Tanzania inakwenda katika dawa za binadamu ambazo tunaletewa kutumia. Kuna ubaya gani (nchi) ikaanza kutoa vibali kwenye maeneo mbalimbali na kuhalalisha watu waanze kulima bangi hiyo na kupata faida?" Kishimba alihoji.

Mbunge huyo alisema haungi mkono kauli ya Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma (CCM), ambaye amekuwa akitaka bangi kuhalalishwa kwa ajili ya kuvuta.

"Ni vizuri Waziri wa Kilimo (Japhet Hasunga) awasiliane na Waziri wa Afya (Ummy Mwalimu) waone namna gani watafanya, lakini watambue kwamba bangi ni zao ambalo pia haliliwi na wadudu. Hekari moja ya bangi unapata gunia sita," alisema.

Baada ya Kishimba kuwasilisha mchango wake, Spika wa Bunge Job Ndugai, alimpongeza mbunge huyo kwa uwasilishaji mzuri na kuwataka wabunge kuiga uchangiaji wa kujikita katika eneo moja.

"Niwape siri, muongee kama Kishimba, unakuja na kitu chako fulani, unajikita sehemu moja. Hii hoja ni nzuri sana, naamini Jenista (Mhagama - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana, Kazi na Watu Wenye Ulemavu) ameipigia mstari," Spika Ndugai alisifu.

# IFAD yaimwagia Tanzania bil. 127/-

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) umetenga Sh. bilioni 127.3 kwa ajili ya ufadhili wa miradi ya kilimo nchini kwa miaka mitatu kuanzia mwakani.

Rais wa IFAD, Gilbert Houngbo, alisema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, alipokutana na kufanya mazungumzo na Rais John Magufuli.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema pamoja na kutenga fedha hizo, Houngbo ambaye ni Waziri Mkuu mstaafu wa Togo, alimpongeza Rais Magufuli na

INAENDELEA UK 8


NMB
Karibu yako

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 19 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 19 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam saa 4 asubuhi siku ya Jumamosi, Juni 15, 2019. Agenda itakuwa kama ifuatavyo:**

19.1 MATANGAZO NA AKIDI

19.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

19.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 18 ULIOFANYIKA TAREHE 2 JUNI 2018

19.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 18 WA WANAHISA

19.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

19.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

19.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

19.8 KUTEUA WAKURUGENZI

19.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2019

19.10 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima aje na nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni kabla ya saa 4 asubuhi Ijumaa ya tarehe 14 Juni 2019.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake mwenyewe. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini.
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 66 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 33 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2018.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| Tarehe ya tangazo: | 17 Mei 2019 |
| Hisa kuuzwa pamoja na gawio : | 17 Mei 2019 |
| Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio : | 6 Juni 2019 |
| Hisa kuanza kuuzwa bila gawio: | 7 Juni 2019 |
| Daftari la wanahisa kufungwa: | 11 Juni 2019 |
| Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe | 27 Juni 2019 |

**Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,**

Lilian R. Komwihangiro
**Katibu wa Kampuni**

10 Mei 2019

215238302

www.nmbbank.co.tz

HABARI KITAIFA

# Mkakati wa kupunguza madhara ya maafa waja

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mkakati wa taifa wa upunguzaji wa madhara ya maafa.

Akizungumza hivi karibuni na Nipashe, Mchumi Mwandamizi na Mtaalamu wa Usimamizi wa Maafa wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Charles Msangi, alisema mkakati huo ni utekelezaji wa mkataba wa Sendai, uliosainiwa mwaka 2015 wa kuzitaka nchi kuwa na mpango wa kupunguza madhara yanayotokana na maafa.

Mkataba wa Sendai utatekelezwa hadi mwaka 2030, lengo ni kuongeza jitihada za kukabiliana na majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu yanayotokea duniani kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Majanga hayo ni tetemeko la ardhi, magonjwa, njaa, ukame kupindukia, mafuriko, mvua nyingi, mabadiliko ya vipindi vya mvua, maporomoko ya ardhi na miamba na kuongezeka kwa kina cha bahari, huku sehemu ya ardhi ikimezwa.

"Sendai ni makubaliano ya hiyari, katika kutekeleza serikali ilitunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Namba saba ya mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2017," alisema na kuongeza:

"Vilevile, imerejea sera ya taifa ya menejimenti ya maafa ya mwaka 2004, ambapo imeandaliwa rasimu ya sera ya taifa ya upunguzaji wa madhara ya maafa mwaka 2018 na maoni ya kuiboresha yanaendelea kupokelewa," alisema.

Msangi alisema katika utekelezaji wa mkataba huo, makundi mbalimbali yanashirikishwa ikiwamo kamati za usimamizi wa maafa kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa, kata, wilaya na mkoa ambazo zipo kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa namba saba ya mwaka 2015.

Kuhusu matukio ya vimbunga yaliyotokea nchi za Msumbuji, Malawi na Zimbabwe, alisema Tanzania imejifunza kuwa kutokana na mabadiliko ya tabia kuna uwezekano mkubwa wa majanga ambayo hayakuwa ya kawaida yanayoweza kutokea nchini.

"Serikali inachokifanya ni kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji hali ya hewa na kutoa tahadhari kwa umma kunahitaji kupewa kipaumbele, kuimarisha utoaji wa elimu ya majanga kwa umma, kujenga uwezo wa wataalamu wajue majukumu yao katika masuala ya usimamizi wa maafa," alibainisha.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa kingo za katikati za barabara ya Chang'ombe-Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Mwanaharakati Chadema aweka msimamo

**Na Romana Mallya**

MWANAHARAKATI Mdude Nyangali maarufu (Mdude Chadema), amefunguka na kueleza kuwa licha ya kutekwa na watu wasiojulikana na kupigwa kipigo ambacho hajawahi kukipata, hataacha harakati zake mitandaoni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mdude alisema tukio lililomtokea Mei 4, mwaka huu, ni la utekaji na si kwamba alipotea kama Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alivyoeleza bungeni.

Alisema anamtilia shaka Masauni kuwa anawajua waliomteka na kumwomba Rais John Magufuli amfute kazi.

"Kuna uhusiano kati ya maelezo ya Masauni bungeni aliyowataka vijana wawe makini kwenye mitandao kwa kuichafua serikali kuwa hawatawavumilia na wakati nimetekwa watekaji waliniambia kuwa nimeichafua serikali ninatumiwa na mabeberu," alisema.

Alisema kwa kauli hizo mbili, anamtuhumu Naibu Waziri Masauni kuwa anawajua watekaji.

Pia alilituhumu Jeshi la Polisi kuwa ndilo lililohusika na tukio la kutekwa kwake kwa sababu licha ya kutokea mita chache kutoka kituo cha polisi kilipo na yeye kupiga kelele za msaada, hakusaidiwa.

"Mwizi hawezi kujichunguza. Ninacho

INAENDELEA UK. 8




## WMA sasa kuanza vipimo vya umeme

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKALA wa Vipimo (WMA) umesema unatarajia kuanza kupima vipimo vya umeme, lengo kuu likiwa ni kumlinda mtumiaji ili aweze kujihakikishia kuwa vipimo atakavyotumia ni sahihi kulingana na sheria ya vipimo nchini.

Mkurugenzi wa Vipimo WMA, Stellah Kahwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akieleza kuhusu maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yanayoadhimishwa kila Mei 20, ambayo kwa mwaka huu yamebeba kaulimbiu isemayo 'Mfumo wa vipimo kimataifa kimsingi unaboreshwa'.

"Katika kuhakikisha mwananchi anaendelea kuwa salama, WMA tunaelekea kuanza kupima vipimo vya umeme, tunachosubiri kwa sasa ni serikali ituwezeshe vifaa ili tuanze kufanya kazi hiyo," alisema Kahwa.

Alisema WMA wameshaanza kufanya uhakiki wa dira za maji na mamlaka zote za maji na waagizaji wote huleta dira zao kwa ajili ya kuhakikiwa, hivyo hata kwenye upimaji wa vipimo vya umeme WMA itafanya uhakiki kama huo.

Kadhalika, Kahwa aliwaonya wafanyabiashara wanaoweka sumaku katika mizani yao kwa lengo la kuwaibia wateja wanaponunua bidhaa kwao.

Alisema kuweka sumaku katika mizani ni kinyume na sheria na taratibu za vipimo, hivyo yeyote atakayekamatwa atachukuliwa adhabu.

"Adhabu kwa watu wanaonyonga mizani au kuweka sumaku inafahamika, faini yake ni kuanzia Sh. milioni moja na kuendelea, hivyo ninawaonya wafanyabiashara waache mara moja tabia hiyo," alisema Kahwa.

Alisema kwa sasa WMA inafanya kazi ya ukaguzi katika sekta ya biashara, kilimo, usafirishaji, maji, madini, mafuta, viwanda, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa kwa usahihi kulingana na thamani ya fedha inayotolewa.

HABARI KITAIFA

# Tanzania ya 9 uwazi wa manunuzi ya umma duniani

**Na Salome Kitomari**

TANZANIA imeshika nafasi ya tisa kwenye uwazi wa mikataba ya manunuzi ya umma kati ya nchi 25 duniani.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Shirika Lisilo la Kiserikali la Maendeleo Hivos, imeonyesha kuwa katika eneo la uwepo wa sheria zinazosaidia utekelezaji wa manunuzi ni asilimia 100.

Ripoti hiyo imeonyesha kuwa kwenye ufanisi wa manunuzi ya umma Tanzania imepata asilimia 90.

Aidha, kwenye eneo la uwajibikaji Tanzania imepata asilimia 71.43, huku kwenye eneo la ushindani imepata asilimia 89.5.

Ripoti hiyo imeonyesha kuwa Tanzania haijafanya vizuri kwenye eneo la uwazi kwenye utaratibu wa manunuzi ya umma kwa kupata asilimia 34.4.

Aidha, ripoti hiyo imebainisha kuwa mfumo wa kushughulikia manunuzi kielektroniki umesaidia kuwezesha utaratibu wa manunuzi kufanyika kirahisi.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa mifumo iliyojengwa kwenye utaratibu wa manunuzi, ikiwamo kutangaza zabuni na kuwezesha wahusika kuzijaza kirahisi zaidi.

Aidha, kwenye eneo la kutoa zabuni Tanzania imepata asilimia 80.

# NEMC yahimiza uhifadhi wa mti wa msandali

**Na Mwandishi Wetu, MANYARA**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi wa Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka Watanzania kujikita katika upandaji wa miti ya misandali kitaalamu 'Osyris lanceolata' ikiwa sehemu ya kutunza mazingira na pia fursa nzuri ya biashara kutokana na umuhimu wa miti hiyo katika kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Akizungumza baada ya kutembelea kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kutengenezea manukato cha Sierra limited kilichopo mkoani Manyara, Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu, alihimiza umuhimu wa kupanda wa msandali na aina mbalimbali ya miti ya mingine kutokana na faida zake kimazingira na kiuchumi.

"Hii ni fursa kwa vijana kujikita katika kupanda mashamba ya miti ya misandali ambayo faida yake kwa baadaye ni kubwa kutokana na uhitaji mkubwa wa mti huo katika kuzalisha malighafi ya kutengenezea manukato," alisema Prof. Chaggu.

Alisema uwekezaji wa aina hii kwa vijana unawaletea faida kubwa kiuchumi baada ya kuivuna na pia mazingira yatakuwa yanaendelea kulindwa hali ambayo itapelekea ustawi wa nchi kimazingira kuimalika na pia kiuchumi.

"Ni muhimu kuhamasisha Watanzania nchini kupanda mti wa msandali na aina nyinginezo ambayo inafaida kubwa katika matumizi yake, kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaendelea kuongeza idadi ya miti hii kuwa mingi nchini," alisema Prof. Chaggu.

Prof. Chaggu alisema utafiti unaonyesha kupungua kwa mti huu kutokana na umuhimu wake mkubwa katika kutengeneza dawa za maradhi mbalimbali kwa binadamu na pia kutengeneza mafuta yanayotumika kuzalisha manukato hivyo kama wadau wa mazingira wanalazimika kuhamasisha upandaji wa miti hii ili kuiendeleza na kuja kusaidia vizazi vijavyo.

"Nchi yetu ina maeneo mengi ambayo tunaweza kupanda miti ya aina ya msandali kwa lengo la kuongeza idadi ya miti hiyo nchini na pia kuwa sehemu ya fursa kwa vijana kujipatia kipato kupitia uwekezaji wa miti," alisema.


NMB
Karibu yako

## Maboresho ya Mawasiliano na Taarifa za Kibenki Kwa Wanahisa wa NMB Kwa ajili ya Malipo ya Magawio

Tunaomba wanahisa wote wa NMB waboreshe maelezo ya mawasiliano yao na taarifa za kibenki kwa ajili ya akaunti zao husika wanazotumia. Tangu Benki ilivositisha mchakato wa malipo ya hundi kwa magawio, tunaomba taarifa za akaunti za kibenki kwa kila mmiliki au mdhamini kuborehswa katika matawi ya NMB yaliyopo nchini kote.

Hii ni kwa ajili ya wanahisa wote wa NMB ambao hawajapata gawio lolote tangu waliponunua hisa, wale waliopata baadhi ya magawio, waliobadilisha maelezo ya kibenki katika kipindi hicho, waliobadilisha namba za simu na anuani ya makazi.

Tafadhali tembelea tawi lililo karibu nawe na ujaze fomu husika ya gawio la mwanahisa vizuri iwasilishe kwa meneja wa huduma kwa wateja au tuma kama barua au barua pepe katika anuani zifuatazo hapo chini:

**Anuani:**
**NMB Plc – Makao Makuu**
**Ohio/Ali Hassan Mwinyi -Makutano**
**Ghorofa ya NNE - Idara ya Fedha**
**S.L.P 9213.**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255222322000**
**Nukushi: +255222112148**

**Kwa maelezo Zaidi, tafadhali wasiliana na:**

- Dividend_unit@nmbtz.com
- Njabha.Njabha@nmbtz.com or call 0222322356
- Dismas.Nsindo@nmbtz.com or call 0222322369
- Veronica.pascal@nmbtz.com or call 0222322374

www.nmbbank.co.tz

215238902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Waziri Lugola kwa trafiki litekelezwe

**KWA** muda mrefu madereva wamekuwa wakilalamikia tabia ya baadhi ya askari wa usalama barabarani kuwabambikia kesi za makosa ya picha za mwendokasi (speed rader).

Kilio cha madereva ni kuwa picha hizo hazina uhalisia, na kwamba lengo la askari hao ni kujipatia mapato.

Baada ya kilio hicho cha muda mrefu dhidi ya askari hao, serikali imefunguka na kutoa onyo kwa askari hao, kwamba wakiendelea na tabia hiyo watawajibishwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, andiye aliyetoa angalizo kwa askari hao, akisema kwamba trafiki wanaowabambikia madereva makosa hayo wakibainika watawajibika kuzilipa wao wenyewe faini hizo sambamba na kuondolewa katika kitengo hicho.

Alitoa agizo hilo juzi mjini Morogoro alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maafikiano kati ya vyama vya watoa huduma za usafirishaji nchini kuhusu kusitisha kusudio la madereva wa mabasi ya abiria kufanya mgomo wakishinikiza kutimiziwa madai yao mbalimbali ikiwamo ya mikataba ya kazi.

Alisema maamuzi hayo yametokana na makubaliano ya pamoja kati ya viongozi wa vyama hivyo vya usafirishaji pamoja na wizara mtambuka za serikali kwa nia ya kutatua changamoto walizowasilisha katika kikao hicho kuhusu kubambikiwa makosa na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani.

Waziri Lugola, alisema moja ya makosa yanayolalamikiwa na madereva hao ni pamoja tochi zinazopiga picha mabasi na kurushwa kwenye simu za askari zinakosa uhalisia wa tukio ikiwamo kutoonekana kwa namba za usajili pamoja na vibao vya kuzuia makatazo mbalimbali na kusababisha utata na mivutano yenye nia ya kujenga mazingira ya rushwa.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kuanzia sasa askari hao wanapaswa kupiga picha katazo mbalimbali za barabara mbele ya gari ikionyesha mwonekano usio na shaka, namba ya usajili pamoja na eneo la alama iliyokiukwa na dereva ili kuwapo na ushahidi halali, vinginevyo dereva huyo asichukuliwe hatua yoyote.

Alisema dereva anapokuwa na shaka na picha iliyopigwa dhidi ya gari lake kama haionyeshi usajili wa namba za gari na eneo la kibao cha zuio asikubali kuadhibiwa badala yake amweleze huyo askari azitume picha hizo kwa msimamizi wa kikosi cha usalama barabarani na aende huko.

Uamuzi huo umetolewa wakati mwafaka, kutokana na madereva wengi kulalamikia vitendo vya baadhi ya trafiki hao ambavyo vinaashiria kuwa lengo lao ni kujitafutia kipato kupitia rushwa.

Tunatambua mchango mkubwa wa trafiki katika kusimamia usalama barabarani, ikiwamo kupunguza matukio ya ajali, lakini jambo la msingi ni kuwa hawanabudi kuelewa kuwa hawapo juu ya sheria bali wanapaswa kiziheshimu na kuzifuata.

Kwamba kinyume cha hapo watapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

Ni matarajio yetu kuwa askari wote wa usalama barabarani wamesikia katazo la Waziri Lugola na watalizingatia.

Kwa upande wao madereva wasikubali kutekeleza maelekezo ambayo yanakwenda kinyume cha katazo la waziri, badala yake watoa taarifa kwa mamlaka za juu kama ofisi za trafiki mikoa, makao makuu na kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, askari watakaokaidi washughulikiwe.

Sio sawa kwa askari wanaoendekeza uonevu na vitendo vya rushwa kuwageuza madereva kuwa chanzo chao mapato bila sababu za msingi.

Ifike mahali Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa itumike kuwafuatilia na kuwatia mbaroni trafiki wanaofanya vitendo hivyo ili sheria ichukue mkondo dhidi yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mamlaka zielimishe raia kujenga utamaduni wa kubeba kitambulisho



Na Raphael Kibiriti

**KILA** raia ana wajibu wa kutekeleza katika suala zima la kuhakikisha ustawi wake na taifa kwa ujumla.

Wajibu ambao kimsingi unaangukia katika uga wa kisheria pia kwenye mizania ya mila na tamaduni za jamii anayoishi.

Kwa mfano kutii sheria, kulipa kodi, kulinda usalama wa nchi, amani ya jamii yake, yote haya ni wajibu wa raia mwema kwa taifa lake.

Pamoja na hayo, kuna wajibu wa kawaida katika maisha ya kila siku ambao hata hivyo bado haujatiliwa maanani kwa uzito unaostahili na wananchi walio wengi.

Si wananchi tu, lakini hata mamlaka za serikali zinazohusika na jukumu la kutoa elimu ili raia wawe na utamaduni wa kutimiza wajibu huo kwa minajili ya kuepuka usumbufu na mazonge mbalimbali wanayoweza kukumbana nayo.

Muungwana anazungumzia utamaduni wa kutembea na kitambulisho cha taifa ama kingine kinachotambulika na mamlaka, kikiwamo cha mpigakura ama hati ya kusafiria kwa wale walio nazo.

Amechukua fursa ya kuandika hili baada ya kukumbana na operesheni ya Idara ya Uhamiaji katika safari aliyoifanya mwezi Machi mwaka huu kwenda Mpanda, mkoani Katavi, kusalimia ndugu na jamaa.

Safari yake ya kurejea jijini kutoka Mpanda ilikuwa ni ya basi na ilianzia Sumbawanga mkoani Rukwa kupitia mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Morogoro, Pwani kisha jijini.

Sasa baada ya kutoka Mbeya mjini mwendo kama wa saa moja alikutana na kizuizi cha uhamiaji ambacho baadaye alijifunza kutoka kwa abiria wengine wanaofanya safari za mara kwa mara wakitumia barabara hiyo kwamba kumbe ni cha kawaida.

Maofisa Uhamiaji wawili waliingia ndani ya basi alilokuwa akisafiria ambao katika lugha ya heshima lakini yenye mamlaka, walitaka kila abiria ndani ya gari hilo kuonyesha kitambulisho cha taifa kwa ajili ya utambulisho.

Hata hivyo, hawakutaka cha taifa tu, kwamba kwa wale ambao hawakuwa nacho, walitakiwa kuonyesha cha mpiga kura ama hati ya kusafiria kama mbadala.

Kwa Muungwana ambaye anajua umuhimu wa kutembea na kitambulisho si kwa safari za mbali kama hii aliyoifanya bali hata anapoenda kazini, katika miadi yoyote ama kwenye burudani hubeba kitambulisho, haikuwa shida kwake.

Hubeba kitambulisho cha taifa, ama cha kupigia kura au cha kazini ili ajitambulishe wakati wowote kikihitajika.

Na hasa ikichukuliwa kwamba vyombo vya usalama huwa na operesheni mbalimbali za kiusalama, zinazohitaji raia wajitambulishe wakati mwingine.

Hivyo alikitoa kwa maofisa hao wa uhamiaji kama ilivyokuwa kwa abiria wengine wenye utamaduni wa kutembea na kitambulisho, kwa sababu wanajua ni wajibu wao wa msingi kufanya hivyo.

Ilikuwa ni bahati mbaya kwa ambao hawakuwa navyo, kwani walitumia muda mrefu kujieleza ili kuwaridhisha maofisa hao kutokana na maswali waliyokuwa wakiulizwa.

Chenye maslahi katika operesheni hiyo ni kwamba, maofisa hao waliweza kukamata abiria watatu ambao hawakuwa raia wa Tanzania kutoka nchi jirani walioingia nchini isivyo halali.

Ni maoni ya Muungwana basi kwa kila raia mwenye umri wa kuanzia miaka 18 kuwa na utamaduni wa kutembea na kitambulisho kinachokubalika na vyombo vya dola, kuepuka mazonge yanayoweza kujitokeza.

Mazonge kama ya kushikiliwa na vyombo vya dola kwa kutokuwa na kitambulisho, hivyo kukatishwa ama kucheleweshwa safarini au pale mtu anapokuwa katika shughuli zake za kila siku za kimaisha.

Aidha, Muungwana anatoa rai kwa mamlaka zinazohusika ikiwamo Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Uhamiaji kwa maana hiyo kutoa elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa raia kutembea na vitambulisho vinavyokubalika.

Kwamba pamoja na mambo mengine vitambulisho, hasa cha taifa vina umuhimu kwa usalama wa nchi katika kubaini wahamiaji haramu kama ilivyotokea katika safari ya Muungwana.

# BARUA/MJADALA

## *Serikali itulipe mafao ya fidia zetu*

**Mhariri,**

POLE kwa majukumu ya kazi. Ninaleta kwako malalamiko ya wakazi zaidi ya 1,000 wa Kata za Mchikichini, Jangwani, Upanga Magharibi zote za jijini Dar es Salaam.

Sisi wakazi wa kata hizo tajwa tunaomba kulipwa mafao ya fidia zetu ili kupisha mradi wa Tanesco katika kata ya Mchikichini na Jangwani.

Tumekuwa tukifuatilia malipo yetu tangu mwaka 2017 hadi leo bado hatujalipwa. Tumefuatilia fidia zetu kwa Mkurugenzi Tanesco, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, pamoja na kwa Katibu Mkuu Hazina, lakini hatujalipwa.

Tunaomba tulipwe kwani tumehangaika sana kudai haki yetu. Tumekwenda katika ofisi nyingi lakini hatujafanikiwa, tunakuja kwako utusaidie kutufikishia kilio chetu kwa Rais John Magufuli, kwani watendaji wake wameshindwa kutusaidia.

Mbali na hilo, sisi wakazi wa kata hizo tunasumbuliwa na kero ya utiririshaji wa maji machafu kutoka mradi wa Dawasco kata ya Upanga Magharibi.

**Iddi Funndi Osama,**
**Katibu wa Kamati ya Mazingira na Maji ya Mvua Kata ya Mchikichini, Jangwani, Upanga Magharibi, Dar**

## *Tuyalinde mazingira ya Tandale*

**Mhariri habari**

NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lililo na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.

Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisaidia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.

Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.

Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.

Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.

**Raia Mwema-Tandale**

# Sauti ya Masauni ichochee utii wa haki za binadamu

**Na Emmanuel Mbise, ARUSHA**




TAMKO la Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yusuph Masauni, alilolitoa bungeni hivi karibuni kuwa askari polisi hawapaswi kuwapiga watuhumiwa wanapokuwa chini ya ulinzi wao, ni habari njema kwa wapenda haki hapa nchini.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi ambazo baadhi ya raia wake wamelalamikia kupigwa, kuteswa na kunyanyaswa wakiwa mikononi mwa polisi.

Kauli ya Masauni ilitokana na swali na Mbunge wa Chonga (CUF), Mohamed Juma Khatibu, aliyetaka kujua ni katika mazingira gani polisi analazimika kumpiga mtuhumiwa.

Akinukuu kanuni za kudumu za utendaji kazi wa polisi, Masauni akasema askari polisi hapaswi kumpiga au kumtesa mtuhumiwa na kuwa inapobainika hivyo polisi huyo anapaswa kufikishwa mahakamani kwa kukiuka taratibu zake za kazi.

Wakati Masauni akijibu hivyo, ni ukweli kwamba katika baadhi ya maeneo ya nchi kuna malalamiko yanayohusu unyanyasaji na mateso wanayoyofanya walinzi hao wa amani dhidi ya raia wa kawaida.

Taarifa zaidi zimekuwa zikiripotiwa hadi kuhusisha watuhumiwa wengine kupoteza maisha wakiwa mikononi mwa polisi. Hilo si jambo jema hata kidogo.

Tamko la Masauni limenishawishi kujadili kuhusu utesaji, unyanyasaji na ukiukwaji wa taratibu za ukamataji kulingana na watuhumiwa.

Ipo mifano ambayo polisi wamekuwa wakilalamikiwa kuwatesa, kuwapiga, kuwaumiza kimwili na kisaikolojia watuhumiwa.

Hivi majuzi tu, iliripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa mwili wa marehemu Hilary Shirima (19) ambao uko katika chumba cha kuhifadhia maiti katika moja ya hospitali ya mkoa hapa nchini, umesusiwa na ndugu zake kwa madai kuwa alipigwa na polisi.

Madai ambayo yanapingana na taarifa iliyotolewa na polisi ambayo ilitaja chanzo kuwa ni matumizi ya dawa za kulevya.

Zipo taarifa za awali zilizokariri madai kwamba Shirima alipigwa na tajiri yake aliyekuwa akimuuzia duka kwa madai ya kusababisha hasara.

Zipo pia kesi nyingi zinazohusisha watuhumiwa kukiri makosa baada ya kushurutishwa, kupigwa, kuteswa na polisi.

Si rahisi kujua malengo ya polisi wasiokuwa waadilifu kuwapiga na kuwatesa watuhumiwa, lakini huenda wanafanya hivyo ili kuwashurutisha ama wakiri makosa yao, hasira, msongo wa mawazo na kazi kubwa wanayoipata kuwatafuta watuhumiwa hadi kuwapata.

Kuna maswali mengi ya kujiuliza, miongoni mwa hayo ni, hivi askari polisi hasa wa idara ya upelelezi, hawana mbinu mbadala za kupata taarifa kutoka kwa watuhumiwa hadi wawapige, kuwatesa ama kuwajeruhi?

Katika mazingira ya kawaida ni nani ambaye yuko tayari kuendelea kuteswa na polisi wanaotaka kusikia ukikiri kosa ili wamalize kazi yao na kuikabidhi mahakama watuhumiwa?

Kama hali ndivyo, kwamba mtuhumiwa ananyanyaswa na kuteswa ili akiri kosa na kufikishwa mahakamani, basi mbinu hiyo inapaswa kubadilishwa kwa sababu haisaidii katika kutenda haki ndani ya taifa linaloheshimu misingi ya utawala bora na utawala wa sheria.

Inaweza kuaminika kwamba si jambo jema kuzitaja mbinu zinazotumiwa na polisi kukusanya ushahidi, lakini ukisoma vitabu na taarifa za tasnia hiyo kwa nchi nyingine hasa zilizoendelea, wakusanya ushahidi wanafundishwa stadi zisizohusisha mateso na unyanyasaji wa mtuhumiwa.

Pamoja na changamoto katika kuzipa, kuzitumia na kuziendeleza stadi na mbinu za kupata taarifa, kuna changamoto nyingine zinazowakabili askari wetu hao. Nyingine zimeshaandikwa na kutangazwa kwenye vyombo vya habari.

Sababu kama ya kufanya kazi kwenye eneo moja kwa muda mrefu, inaelezwa kumfanya mtu asiwe mbunifu katika utendaji kazi wake.

Pia kuna suala la kipato kidogo halali ambalo linasababisha utegemezi kwa vipato vya nje, hivyo inawezekana hali kama hiyo ikasababisha utesaji, unyanyasaji, upigaji watuhumiwa pengine kwa kushawishi watuhumiwa kutoa rushwa.

Itakumbukwa kwamba hata wanasiasa wawili waliotoka gerezani hivi karibuni, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na Mbunge wa Tarime, Ester Matiko, walidai kupewa malalamiko kutoka kwa mahabusu wanaodai kuwa na kesi za kusingiziwa, zisizo na ushahidi na ndio maana `zinakaa' muda mrefu kukamilika.

Inastahili kwa polisi kutambua kwamba pamoja na kutii maadili ya kazi zao, lakini kuna hasara kwa taifa pale mtuhumiwa anapowekwa mahabusu kwa shinikizo zinazotokana na mateso na unyanyasaji, ingawa pia ni kinyume cha haki za binadamu.

Kutesa kunafanya watuhumiwa kuwa kama wamehukumiwa wakiwa mikononi mwa polisi. Hata kama wakija kuachiwa huru na mahakama adhabu wanayokuwa wamepata ni kifungo tosha.

Mahakama ndio mhimili pekee unaotarajiwa kutoa haki. Polisi waisikilize sauti ya Masauni, kwamba wanapaswa kutimiza wajibu kwa kufuata maadili, sheria za nchi na kanuni zinazowaongoza.

Na kutokana na hali hiyo, ninashawishika kuziasa mahakama zetu kuhakikisha watuhumiwa wanaoshtakiwa na kufikishwa huko, wanapata haki wanazozistahili.

Endapo mahakama zitajiingiza katika mtego unatokana na vitendo vya unyanyasaji na mateso, watu watakosa imani. Ipo hatari watu wasio na hatia kufungwa maisha ama kunyongwa.

Kwa kuandika hivi sina maana mahakama ziwe zinawaachia huru washtakiwa hata kama wana makosa, la hasha. Bali zisaidie kuitafuta haki, zipembue kwa kina ukweli wa mashauri wanayofikishiwa.

Hata wanapobaini uzembe katika mchakato unaowafikisha watuhumiwa mahakamani, waendelee kukemea kama inavyoonekana mara kadhaa wakitimiza wajibu huo.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

## HABARI KITAIFA

# Korosho moto bungeni

INATOKA UK 2

guzi utakaofanyika, pia uangalie ubora wa korosho zilizohifadhiwa kwenye maghala, akidai kuwa zikikaa zaidi ya miezi sita haziwezi kuwa salama.

Alilieleza kuwa jimboni kwake kuna vyama vya ushirika 11 na wakulima 1,281, lakini hakuna aliyelipwa licha ya taarifa kueleza kuwa wamelipwa.

"Watu waliofanya ovyo wanajulikana na kama wasipochukua hatua wenyewe, wasipofanya, tutaleta kusudio jinsi walivyofanya mmoja mmoja na jinsi ambavyo wanatakiwa kuchukua hatua kwa sababu waliyoyafanya ni kuhujumu, korosho, wananchi pia ni kuhujumu uchumi wa nchi.

"Hivi tunavyoongea Mheshimiwa Spika, bahati mbaya zoezi lilikuwa na dhuluma, lilikuwa na rushwa, lilikumbwa na ubabaishaji mwingi na uongo mwingi sana.

Nnauye pia aliitaka serikali kuipeleka bungeni Sheria ya Korosho ili ifumuliwe kwa kuwa imekuwa chungu kwa wakulima wa zao hilo.

"Kile kipengele tulichokinyofoa kimetuletea shida sana, sasa leteni sheria yote tuipitie. "Napendekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aende kukagua, atuletee ripoti hapa ndani namna zoezi lililovyoenda ili tuchukue hatua ya kuziba mapengo.

"Kama nilivyosema, Rais wengi wamemdanganya, sasa ni vizuri wawajibike na Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukawa 'specific', si sahihi kuiingiza serikali katika mambo yaliyofanyika ovyo.

"Leo tukiulizana korosho yetu ipo wapi, haiwezi kukaa zaidi ya miezi sita hapa nchini ikabaki salama, mngetuambia kuna korosho sahihi, huu ni uongo na tukiendelea kuusema huu uongo na bado tunaendelea kubaki hatutabaki salama," Nnauye alisema.

**MNYIKA, SELASINI**

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), alimwomba Rais John Magufuli alivunje Baraza la Mawaziri, akidai kuwa limemshauri vibaya katika suala la korosho.

Mnyika ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Tanzania Bara, alisema Baraza la Mawaziri linatakiwa kuwajibishwa kwa kumshauri vibaya Rais katika suala la korosho, akilieleza Bunge kuwa korosho sasa zinaoza kutokana na kukosekana kwa wanunuzi.

Hoja hiyo ya Mnyika kuhusu kuharibika kwa korosho, iliungwa mkono na Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini (Chadema), ambaye alimshauri Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuunda kamati ya wabunge wachache ikague maghala ya kuhifadhi korosho ili kubaini kama zimeoza au bado ziko salama.

Huku akimsifu Spika Ndugai kwa kuunda kamati zilizochunguza masuala mbalimbali yakiwamo ya madini ya tanzanite, Selasini alisema: "Nimeitazama picha ya Rais akiwa ameshika paji la uso, anaonyesha kutafakari sana. Picha inamwonyesha kuzeeka kuliko alipoapishwa.

"Inaonekana Rais ana mawazo mengi. Kazi ya Bunge hili ni kuishauri serikali. Kazi ya Bunge hili ni kuisimamia serikali, tunafanya makosa makubwa sana kufanya siasa ndani ya Bunge hili.

"Nimetangulia kukusifu Spika, kama kuna ubishi wa korosho zimeoza ama hazijaoza, tengeneza

INAENDELEA UK.26




Kiongozi Mkuu wa Waislamu Shia Ithnasheriya Tanzania, Maulana Sheikh Hemed Jalala, akizungumza na wajane wa Kata ya Kigogo katika semina ya kumbukumbu ya kifo cha Bi. Khadija (A.S) ambaye ni Mke wa Mtume Muhammad (S.A.W.W) pamoja na kushiriki futari ya pamoja, iliyoandaliwa na kitengo cha kinamama wa Chuo cha Imam Swadiq (A.S), iliyofanyika Masjid Ghadir Kigogo Post, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanaharakati Chadema aweka msimamo

INATOKA UK 4

taka ni uchunguzi huru, tunaweza kuita shirika lolote lililobobea kwenye uchunguzi lije kuchunguza tukio hili," alisema.

Wakati akisimulia tukio hilo, mwanaharakati huyo alijikuta akilia na kueleza kuwa alitekwa na kundi la watu waliokuwa kati ya wanane na tisa wakiwa na silaha na magari wawili aina ya Land Cruiser na Nissan Patrol, moja likiwa halina namba na walimpiga hasa kichwani.

Alisema watekaji hao walimpiga kipigo ambacho hakuwahi kupigwa licha ya matukio kadhaa kumkuta awali.

Mdude alidai kuwa tukio hilo ni la utekaji kwa sababu eneo alilochukuliwa ni mwenyeji na ameishi hapo zaidi ya miaka 20 hata akitembea akiwa amefumba macho anajua anakokwenda.

"Kutekwa kwangu kunahusiana na masuala ya siasa kwa sababu ya itikadi yangu. Mimi ni Chadema na ni kiongozi wa kanda, mimi ni Ofisa Mafunzo na Oganizesheni Kanda ya Nyasa ambayo ina mikoa mitano na Mwenyekiti wa Kanda ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Katibu wa Kanda ni Emmanuel Masonga," alisema.

Mdude alibainisha kuwa jambo ambalo limesababisha atekwe ni kutokana na misi

INAENDELEA UK 26

# IFAD yaimwagia Tanzania bil. 127/-

INATOKA UK.3

serikali yake kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kukuza uchumi.

Kiongozi huyo pia alipongeza utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na IFAD, kutilia mkazo umuhimu wa uwekezaji usiokuwa tegemezi, unaolinda utu, unaozalisha kipato kwa wananchi na unaojenga misingi endelevu ya kujitegemea.

Alibainisha kuwa baada ya kutenga fedha hizo, IFAD inaisubiri Tanzania kuainisha maeneo mahsusi ya miradi ya kilimo ambayo fedha zitaelekezwa na alieleza kuwa ana matumaini miradi hiyo itafanikiwa kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi yenye amani na serikali ilivyo na dhamira ya maendeleo.

Taarifa hiyo ilisema Rais Magufuli aliishukuru IFAD kwa ushirikiano wake mzuri na Tanzania na kumhakikishia Houngbo kuwa ushirikiano na uhusiano huo ulioanza mwaka 1978 utadumishwa kwa maslahi ya Watanzania.

Rais Magufuli, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alisema fedha zilizotengwa katika mpango huo wa miaka mitatu zitaelekezwa katika maeneo yenye maslahi mapana ya sekta ya kilimo ikiwamo kuwezesha matumizi ya zana bora za kilimo katika uzalishaji.

Aliyataja maeneo mengine kuwa ni kuzalisha mbegu bora za mazao, kutatua changamoto ya masoko ya mazao, kuboresha ufugaji na aliishukuru IFAD kwa kutoa fedha pasipo masharti ya maeneo zinakopaswa kuelekezwa.

Rais Magufuli aliiagiza Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa kuainisha maeneo yatakayopokea fedha hizo ili utekelezaji wa mpango huo uanze.

**IN THE HIGHT COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO. 41 OF 2017**

JOSEPH JUMA BIGAZI....................................PLAINTIFF
VERSUS
SIMON JOHN MALIMBO.................................1ST DEFENDANT
KERVIN JOSHUA..........................................2ND DEFENDANT
BW. SAJAD HABIB RAI.................................3RD DEFENDANT

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION.**

**TO:**
**SIMON JOHN MALIMBO,**
**DAR ES SALAAM.**
**KERVIN JOSHUA,**
**DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has filed a suit against you with particulars set out in the plaint filed in this Court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication.

You are directed to collect copies of the summons and plaint from the Court's Registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 18th day of June, 2019 at 2:30 pm when this case will be heard.

**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default to enter appearance on the day and time mentioned above, the suit will proceed and a decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 8th day of May, 2019.

DEPUTY REGISTRAR

215239502

HABARI KITAIFA

## Wahitimu kidato cha sita waelezwa siri mafanikio

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANAFUNZI waliohitimu kidato cha sita mwaka huu, wametakiwa kuepuka masuala yanayoweza kuchangia kuharibu ndoto zao za kimaisha ikiwamo kushiriki katika anasa na starehe.

Badala yake wametakiwa kujilinda na kuwa wavumilivu hadi ndoto zao zitakapotimia.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Mkombozi, Mwaka Mwabulambo, wakati akizungumza katika mahafali ya kidato cha sita katika shule za sekondari za Kaizirege na Kemebos katika Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera.

Mwabulambo alisema kuwa anasa na starehe na vitendo visivyofaa kama matumizi ya dawa za kulevya na biashara ya ngono havifai katika jamii na vinawafanya vijana kupoteza mwelekeo kimaisha, na kuwataka wanafunzi hao wanaporudi nyumbani kuwa raia wema, ili kuifanya jamii kuendelea kuwa na ustawi.

"Soko la ajira linawasubiri, kwa hiyo mnapaswa kusoma kwa bidii, maana matarajio ya waajiri ni kupata wasomi wanaojitambua, ambao wataweza kufanya kazi kwa bidii na kujenga uhusiano mwema na watu wengine kwa manufaa ya waajiri na taifa kwa ujumla.

Alisema uwapo wa taasisi zinazotoa elimu kusaidia wananchi kukabiliana na changamoto za kiuchumi kwa kutoa elimu inayoweza kuwasaidia wahusika kupata ajira ndani na nje ya nchi, ni msaada mkubwa kwa wananchi na serikali katika kuandaa taifa la wasomi wenye sifa zinazostahili.

"Sisi kama taasisi za kifedha, tuko tayari kushirikiana na serikali na taasisi za kielimu, ili kuhakikisha watoto wanatengenezewa mazingira bora ya kujifunzia, yatakayowezesha kupatikana kwa wataalamu wenye sifa, watakaoshirikiana na serikali kuwezesha kufikia uchumi wa kati kupitia sera ya sasa ya viwanda," alisema.

Akizungumza katika mahafali hayo yaliyowahitimisha watoto 134, Meneja wa Shule za Kemebos na Kaizirege, Eurogius Katiti, aliwataka watoto hao kuongeza jitihada katika masomo badala ya kuendekeza starehe, maana safari yao ya kuelekea katika mafanikio ndio imeanza.

# Sababu mkataba TBA, halmashauri kuvunjwa

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

HALMASHAURI ya Mji wa Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe, imevunja mkataba na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wa kujenga hospitali ya wilaya.

Hatua hiyo imetokana na serikali kutoa shilingi bilioni tatu kukamilisha ujenzi huo, lakini ukatekelezwa kwa kusuasua.

Wakazi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma wanategemea kupata tiba kwenye Kituo cha Afya cha Tunduma ambacho kimekuwa kikielemewa kutokana na wingi wa watu wanaotoka maeneo mbalimbali ikiwamo nchi jirani ya Zambia kupata tiba.

**serikali ina nia njema na wananchi wake, lakini kitendo cha TBA kufanya kazi za ujenzi kwa kusuasua kimewapa hofu mradi kutokamilika kwa muda uliopangwa.**

Regina Bieda, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, hivi karibuni alisema serikali ilitoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, lakini TBA ambayo imepewa zabuni ya ujenzi huo. inasuasua hali inayowapa hofu ya kuukamilisha mradi huo kwa muda mwafaka.

"Kutokana na hali hiyo, walikaa vikao vya halmashauri kujadili hatima ya ujenzi huo, ikatulazimu kutoa notice (taarifa) ili kamati ya ujenzi imkabidhi kiongozi wa ujenzi huo wasimame ili kutangaza tenda ya kumpata mkandarasi mwingine atakayeweza kuujenga mradi huo kwa muda mwafaka," alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ally Mwafongo, alisema serikali ina nia njema na wananchi wake, lakini kitendo cha TBA kufanya kazi za ujenzi kwa kusuasua kimewapa hofu mradi kutokamilika kwa muda uliopangwa.

Mwafongo alisema TBA ilipewa kazi hiyo toka mwaka jana, lakini imekuwa ikishindwa kuheshimu mkataba licha ya kuwaongezea muda mara kadhaa, hivyo wameandikia barua ya kusitisha mkataba na kampuni hiyo ili ipewe kampuni nyingine kunusuru fedha kurudi hazina kuu.

Hivi karibuni, Katibu Tawala mkoani Songwe, David Kafulila, alisitisha mkataba wa ujenzi wa nyumba ya mkuu wa mkoa na ya katibu tawala zilizokuwa zikijengwa na TBA kwa madai ya kusuasua kwa ujenzi ikihofiwa fedha kurejeshwa hazina kuu.




Naibu Mkurugenzi wa Kampuni ya Halotel, Nguyen Tien Dung, akiongea na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa huduma ya Halopesa Visa on Mobile, katika makao makuu ya ofisi za Halotel, jijini Dar es Salaam. Huduma hiyo itawawezesha wateja wote kulipia bidhaa, au kufanya miamala ya kifedha kupitia Visa. Kushoto ni Mkurugenzi wa Visa nchini, Olive Njoroge, kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Halopesa, Magesa Wandwi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri awapa saa 14 makandarasi

**Na Dege Masoli,** MKINGA



WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (pichani), amewapa saa 14 makandarasi kuwasilisha maelezo yao kwake kwa nini wasinyang'anywe kazi hiyo kutokana na kutoridhishwa na kasi ya utekelezaji wa majukumu yao ya kuunganisha umeme vijijini.

Aidha, Waziri Kalemani alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kuchunguza sababu za ucheleweshaji wa mradi huo na kuwakata makandarasi hao asilimia 10 ikiwa ni sehemu ya adhabu dhidi yao.

Waziri Kalemani alitoa agizo hilo kwa makandarasi hao alipokuwa akizungumza na wakazi wa vijiji vya Kata ya Vuo wilayani Mkinga, ambapo alionyesha kutoridhishwa na kasi ya uunganishaji umeme katika vijiji vya wilayani humo.

Kampuni zinazopewa kazi ya kuunganisha umeme wilayani hapa ni ya JV Radi Service Ltd, Njarita Ltd na Aguila Ltd ambazo zimetakiwa kuwasilisha kwa waziri huyo maelezo ya kwanini wasiondolewe kwa kushindwa kuunganisha vijiji 19.

Alisema wizara yake haiwezi kuona makandarasi wakichelewesha kutoa huduma hiyo kwa wananchi wakati walisaini mkataba wa kufanya kazi hiyo kwa wakati.

Aliutaka uongozi wa REA kuhakikisha hadi ifikapo Juni 30, mwaka huu, yawe yameshawekwa magenge (kambi) katika vitongoji vya Vuo, Jirihini, Loko na Bajo ili Julai vijiji vyote viwe vimeshaunganishiwa umeme.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Emmanuel Yesaya, alisema atahakikisha umeme unafikishwa katika vijiji hivyo katika muda uliotolewa na Waziri Kalemani ili kutoa nafasi ya REA awamu nyingine ya tatu ya mradi huo uweze kuanza.

Naye Mbunge wa Mkinga, Dunstan Kitandula, alisema wilaya hiyo ina jumla ya vijiji 85 na vitongoji 335, vijiji 40 kati ya hivyo havijapata huduma ya umeme.

# Walimu 8,000 elimu maalum wahitajika

MAHITAJI ya walimu wa elimu maalumu nchini ni 8,882 katika shule maalum na vitengo vinavyopewa wanafunzi wenye mahitaji maalum 706, Bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Grace Tendega, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kuhakikisha kunakuwa na walimu wa kutosha kwa watu wenye ulemavu.

**serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu wa taaluma hiyo.**

Akijibu swali hilo, Manyanya alisema hadi Desemba, mwaka jana, walimu 5,556 wenye taaluma ya elimu maalum ngazi za astashahada, stashahada na shahada walihitimu katika vyuo mbalimbali nchini ikiwamo Chuo cha Ualimu Patandi na Chuo Kikuu Dodoma (Udom).

Hata hivyo, alisema ili kuhakikisha walimu wa kada hiyo wanapatikana kwa wingi, serikali imekamilisha upanuzi wa Chuo cha Ualimu Patandi ili kukiongezea uwezo wa kudahili.

"Pia chuo kimeanzisha kozi ya elimu maalum katika ngazi ya astashahada kwa walimu tarajali kwa mwaka wa masomo 2018/19. Hatua hii itaongeza idadi ya walimu wanaojiunga na mafunzo ya ualimu wa elimu maalum ili kupunguza changamoto ya walimu wenye taaluma hiyo wanaohitajika nchini," alisema.

Aidha, alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu wa taaluma hiyo.

Manyanya alisema changamoto hiyo inasababishwa na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu kutokana na mabadiliko chanya ya kimtazamo na uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watu hao.



Mtaalamu wa upishi wa bia za TBL, Calvin Nkya, akitoa maelezo kuhusiana na uzalishaji bia kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa wanafunzi wanajeshi kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi cha Nigeria walipotembelea kiwanda cha TBL cha Ilala jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**


# Ardhi yakumbwa na uhaba watumishi

NAIBU Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, amesema kuna upungufu wa watendaji 1,411 katika sekta ya ardhi nchini.

Mabula alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tunduru Kaskazini (CCM), Ramo Makani, ambaye alihoji ikama ya wataalamu wa ardhi katika halmashauri za wilaya ni ipi na lini wilaya ya Tunduru itafikia kiwango hicho.

"Je, ni lini serikali itatekeleza ahadi yake ya kurudisha eneo la ekari takribani 2,000 za shambapori la Nambarapi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili nayo irejeshe ardhi hiyo kwa wananchi wa vijiji husika kikiwamo cha Nambarapi?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mabula alisema mahitaji ya wataalamu hao ni 2,957 na kwamba kwa mujibu wa viwango vya kiutendaji vya mwaka 2016, ikama ya watumishi wa ardhi katika halmashauri za wilaya ni maofisa ardhi watatu, wapima ardhi watatu, maofisa mipango miji watatu, wathamini watatu na mafundi sanifu upimaji/maofisa ardhi wasaidizi wanne.




Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa sasa ina watumishi wanne wa sekta ya ardhi ambao ni maofisa mipango miji wawili, mpima ardhi mmoja na ofisa ardhi msaidizi mmoja.

"Serikali inaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuajiri watumishi wa sekta ya ardhi ili kufikia kiwango kinachohitajika, hivyo kuongeza ufanisi na wizara itawapanga upya watumishi wa sekta ya ardhi ili kuwa na uwiano wenye tija," alisema.

Alisema kwa sasa kuna upungufu wa watendaji kwenye sekta ya ardhi ambapo ilitakiwa nchi nzima wawe 2,957 na waliopo ni 1,546 hivyo upungufu ni 1,411.

Alifafanua kuwa shambapori lenye ekari takribani 2,000 linatambulika kama shamba Na. 69 Nambarapi na lina ukubwa wa hekta 744 (ekari 1,913).

Mabula alisema mwaka 2003 kulianza kujitokeza migogoro ya kugombea ardhi ya shamba hili hali iliyosababisha kufunguliwa kwa shauri Na. 03/2016 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Tunduru.

Pamoja na hayo, alisema shauri hilo lilikuwa kati ya Tamcu LTD dhidi ya wananchi wanne (Hassan Mussa Ismail, Ismail Mussa Ismail, Sophia Mussa Ismail na Said Ndekelo) na katika shauri hilo Chama cha Ushirika Wilaya ya Tunduru kilipata ushindi.

Alisema pamoja na ushindi wa TAMCU Ltd, wananchi wa kijiji cha Nambarapi waliomba ardhi katika shamba hilo na ekari 1,000 zilimegwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na kuigawa kwa wananchi.

## Lugola atuma salamu polisi

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameapa kuwa atakula sahani moja na askari polisi wenye tabia ya kukamata ovyo na kuziweka kwenye vituo pikipiki huku baadhi ya vifaa vyake vikipotea.

Lugola aliliambia Bunge jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rehema Migilla, ambaye alisema waendesha bodaboda wengi wanakamatwa na kubambikiwa makosa bila uchunguzi na kuambiwa walipe fedha, huku wakiaelezwa kuwa wasipotoa wanakuta pikipiki zao zimeondolewa baadhi ya vifaa.

"Tunataka hapa waziri atuambie hapa kama wanaotoa vifaa hivyo ni polisi na kama ni wao kwa nini wanafanya hivyo na serikali ina mpango gani kuwarudishia wananchi hao pikipiki zao ili zisiharibike,"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waziri Lugola alitaja baadhi ya makundi ambayo pikipiki zao zinatakiwa kukamatwa kuwa ni pamoja na ambaye pikipiki yake ilihusika kwenye uhalifu, kesi ya ajali au iliyoibwa na ambayo haina mwenyewe.

Alibainisha kuwa pikipiki zilizobaki zote ziwe hazina kofia ngumu 'helment', na vinginevyo hakuna itakayokamatwa bali upo utaratibu wa kutoa faini ndani ya siku saba.

"Hivyo kwa zile pilipiki zinazokamatwa huwa wanaandikiwa hati ya vilivyopo ili ikitokea vifaa kupotea aliyeichukua atawajibika,"alisema.

"Mwanzoni nilikuwa najiuliza kwa nini watu wanapoagiza magari vitu vinachomolewa ikiwa ni pamoja na pikipiki zilizopo vituo vya polisi," aliongeza.

Alimhakikishia Mbunge huyo kuwa ifikapo jioni (jana) kama kuna changamoto kama hiyo au kuna bodaboda yenye tatizo hilo katika wilaya yake atalishughulikia na kama kuna pikipiki iko kituoni na ina tatizo la vifaa kupotea atakula sahani moja na polisi.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema pamoja na jitihada za vijana wengi kujiajiri kuendesha pikipiki wamekuwa wakisumbuliwa na polisi kwa kukamatwa mara kwa mara.

"Kwa nini wanapokamatwa pikipiki zao na polisi wanapoenda kuzichukua hukuta baadhi ya vifaa kama betri hazipo,"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hamad Yusuph Masauni alisema sheria ya usalama barabarani sura ya 168 iliyorejewa mwaka 2002 inampa mamlaka askari polisi kusimamisha chombo chochote barabarani na kukikagua kubaini kama kina makosa na hatimaye kukizuia au kukamata.

"Chombo cha moto kinapokamatwa hutunzwa kituoni kwa mujibu wa mwongozo wa Jeshi la Polisi Namba 229 na inapotokea kielelezo kimeharibiwa uchunguzi hufanyika na hatua kuchukuliwa kwa waliohusika na upotevu huo,"alisema.

# Wanahisa benki CRDB wamkumbuka Dk. Mengi

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WANAHISA wa benki ya CRDB walimtaja aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, kuwa alifanikisha kwa kiwango cha juu kuanzishwa kwa benki hiyo mwaka 1996.

Hayo yalibainishwa katika mkutano wa 24 wa wanahisa wa benki hiyo jijini hapa mwishoni mwa wiki.

Dk. Mengi alifariki dunia mapema mwezi huu Dubai na kuzikwa wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

Wanahisa hao walisimama kwa dakika moja, kumkumbuka Dk. Mengi ambaye alitoa mchango mkubwa kwa taifa wakati wa uhai wake.

Mmoja kati ya wanahisa, Beno Nkoswe, alisema umuhimu wa Dk. Mengi katika uanzishaji wa benki ulikuwa mkubwa.

"Tulikuwa watu kama saba hivyo tukiendesha vikao vya uanzishwaji wa benki hii, pale katika hoteli ya Starlight Dar es Salaam, kuna kipindi tulikata tamaa katika kukamilisha taratibu za Benki Kuu, hasa zilikuwa zinahitaji fedha kama dhamana kabla ya kupewa kibali cha kuanza shughuli, lakini Mengi alikuwa anaokoa jahazi dakika za mwisho," alieleza.

**Kwa kweli wenzangu waliokuwapo akiwamo Prof. Simon Mbilinyi, watakumbuka tulipokwama kupata fedha na hata mfadhili wetu mkuu alipoongeza, bado kiasi cha fedha hakikutimia mpaka Mengi aliposaidia na ndipo benki hii kubwa zaidi nchini ilipoanza kazi.**

Nkoswe alisema wakati benki hiyo ikipongezwa kwa mafanikio makubwa ya kupanuka katika kipindi cha miaka yake 23, ni vyema katika historia kumkumbuka Dk. Mengi aliyekuwa mmoja wa kati ya watu waliotoa mchango mkubwa, hadi benki hiyo ikasajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

"Kwa kweli wenzangu waliokuwapo akiwamo Prof. Simon Mbilinyi, watakumbuka tulipokwama kupata fedha na hata mfadhili wetu mkuu alipoongeza, bado kiasi cha fedha hakikutimia mpaka Mengi aliposaidia na ndipo benki hii kubwa zaidi nchini ilipoanza kazi," alisema.

Katika hatua nyingine aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo,

Dk. Charles Kimei, aliwaaga rasmi wanahisa baada ya kuitumikia benki hiyo kwa miaka 22 wakati wa mkutano huo.

Dk. Kimei aliteuliwa kuiongoza benki hiyo mwaka mmoja, mara baada ya kuanzishwa kwake miaka 23 iliyopita.

Akizungumza wakati akiwaaga wanahisa hao, Dk. Kimei alisema benki hiyo imepata mafanikio makubwa katika uendeshaji wa biashara, licha ya kuwapo kwa mitikisiko ya mara kwa mara ya kiuchumi.

Aliwaeleza wanahisa kwamba pamoja na mitikisiko hiyo, lakini benki hiyo ilisimama imara.

Baadhi ya wanahisa akiwamo Mwenyekiti wa mkutano huo, Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Askofu Brigedia Jenerali, Augustino Ramadhani, alimpongeza Dk. Kimei kwa kusimamia benki hiyo kwa mafanikio makubwa.

Aidha, alimtaka Dk. Kimei kuendelea kuisaidia benki hiyo na kutoa ushirikiano na ushauri wa mara kwa mara.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Musa Nsekela, alisema benki hiyo imeingia katika mikataba mikubwa, ikiwamo ya uchimbaji wa gesi, viwanda vya sukari, nishati, kilimo na viwanda.

Alisema benki hiyo imewekeza kwa wanahisa ambao ndiyo walionunua hisa za zaidi ya Sh. bilioni 800.



Katibu wa Jukwaa la Uwezeshaji Mkoa wa Pwani, Elina Mgonja (kushoto), akiendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo kwa wanawake wanaofaidika na mikopo inayotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Global Together kutoka Korea Kusini kwa kushirikiana na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Shirika la Elimu Kibaha (KEC SACCOS Ltd), mjini Kibaha, mkoani Pwani. **NA ICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waweka mikakati ya ikolojia ya Serengeti

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WADAU wa ikolojia ya Serengeti Mara inayoziunganisha Tanzania na Kenya wameanza utekelezaji wa mradi wa miaka miwili wa kuboresha ushirikiano, usimamizi wa sheria za kudhibiti ujangili kwa kushirikisha jamii.

Mradi huo wa miaka miwili unaofahamika kama uhifadhi wa mazingira ya Serengeti-Mara (SEMA), unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya kwa Euro 856,000 (zaidi ya Sh. bilioni 2.1) ambapo utakamilika mwaka 2020.

Meneja wa programu wa mradi huo, Amani Shipella, akizungumza katika mkutano wa wadau wa mkakati wa wanyamapori katika ikolojia ya Serengeti Mara, alisema mradi huo pia umelenga kukomesha migogoro kati ya wanyamapori na wananchi.

Pia watajenga uwezo wa kutumia sheria ya uhifadhi wa wanyamapori na kuhakikisha rasilimali zinazopatikana zinatumika kwa manufaa ya jamii zinazozunguka ikolojia hizo.

"Utekelezaji wa mpango wa mradi huo ni kuondoa migogoro katika ikolojia hiyo inayohusisha hifadhi za Taifa ya Serengeti nchini na Maasai Mara nchini Kenya kwa jamii kujengewa uwezo wa shughuli za kiuchumi, huku ikishiriki katika ulinzi wa wanyamapori," alisema.

Shipella alisema ikolojia ya Serengeti Mara ni eneo muhimu kwa uhifadhi, lenye hadhi ya kimataifa, na ni la kujivumia kwa nchi za Kenya na Tanzania, kwa vile lina fursa nyingi za kiuchumi, hivyo litakuwa na manufaa endapo changamoto mbalimbali zitatatuliwa.

Alisema kuwa mradi huo unatekelezwa kwenye eneo lenye jamii fukara na migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, kuzunguka hifadhi hizo mbili.

Shipella aliwataja walengwa ni wakulima wadogo, hasa wanawake na vijana, mashirika ya wakulima, sekta ya umma na binafsi na taasisi za utafiti katika Wilaya za Tarime, Bunda na Serengeti na Kaunti ya Narok na Bomet nchini Kenya.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa eneo la Afrika ya Mashariki wa asasi isiyokuwa ya kiserikali ya Vi Agroforestry inayoratibu mradi huo, Lena Kalmelid, alisema migogoro kati ya wanyamapori na binadamu imeelezwa ni changamoto kubwa inayoikabili ikolojia ya Serengeti-Maasai Mara, ambapo jamii inawachukulia wanyamapori kama maadui wakubwa na si rasilimali.

# Ufugaji wa kisasa wanufaisha maelfu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFUGAJI zaidi ya 9,000 wa mikoa ya Arusha, Tanga, Mwanza na Dar es Salaam, wanatarajiwa kunufaika na elimu ya ufugaji bora wa kisasa, utakaowakwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa kikao cha kuweka mikakati ya kuwafikia wafugaji hao kupitia elimu kwa njia ya redio, ofisa mradi wa Shirika la Radio kwa wakulima, Eliakunda Urio, alisema wamekuwa wakifanya kazi na wakulima na wafugaji kwenye maeneo ya mradi kuhakikisha makundi hayo yanafikia malengo yao kwa kupata elimu bora.

Alisema wamefikia hatua ya kutumia vyombo vya habari kwa sababu ni nyenzo muhimu inayoweza kutatua changamoto ya uhaba wa wataalamu wa maofisa ugani inayowakabili wakulima na wafugaji nchini, kwa kuandaa vipindi vinavyotoa fursa kwa walengwa kuwasiliana moja kwa moja na wataalamu.

Naye Ofisa Msaidizi Kitengo cha Radio ya shirika hilo, Clara Moita,

alisema elimu hiyo inatolewa kupitia mradi wa miezi sita wa afya ya mifugo, ambapo wamekuwa wakitoa mafunzo kwa waandaaji wa vipindi kabla ya kuanza kutekelezwa kwa vipindi hivyo kwa wakulima.

Clara alisema elimu hiyo imekuwa ikileta mafanikio makubwa, kutokana na kuwafikia wakulima wengi, hasa waliopo vijijini na kwa wakati mmoja na hatimaye kuongeza pato kutokana na kufuga na kulima kisasa.

Naye mfugaji wa kuku kutoka Nyamagana, mkoani Mwanza, Betty Masumbigana, alisema wamekuwa wakikabiliana na changamoto nyingi katika ufugaji wao, ikiwamo magonjwa yanayoshambulia mifugo mara kwa mara, hivyo kupitia vipindi hivyo, wameona manufaa makubwa.

# Madiwani wahofu kutoweka kwa WEO

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, limehoji taarifa za 'kutoweka' kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kimochi (WEO), Ramadhan Mfinanga, katika kituo chake cha kazi kwa muda sasa, huku likitaka mamlaka husika kuchukua hatua.

Aliyeibua taarifa za kutoweka katika kituo cha kazi na kutaka kutolewa taarifa rasmi ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ni Diwani wa Kata ya Arusha Chini, Rodgers Mmari.

"Mheshimiwa Mwenyekiti (Michael Kilawila), kabla ya kuthibitisha muhtasari wa kikao chetu cha kawaida cha Baraza la Madiwani na viongozi wa vyombo vyetu vya usalama wako hapa, tunaomba tupate taarifa za kuhusu suala la Mtendaji wa Kata ya Kimochi kama ameenda kwenye kazi maalum au ni utoro," alihoji Mmari.

**Si kwamba amepotea, anaonekana huko mitaani, inawezekana nyie mnamtafuta kwa barua, lakini hata hela bado zilikuwa zinakuja ofisini.**

Baada ya kauli hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Castory Msigala, alisema ni kweli wanazo taarifa za kutoonekana katika kituo cha kazi mtendaji huyo na kwamba wamemtafuta mara kadhaa, lakini hapatikani.

"Ni kweli Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba mtendaji wetu hajapatikana mpaka sasa na tunajiandaa kuchukua hatua," alieleza Msigala.

Diwani wa Kata ya Kimochi, Eufemia Massam, akichangia kuhusu kutoonekana kwa mtendaji huyo, alisema si kweli kwamba haonekani mtumishi huyo, isipokuwa anaonekana mitaani.

"Si kwamba amepotea, anaonekana huko mitaani, inawezekana nyie mnamtafuta kwa barua, lakini hata hela bado zilikuwa zinakuja ofisini," alisema Massam.

Akihitimisha mjadala kuhusu kutoonekana kwa mtendaji huyo wa kata, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Michael Kilawila, alisema licha ya kupokea taarifa za utoro za ofisa huyo ni lazima mwajiri wake achukue hatua stahiki za kuziarifu mamlaka nyingine.




Mmoja ya wahitimu wa kozi ya wiki mbili ya masuala mbalimbali ya uhifadhi na utalii wa Mlima Kilimanjaro na Meru, akifurahia cheti chake, baada ya kuhitimu katika Chuo Cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori cha Mweka (CAWM), mkoani Kilimanjaro. Mafunzo hayo yalitolewa bure kwa wapagazi (tour porters) na chuo hicho, kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo UNDP). **PICHA: JAMES LANKA**

# Walilia soko la kimataifa la mboga, nafaka

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAWAKE wajasiriamali Mkoa wa Kilimanjaro, wameomba kujengwa soko la kimataifa la mboga na nafaka katika eneo la Lokolova Halmashauri ya Moshi ili kuweza kukuza biashara zao na uchumi wa mkoa wao.

Wakizungumza na Nipashe wakatiwa uzinduzi wa jukwaa la wanawake wajasiriamali na wakulima katika kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi, Anifa Koshuma, alisema kukosekana soko la kuaminika la mboga, matunda na nafaka kunachangia kushindwa kujikimu kimaisha.

"Ni kweli katika Mkoa wa Kilimanjaro kulikuwapo na taarifa za ujenzi wa soko la kimataifa la mboga, matunda na nafaka (Lokolova), lakini hadi kufikia sasa hatujui kilichoendelea ... tunaiomba serikali ya mkoa na wizara husika kuangalia namna ya kutusaidia ujenzi wa soko hilo," alisema na kuongeza:

"Ikiwa serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wizara husika watafuata sera ya rais ya uchumi wa kati kwa kuhakikisha wanafufua viwanda vilivyokufa na kujenga vipya.. pia mamlaka hizo ziangalie namna bora ya kuhakikisha soko hilo linajengwa ili wakulima wapate soko la uhakika," alisema Mwanaisha Omary.

Alisema hali ya masoko ya bidhaa za kilimo kwa sasa siyo ya kuridhisha kutokana na bei iliyopo sokoni kuwa chini na kusababisha wajasiriamali waliochukua mikopo kwenye taasisi za kifedha kushindwa kurejesha kwa wakati. Mgeni Ramadhani, alisema wakulima kwa sasa wamekata tamaa na kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutengua zuio la usafirishaji wa mazao ya kilimo ambayo hayajaongezewa thamani kwenda nje ya nchi kutokana na chakula kilichopo nchini kutosheleza mahitaji ya Watanzania.

"Kwa sasa tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutoa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi ili wakulima waweze kunufaika na kurejesha mikopo katika taasisi za kifedha," alisema Ramadhani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Manispaa ya Moshi, Rose Minja, alisema serikali imefuta riba kwa mikopo inayotolewa na halmashauri ili kuongeza thamani mazao ya mashambani kwa kuanzisha viwanda vidogo kwa lengo la kuuza bidhaa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aidha, Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu, Mkoa wa Kilimanjaro, Lyidia Riwa, alisema kwa sasa hawawezi kuzungumzia suala la soko hilo kwa kuwa lipo ngazi za juu.

"Ninachofahamu ni kuwa yapo mambo madogo madogo yakukamilisha ili ujenzi huo uanze," alisema Riwa.

Hata hivyo, Nipashe ilimtafuta Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Joseph Kakunda, kwa njia ya simu ili kutoa ufafanuzi wa hatima ya soko hilo na kusema hana taarifa zozote za ujenzi wa soko hilo kwa sasa na kuahidi kulifanyia kazi mara zitakapofika ofisini mwake.

"Hayo masoko yapo ndani ya halmashauri na mkoa husika ndio wasimamizi wakubwa wa miradi hiyo... lakini ikiwa kuna mahali wamekwama walete taarifa hiyo wizarani kwangu na tutaona namna ya kuongeza nguvu ili kusaidia kuondokana na changamoto hiyo," alisema.

# Aiomba serikali kukarabati samani za hospitali

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATANZANIA wenye uzalendo na ujuzi wa kuisaidia jamii wametakiwa kuwekeza nguvu zao hasa katika sekta ya afya ili kuisaidia serikali katika uboreshaji wa miundombinu ya sekta hiyo.

Aidha, Watanzania wenye karakana zenye uwezo wa kukarabati vifaa na miundombinu katika sekta ya afya wameombwa kujitokeza kufanya kazi za kizalendo kama sehemu ya mchango wao katika maendeleo ya nchi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, Japhet Boniface, alisema hayo wakati akipokea vitanda viwili na kiti mwendo kimoja vilivyokarabatiwa na mmoja wa wazalendo mkoani hapa.

"Huu ni mfano dhahiri, mwenzetu ambaye ni fundi, imempendeza amekarabati vitanda na viti mwendo bila malipo kutoka serikalini, huu ni mfano wa kuigwa," alisema.

Vitanda hivyo vilivyopo katika hospitali hiyo vilitolewa kwenye vyumba mbalimbali ili kuhakikisha vinatumika kuwahudumia wagonjwa. Japhet alisema kuwa Watanzania wazalendo wenye ujuzi ikiwa watajitokeza kusaidia sekta ya afya, kuleta unafuu wakati wa utoaji wa huduma.

"Mhandisi Fadhili Athuman, alifika katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi na kukuta shehena ya vitu chakavu, aliomba kuvifanyia kazi na tulimpa vitanda viwili na kiti mwendo kimoja, amekifanyia kazi na kwa sasa vipo vinafaa kwa ajili ya matumizi ya hospitali.

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kumpa kazi hizi za utengenezaji wa vitanda chakavu ili kuepusha gharama ya kununua vipya pesa inayogharimu serikali," alisema.

Kwa upande wake Fadhili, alisema baada ya kuona vitanda chakavu aliamua kuomba nafasi ya kuvifanyia kazi kwa kutumia ujuzi wake ili kuona namna ya kuishawishi Wizara ya Afya kumpa kazi kwa gharama nafuu, lakini katika ubora wa hali ya juu.

"Niliamu kufanya hivyo baada ya kuona fursa ndani ya uchakavu wa shehena hizo za hospitali kwa kuwatumia vijana waliomaliza Veta kozi mbalimbali ili kuhakikisha wanapata ajira na kufundishwa namna ya kutumia fursa zinazotuzunguka," alisema.

"Ninaomba serikali kupitia Wizara ya Afya kunipa kazi hiyo ili kuona namna ya kuitumikia nchi yangu na kutoa ajira kwa vijana waliomaliza chuo cha ufundi Veta," alisema.

Aidha, baadhi ya vijana walioshirikiana katika kufanya kati hiyo walikiri kuweza kufanya kazi hiyo kwa utaalamu waliopata katika Chuo cha Ufundi Veta, na kusema kwa kufanya hivyo kutapunguza tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini," alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 21, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 19

## Yasiyomalizika kuhusu ubaya katika uhusiano, mantiki yake kisaikolojia

Ukurasa 15



## Wana Suba wapania kuwakwamua wanafunzi 846 waliobaki nyumbani

Ukurasa 18.



### JE, WAJUA?

Mambo matano yanayodhihirisha dunia 'si ya wanawake'



# Chuo cha Ualimu Vikindu katika mahafali ya 18 ya kutoa walimu

Ukurasa 16



IGP Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Mnyonge, mnyongeni haki yake mpeni

NAANZA kuandika makala hii kwa kutumia msemo "Mnyonge, Mnyongeni, haki yake Mpeni" kwa maana ya kwamba si mambo yote yanayofanywa na Jeshi la Polisi ni mabaya, la hasha.

Kuna mengi mazuri na yenye thamani kubwa kwa maisha yetu na mali zetu yanayotekelezwa na Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Hivyo jamii inapaswa kuwa na moyo wa shukrani kwa polisi wanaotulinda sisi na mali zetu wakati tumelala na sio kuwakejeli na kuwadharau.

Kwa nyakati tofauti baadhi ya watu wasiokuwa na shukrani hupenda kuwakejeli askari polisi na Jeshi la Polisi wakati linapotekeleza jukumu lake la msingi la kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa lengo la kuwawezesha Watanzania waendelee kuwa na amani na utulivu.

Hali ya usalama nchini hupimwa kwa takwimu za makosa mbalimbali ya jinai yanayoripotiwa katika vituo vya polisi na sio jambo la hisia au kudhaniwa

kwa mujibu wa takwimu za makosa ya jinai zinaonyesha kuwa makosa makubwa na madogo ya jinai kwa pamoja yamepungua kwa asilimia 6.9 kutoka makosa 50,424 kwa mwezi Januari 2019 hadi makosa 46,940 kwa mwezi Februari 2019.

Kwa upande wa matukio ya usalama barabarani, takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya matukio makubwa ya usalama barabarani 254 yaliripotiwa mwezi Februari 2019, ikilinganishwa na matukio makubwa 279 yaliyoripotiwa mwezi Januari 2019, ambao ni upungufu wa makosa 25 sawa na asilimia 9.

Licha ya kukashifiwa na kupata kejeli nyingi kutoka kwa baadhi ya watu wenye lengo la kuharibu taswira nzuri ya Jeshi la Polisi, askari polisi bado wanaendelea kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaimarika.

Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, wakati akiwasilisha bungeni, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20, amesema kuwa hali ya uhalifu nchini imepungua kwa kiasi kikubwa.

Kwamba katika kutimiza jukumu hilo Jeshi la Polisi limeendelea kuimarisha misako, doria na operesheni kwa kutumia mbinu mbadala za kudhibiti uhalifu sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Pia, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya makosa makubwa ya jinai 45,574 yaliripotiwa katika vituo vya polisi nchini ukilinganishwa na makosa 47,236 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18.

Upelelezi wa makosa hayo ulifanyika ambapo kesi 17,631 zikiwa na watuhumiwa 37,267 zilifikishwa mahakamani.

Aidha, katika kudhibiti uhalifu wa matumizi ya silaha, Jeshi la Polisi lilifanya operesheni ambapo jumla ya silaha 351 na risasi 4,844 za aina mbalimbali zilikamatwa na jumla ya watuhumiwa 239 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Wote tujiulize, je, kama isingekuwa juhudi za Jeshi la Polisi katika kudhibiti uhalifu huo wa kutumia silaha hali ingekuaje huku mitaani kwetu? Au tunadhani uhalifu unapungua tu bila kazi yoyote kufanyika? Hapa ndipo msemo huu unapotumika mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

Jeshi la Polisi linapaswa kupongezwa na kuunga mkono polisi kwa kuwatia moyo ili waendelee kudumisha amani na usalama nchini.

***Imetolewa na;***
***Kitengo cha Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***
***S.L.P 9141***
***Dar es Salaam***
***Baruapepe habariphq@yahoo.com, habari.phq@tpf.go.tz***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Asiyeangalia huishia ningalijua

MTU asiyeangalia aendako huishia kusema 'laiti ningejua' baada ya kufikwa na jambo.

Methali hii yatushauri tuwe watu wa kukanyika au wanaofuata ushauri tunaopewa na wanaotutangulia kwa maarifa au ujuzi kama vile wazee.

'Kanya' maana yake ni kataza mtu kutofanya jambo linaloweza kumletea hasara au madhara; kanyana, kanyia, kanyika, kanywa.

'Ushauri' ni maoni anayopewa mtu ili yamsaidie kufikia mapatano fulani na wengine. Maelekezo kama vile ya kiufundi anayotoa mtaalamu kuhusu namna ya kufanikisha jambo.

Wahenga walisema "Asiyeonywa huona (kwa) macho yake." Mtu anayekanywa kisha akayapuuza maonyo yale huishia kufikwa na madhara.

Methali hii hutumiwa kumtajia au kumwelezea mtu anayepewa ushauri na kuupuuza, kuwa atakuja kupatwa na madhara.

Kuna wanaonibeza (kitendo cha kupuuza kitu, mtu au jambo; kitendo cha kuonyesha hisia ya kejeli kwa mtu). Baadhi ya wanaonifahamu huniambia: "Ah! tangu lini Mmasai/Mchaga akajua Kiswahili?"

Wengine hunambia: "Rudi kwenu masaini na uchagani ukawafunze nduguzo Kiswahili fasaha. Kwenu mbuzi mwaita 'mbusi', nazi mwaita 'nasi', viatu mwasema 'fiatu.' Utatufundisha nini wewe? Sisi ndiwo wa kukufunza wewe."

Hata hivyo, wapo wanaounga mkono safu yangu ya "Tujifunze Kiswahili" kila Jumanne katika gazeti hili unalosoma sasa - Nipashe. Ukisema hutaki, kuna wanaotaka.

"Habari za leo. Shukrani kwa juhudi yako ya kutuelimisha matumizi mazuri ya lugha yetu, Kiswahili. Waandishi wa habari za michezo wana kawaida ya kutokamilisha sentensi. Hebu angalia mfano huu:

" ... ni timu kubwa na tunaiheshimu, lakini tumejiandaa kupata matokeo," alisema kocha wa timu. Hapa nashindwa kuelewa ni matokeo ya aina gani. Je, neno 'matokeo' lina maana sawa na ushindi? Naitwa Kissiwa, niko Zanzibar (+255 0713 768 335).

Siku iliyofuata akanitumia ujumbe mwingine: "Asalaam aleykum. Matumizi mabaya ya neno 'lakini.' Waandishi/wazungumzaji huandiika/husema, 'lakini pia ...' na kuendelea na maelezo yao.

"'Lakini' huonesha hitilafu wakati 'pia' ni ziada. Iweje maneno haya yaunganishwe? Kwa nini lisitumike moja tu kati ya hayo?" Kissiwa.

Neno 'lakini' hutumiwa sana na viongozi wetu na ingawa nimelitolea maana yake mara nyingi, bado laendelea kutumiwa tofauti kabisa na maana yake. Kama alivyoandika Bw. Kissiwa, maana ya 'lakini' ni tamko la kuonesha kasoro ya jambo; neno linaloonesha upungufu, kasoro au hitilafu; isipokuwa, ila.

Mfano: "Alitaka kwenda kwa mwfulani (jina linalotumika kumtaja mtu ambaye yupo ila jina lake linafichwa) lakini alikatazwa na wazazi wake kutokana na tabia chafu ya huyo mwafulani.

Neno 'Pia' lina maana tano: i) Kitu chenye umbo la koni cha kuchezea watoto kwa kukizungusha wakati kimesimama ncha; ii) Mfupa unaochezacheza ulio juu ya goti; iii) Omo ya chombo cha majini yenye umbo la duara; iv) vilevile; na v) Bila ya kubaki, pamoja na.

Msomaji mwingine alinitumia ujumbe ufuatao: "Mzee Maro (yeye aliandika Malo) umefundisha vitu vya msingi sana. Hata mimi nimefurahi sana. Nakutakia kazi njema. Ni mimi Mustafa nikiwa Mtwara." 0684 307081.

Nawashukuru wote walionitumia maoni yao. Mimi si mwalimu kama waniitavyo wengine ila ni mwanafunzi wa Kiswahili. Kidogo nipatacho huwashirikisha na kuwagawia wenzangu. Karibuni hata kwa kunikosoa kwani akuambiaye usikombe mboga ataka ushibe.

Sasa soma jinsi Kiswahili kinavyopelekwa arijojo (hali ya kupotea; kupoteza mwelekeo).

"Mnyalu buana, yaani juzi wenzako walikuwa wanakuangalia halafu wakacheeka ila mimi sikucheka, niliwaza ikitokea itakuwaje?"

"Ndugai buana, yaani unamtaja mke wa mwenzako kuwa ni mzuri, hee si unajua Wagogo wa Dodoma kuamua huwa wanaamua kwa haraka mara moja. Sawa lakini mmh!"

"Spika buana, eti wabunge wanapiga kelele kama vilabuni!"

"Lakini kikubwa alichowaacha hoi wabunge na kutaka wampigie makofi mkongwe huyo wa siasa za Tanzania, ni pale aliposema ndiyo mwalimu wake kwa kila kitu. Nyoka wa makengeza buana!"

Neno buana halimo kwenye msamiati (maneno yote yanayotumika katika lugha) wa lugha ya Kiswahili ila yanaingizwa na waandishi wetu baada ya kusikia maneno ya vijiweni na mitaani! Eti buana ndio bwana! Twaipeleka'pi lugha yetu?

Sasa hata wazungumzaji kutamka au waandishi kuandika maneno ya Kiswahili kwa ufasaha wanashindwa! Ndo maana wahenga walisema "Kuchamba (ashaakum) kwingi mwisho huondoa mavi."

Methali hii hutumiwa kupigia mfano jambo ambalo limeonesha dalili fulani ambazo zimepuuzwa kisha likaishia kuharibika. Tusiyadharau mambo madogo; huweza yakawa makubwa baadaye.

Mambo madogo kuwa makubwa ni kama haya: "Yale maji ya mjengoni yanayorukaruka yamekauka ama vepee?" Eti waandishi wameona neno vipi halifai ila linalofaa ni vepee! Haya ndio matokeo ya kuchamba kwingi ...!

"Mwenyewe anajiitaga mawe matatu. Ndo lugha ya wenzetu wa Kanda ya Ziwa kusema nakulaga, nakwendaga, nasemaga n.k. badala ya hula, huenda, husema, n.k.

Hata wasomi sasa wameathirika kwa matumizi mabaya ya maneno kama ilivyo hapa:

"Kwa kifupi tunasema pole Msigwa, yaani ulivyoachwa kwenye mataa hata swali la nyongeza ukanyimwa maana ulitaka kuja kivingine."

'Taa' ni neno lenye maana mbili:
i) chombo kinachowashwa na kutoa mwangaza kwa ajili ya kuonea. Kuna taa za aina nyingi: kibatari/koroboi, fanusi, karabai (taa yenye chemli/chemni inayotumia mafuta na upepo na hutoa mwangaza mkali) na taa ya gesi inayotumiwa migodini).

Neno hili halina wingi wa kuitwa 'mataa!' Moja ni taa na nyingi ni taa. Husemwa taa hii (moja) au taa hizi (zaidi ya moja) na si 'mataa.'

ii) Pia 'taa' ni samaki mkubwa mwenye umbo bapa na mkia mrefu wenye miba na hupenda kulala mchangani. Hapa pia samaki taa mmoja husemwa 'taa huyu' na wengi husemwa 'taa hawa'.

Methali: Kila mlango na ufunguo wake.

***marobarnabas@yahoo.com, 0715/0784 334 096***

UCHAMBUZI

**NA SABATO KASIKA**

# Wana Suba wapania kuwakwamua wanafunzi 846 waliobaki nyumbani

- Ni wanaotakiwa kuingia kidato cha kwanza Halmashauri ya Rorya-Mara
- Wachangishana Sh. milioni 360 kujenga madarasa 18

WADAU wa elimu Tarafa ya Suba wilayani Rorya, wameanza mkakati wa kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 18 yatakayoweza kukwamua wanafunzi 846, waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini bado wako nyumbani kutokana na uhaba wa madarasa.

Aprili 7 mwaka huu, wadau hao ambao ni Umoja wa Maendeleo ya Wananchi wa Tarafa ya Suba walifanya mkutano wa harambee jijini Dar es Salaam ili kukusanya Sh. milioni 360 za kujenga madarasa hayo katika shule sita za sekondari zilizomo kwenye tarafa hiyo.

Shule hizo ni Kisumwa, Kyang'ombe, Suba, Nyihura, Nyamunga na Waningo, ambapo inaelezwa kuwa fedha zinazokusanywa na wadau hao ni sawa na wastani wa Sh. milioni 20 kwa kila darasa, kati ya madarasa 18 yanayohitajika katika hizo shule sita.

Mbali na wanachama wa umoja huo na watu wengine, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rorya, Charles Chacha na mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Albert Machiwa walihudhuria katika harambee hiyo, ambapo michango pamoja na ahadi zilifikia Sh. milioni 70.

Mwenyekiti wa umoja huo Lucas Msimbete alisema nje ya mchango huo uliopatikana siku hiyo, kamati ya harambee ilikuwa tayari imeshakusanya Sh. milioni 15, huku halmashauri nayo ikiwa imeshachangia Sh. milioni tano.

**MWENYEKITI**

Msimbete ambaye ni mwenyekiti wa umoja huo anasema wamepania kuinua elimu katika tarafa hiyo, kwa vile wanatambua kwamba shule hizo ni mali ya wananchi, hivyo hawana budi kuzisaidia kwa hali na mali na pia kuzitunza.

"Hivyo kama wenyeji wa tarafa ya Suba tunaoishi Dar es Salaam, tumeona kuna haja ya kuchangia maendeleo ya nyumbani kwetu... pesa tunazotafuta zitatumika pia kununua vifaa mbalimbali vya kuboresha miundombinu ya shule hizo ili kuwezesha watoto hao kupata elimu," anasema.

Anasema wamepanga kuhakikisha wanafunzi wote 846 waliofaulu, ambao bado wanasubiri madarasa, wanaanza shule ili kuwaepusha na changamoto wanazoweza kukutana nazo iwapo wataendelea kuwa nyumbani.

Msimbete anasema bila kuchukua hatua hizo, wanafunzi wa kike wanaweza kutumbukia katika ndoa za utotoni, huku wa kiume wakijihusisha na uvuvi, kwa vile



Wanafunzi wakiwa katika mtihani wa taifa wa kumaliza elimu ya msingi. Baadhi ya wanafunzi waliofaulu mtihani huo mwaka jana hawajaanza kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa katika maeneo mbalimbali nchini kama ilivyo kwa Tarafa ya Suba, wilayani Rorya Mkoa wa Mara. **PICHA: MTANDAO**

> "Wakati utaratibu wa elimu unaanza mwaka 2016, hawa waliofaulu mwaka jana walikuwa darasa la tano na ndio waliohitimu elimu ya msingi mwaka uliopita, ambapo idadi hiyo ya wanafunzi 1,246 wamefaulu kwenda sekondari katika tarafa ya Suba

tarafa hiyo iko kando ya Ziwa Victoria.

**KATIBU WA KAMATI**

Kwa upande wake katibu wa kamati ya harambee hiyo, Pilly Marwa, anawaasa wadau wa elimu wajitokeze pia kuwaunga mkono.

Anasema wamefungua akaunti kwenye Benki ya CRDB kwa ajili ya shughuli hiyo ambayo CRDB 0150431073801.

"Wadau waendelee kutusaidia michango yao kupitia akaunti hii, inayoitwa Maendeleo-Suba Education Fund na wakishaingiza watoe taarifa kwa viongozi wa kamati," anasema.

**MKURUGENZI HALMASHAURI**

Kwa upande wake Chacha ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo anasema jumla ya wanafunzi 1,246 walifaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, katika shule za msingi za tarafa ya Suba.

Anasema sera ya elimu bure imesaidia kwa kiasi kubwa wanafunzi kuhitimu elimu ya msingi, tofauti na miaka ya nyuma ambapo baadhi waliishia njiani kutokana na ukosefu wa ada na michango mbalimbali shuleni.

"Wakati utaratibu wa elimu unaanza mwaka 2016, hawa waliofaulu mwaka jana walikuwa darasa la tano na ndio waliohitimu elimu ya msingi mwaka uliopita, ambapo idadi hiyo ya wanafunzi 1,246 wamefaulu kwenda sekondari katika tarafa ya Suba," anasema.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanasuba, Lucas Msimbete, akizungumza katika harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa yatakayowezesha wanafunzi zaidi ya 800 walioko nyumbani mwaka huu kuanza kidato cha kwanza.

**CHANGAMOTO**

Chacha anasema kila penye mafanikio kuna changamoto zake, na kwamba utoaji wa elimu bure umeongeza mahitaji ya madarasa kwa vile sasa wanafunzi wanaohudhuria masomo ni wengi, hivyo wazazi na walezi hawana budi kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya shule.

Anabainisha kwamba ufaulu wa wanafunzi hao ni baraka, hivyo ni muhimu wakazi wa tarafa ya Suba na Rorya kwa ujumla, kuungana na kuwa wasiruhusu umaskini uwapoteze watoto hao waliokwama nyumbani.

"Ninawashukuru Umoja wa Maendeleo ya Wananchi wa Tarafa ya Suba umeonyesha mfano mzuri, ila ombi langu kwamba hicho kiasi cha pesa kinachotafutwa kikitimia, watununulie vifaa tu ili tufanye kazi," anasema.

Aidha, anaushari umoja huo kuongeza nguvu kwa ajili ya kujenga mabweni ili kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wa kike kusoma na kufaulu vizuri katika masomo ya sekondari bila vikwazo.

Mkurugenzi huyo anasema elimu ni urithi na pia ni silaha dhidi ya umaskini, hivyo kuna umuhimu wa kuwekeza zaidi katika elimu, kwa vile bila hiyo ni vigumu kujiletea maendeleo.

"Halmashauri yetu imekuwa ikifanya vizuri kwa kushika nafasi ya kwanza katika matokeo ya kidato cha nne kati ya halmashauri tisa za mkoa wa Mara, hivyo tuendelee kushikilia namba hiyo," anasema.

Chacha anabainisha kuwa njia ya kuendelea kufanya vizuri kwa kushika nafasi hiyo ya kwanza ni kushirikiana kuboresha miundombinu ya elimu kadri inavyowezekana ili hatimaye waweze kuwa kinara wa mkoa.

"Suba mmeonyesha njia na mmetuita kuja kushiriki katika harambee hii ambayo ninaamini itasaidia kufanikisha ujenzi wa madarasa yanayohitajika, hivyo nirudie kutoa wito kwa wengine kuiga mfano huu," anasema.

Anasema Wilaya ya Rorya ilianzishwa mwaka 2007 kutoka katika Wilaya ya Tarime na kwamba ina tarafa nne ambazo ni Luo-himbo, Nyancha, Girango na hiyo ya Suba ambayo wakazi wake wanachangishana fedha kunusuru wanafunzi 846 waliofaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka huu.

ELIMU

NA YASMINE PROTACE, MKURANGA

# Chuo cha Ualimu Vikindu katika mahafali ya 18 ya kutoa walimu

## • Kina majengo ya mwaka 1936 • Mkuu wake apanda bodaboda na daladala katika shughuli za kikazi • Wanachuo watumia 'google' kwa kukosa maktaba

LENGO Namba 4 la Maendeleo Endelevu 2030 ya Umoja wa Mataifa (SDGs), linataka elimu bora iliyo jumuishi itolewe kwa watoto wote duniani bila kujali hali zao.

Lengo hilo linataka elimu hiyo iwe ni ile inayokuza fursa za kujifunza kwa watoto wa matabaka yote, katika kipindi cha maisha yao.

Pengine swali la kujiuliza ni kwa nini kuwe na lengo hilo?

Ukisoma maelezo yaliyoambatanishwa katika lengo hilo, utapata jibu kwamba ni kwa sababu elimu bora ni msingi wa maendeleo endelevu na hivyo kufikiwa kwa SDGs.

Kwamba elimu ni nguvu mtambuka inayowezesha kufikiwa kwa lengo la kujitegemea, kuboresha ukuaji wa uchumi, ustawi kwa kufungua fursa za watu kuwa na maisha bora.

Kimsingi, elimu ni moja ya SDGs 17 za Umoja wa Mataifa.

Sasa ili kulifikia lengo hilo, kuna hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na mataifa, pamoja na wadau mbalimbali na mojawapo ya hatua hizo ni kuongeza maradufu mgawanyo wa walimu waliofuzu vizuri.

Kwamba hilo litafanikiwa kwa ushirikiano wa mataifa yote yakiwekeza pamoja na mengine kutoa mafunzo bora kwa walimu, hasa kutoka nchi maskini na zinazoendelea.

### KWA NINI MAFUNZO YA WALIMU NI MUHIMU?

Mwalimu ni muhimu kwa sababu ndiye anayewezeshwa kitaaluma kuamua njia ipi aitumie kujenga mazingira bora kwa mwanafunzi kujifunza.

Yumkini kuna njia nyingi za kuboresha ubora wa elimu, mojawapo ni kunyanyua viwango vya ubora wa walimu.

Kwamba walimu ndio walio mstari wa mbele katika harakati za kutoa elimu bora inayohitajika kwa watoto ili pamoja na mambo mengine, dunia na taifa kwa maana hiyo liwe na wataalamu wa kutosha.

Wataalamu wa kuliendeleza taifa katika nyanja zote za kimaisha, yaani kijamii, kiuchumi, kisiasa, sayansi na teknolojia yake.

Kwamba haitoshi tu kuwaingiza watoto darasani kila siku, bali kuhakikisha kwamba wanajifunza pia.

Tanzania nayo kama mojawapo ya mataifa yaliyosaini utekelezaji wa SDGs imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba lengo Namba 4 la SDGs, linafikiwa katika suala la kuhakikisha kwamba changamoto ya upungufu wa walimu inashughulikiwa.



Wahitimu wa mafunzo ya ualimu Vikindu katika mahafali yaliyofanyika chuoni hapo.
PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE



Kaimu Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Silvia Chinguwile, akizungumzia jambo katika mahafali ya 18 katika Chuo cha Ualimu Vikindu.

> "Tulikuwa na mabweni manne ya zamani, wizara imewezesha ujenzi wa mabweni mapya matatu yanayochukua wanafunzi 80, hivyo bado tuna upungufu wa mabweni matano, lakini pia imewezesha ujenzi wa ghorofa lenye madarasa manane, tuna upungufu sasa wa madarasa matatu



Moja ya mabweni ya Chuo cha Ualimu Vikindu ambayo hayajafanyiwa ukarabati kwa miaka 83 sasa.

Mbali na kujenga vyuo vya ualimu maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kutoa walimu wa ngazi mbalimbali wa kufundisha shule za misingi na sekondari, inaendelea kuimarisha miundombinu ya baadhi ya vyuo.

Ni katika dhima hiyo hiyo ya kutoa walimu wenye taaluma stahiki kufanikisha pamoja na mengine lengo namba 4 la SDGs.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mwaka jana na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, idadi ya walimu wanaofundisha elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu katika sekta ya umma na binafsi iliongezeka nchini.

Iliongezeka kutoka walimu 257,469 mwaka 2012, hadi walimu 332,740 mwaka 2016.

Kwamba kati ya hao, walimu 293,909 wanafundisha shule na vyuo vya serikali, 38,831 wanafundisha shule na vyuo vya ualimu visivyo vya serikali.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo bungeni mwaka jana wakati akiwasilisha muswada wa sheria ya bodi ya kitaalamu ya walimu Tanzania.

### CHUO CHA UALIMU VIKINDU MKURANGA

Moja ya vyuo vinavyozalisha walimu na hivyo kuchangia wataalamu hao muhimu katika sekta ya elimu, ni Chuo cha Ualimu Vikindu Mkuranga.

Chuo hicho ni miongoni mwa vyuo 35 vya serikali vinavyotoa mafunzo ya ualimu katika ngazi mbalimbali.

Pamoja na kazi kubwa kinayoifanya ya kutoa walimu wanaohitajika katika suala la kuboresha elimu nchini, kinakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Hizo ni pamoja na ukosefu wa maktaba, uchakavu wa mabweni, uchakavu wa nyumba za walimu na ukosefu wa kituo cha afya.

Changamoto hizi zinabainishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Nicholaus Kampa kwenye mahafali ya 18 ya wahitimu wa stashahada ya elimu ya msingi na sekondari katika chuo hicho yaliyofanyika hivi karibuni.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo alikuwa Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Sylivia Chinguwile.

Kampa anabainisha kwamba kutokuwapo kwa maktaba katika chuo hicho kunasababisha wanafunzi kutumia simu zao za mkononi kuingia kwenye 'google' ili kutafuta mada na marejeo mbalimbali kwa ajili ya kujifunza na hivyo msaada kwa masomo yao.

"Tunaomba tujengewe maktaba katika chuo hiki kwani walipokuja wakaguzi wa shule, walituomba sana tuwe na maktaba... kwa kweli maktaba ni muhimu kwa wanafunzi," anasema.

Aidha, mwenyekiti huyo wa bodi anasema changamoto ya uchakavu na uhaba wa mabweni inasababisha wanafunzi kulala chini, wengine mzungu wa nne.

"Kwa upande mwingine kutokuwapo kwa zahanati hapa chuoni kunasababisha wanafunzi na walimu wanapougua kwenda vituo vya afya nje ya chuo kupata matibabu," anasema.

### BWALO LA CHAKULA

Kampa anazungumzia pia udogo wa bwalo la chakula akisema haliendani na idadi ya wanachuo waliopo kwa sasa.

Anabainisha kwamba chuo kina zaidi ya wanafunzi 500 ambao baadhi yao wanalazimika kula chini ya miti, kutokana na udogo wa bwalo la chakula lililopo sasa.

### USAFIRI

Mwenyekiti huyo wa bodi anataja changamoto nyingine inayokabili chuo hicho ya kutokuwa na gari la chuo.

Anasema hali hiyo inasababisha mkuu wa chuo kutumia usafiri wa bodaboda au daladala kwenda chuoni hapo au kwenye mizunguko yake ya kikazi.

"Lakini ukosefu wa gari la chuo unasababisha hata wanafunzi wanapougua, inakuwa changamoto sana kuwafikisha katika vituo vya afya kupata matibabu, ukiacha kukwama kwa kazi nyingi za chuo," anasema.

Pamoja na hayo Kampa anaishukuru Wizara ya Elimu kwa kuwezesha ujenzi wa jengo la utawala, bwalo, madarasa, kukamilisha bweni, lakini kwa kuwapatia kompyuta 30.

"Tulikuwa na mabweni manne ya zamani, wizara imewezesha ujenzi wa mabweni mapya matatu yanayochukua wanafunzi 80, hivyo bado tuna upungufu wa mabweni matano, lakini pia imewezesha ujenzi wa ghorofa lenye madarasa manane, tuna upungufu sasa wa madarasa matatu," anasema na kuongeza:

"Tunashukuru pia kwa kutupatia wafanyakazi wa kutosha, kwani chuo kina walimu 76 hadi sasa," anasema.

### MKUU WA CHUO

Kwa upande wake mkuu wa chuo hicho, Amina Tou anabainisha katika risala yake kwamba chuo kilirithi majengo chakavu yaliyojengwa mwaka 1936, wakati walipohamia hapo Vikindu mwaka 2001.

Anasema majengo hayo yalikuwa yakitumika kwa ajili ya shule ya msingi ya kati (Middle School).

"Toka mwaka 1936, hadi sasa ni miaka 83 na majengo haya hayajawahi kufanyiwa ukarabati," anasema.

Mwalimu Amina anasema chuo hicho kilianza rasmi kutoa mafunzo ya ualimu mwaka 1988 huko Bagamoyo katika Chuo cha Uongozi wa Elimu (MANTEP), sasa ni ADEM.

Anasema chuo hicho ambacho ni miongoni mwa vyuo 35 vya serikali vinavyotoa mafunzo ya ualimu kwa ngazi mbalimbali, kilikuwa kikiendesha mafunzo ya kilimo kwa walimu (in service ) kwa shule za msingi Tanzania Bara na Visiwani.

"Kilianza kutoa mafunzo ya ualimu daraja la 111 A mwaka 2001, hatimaye stashahada ya ualimu elimu ya awali na stashahada ya elimu ya msingi kuanzia mwaka 2014," anasema na kuongeza:

"Kwa sasa chuo kinatoa mafunzo ya stashahada ya elimu ya sekondari kwa miaka miwili na ualimu daraja la 111 A kwa muda wa miaka miwili pia."

### TAALUMA

Akiwazungumzia wahitimu, mkuu huyo wa chuo anasema wakiwa chuoni wamejifunza mambo mbalimbali kulingana na matakwa ya kozi zao.

Anasema kwa kozi ya daraja 111A, wamejifunza Ualimu, Kiswahili, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Tehama, Stadi za Kazi, Haiba na Michezo, Sayansi pamoja na Uraia.

Aidha, anabainisha wamejifunza vilevile wamejifunza Stadi za Mawasiliano.

"Kwa upande wa stashahada ya ualimu wa sekondari, masomo waliojifunza ni Kiswahili, Historia, Jiografia, Kiingereza, Ualimu, Stadi za Mawasiliano, Vielelezo na Teknolojia (ICT na Communication Skills).



Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo, Nicholaus Kampa, akizungumza katika mahafali ya 18 ya wahitimu wa chuo cha Ualimu Vikindu.

Anasema kazi ya kufundisha na kujifunza inahitaji umahiri mkubwa ili kuweza kubaini vipaji vya watoto, kuviendeleza na hatimaye kuinua kiwango cha uelewa kwa wanafunzi.

"Ili kufikia kiwango hicho, wahitimu wameiva katika njia na mbinu mbalimbali zilizo bora walizojifunza na kujifunzia katika matumizi ya mbinu hizo...mwanafunzi ndio kitovu cha maarifa," anasema.

### MBINU

Katika mafunzo hao wameweza kupata umahiri katika kubuni kufaragua na kutengeneza zana mbalimbali za kufundishia na kujifunzia, zitakazowasaidia kuwaandaa vijana vizuri walioko shule za sekondari na msingi.

INAENDELEA UK.18

JIELIMISHE

## Ugonjwa wa surua waathiri watu zaidi barani Ulaya



SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema kuwa zaidi ya watu 34,000 barani Ulaya wamepata ugonjwa wa surua katika miezi miwili ya kwanza ya mwaka 2019.

Wiki iliyopita, WHO lilisema kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya visa vya ugonjwa wa surua barani Ulaya, katika miezi ya Januari na Februari mwaka huu.

Visa vilivyorekodiwa katika nchi 42 vimesababisha vifo 13. Idadi ya visa hivyo ilikuwa mara tatu zaidi ya visa vilivyoripotiwa katika miezi miwili ya kwanza ya mwaka 2018.

Nchini Ujerumani, maofisa wa serikali katika Jimbo la Kaskazini la Lower Saxony, walisema kuwa mtu mmoja alifariki kutokana na ugonjwa huo, ijapokuwa hawakutoa umri wala jinsia ya mwathirika huyo.

WHO, linawahimiza maofisa wa serikali kuhakikisha kuwa watu wanaokabiliwa na hatari ya ugonjwa huo wanapata chanjo, huku ugonjwa huo kwa sasa ukienea katika maeneo mengi ya dunia.

Katika taarifa yake, shirika hilo lilisema kuwa iwapo hatua za haraka za kukabiliana na ugonjwa huo hazitachukuliwa, virusi hivyo vitawaathiri watu wengi na kuenea katika mataifa mengi zaidi kwenye eneo hilo na pia nje.

"Kila fursa inapaswa kutumiwa kuwapa chanjo watoto wanaokabiliwa na athari ya kukumbwa na ugonjwa huu, vijana na watu wazima," lilisema.

Ukraine inayokumbwa na janga la ugonjwa huo wa surua ilikuwa eneo la Bara la Ulaya lililoathirika zaidi, huku zaidi ya watu 25,000 wakiathirika katika kipindi hicho. Romania na Albania pia zilirekodi idadi kubwa ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Ugonjwa wa surua pia unaenea katika maeneo mengine ya dunia. Visa vya maambukizi vinaongezeka nchini Marekani, Ufilipino na Thailand.

Watafiti wanadai kuwa ugonjwa huo unasambaa kwa vipimo vya kutia wasiwasi kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao hawajapata chanjo katika baadhi ya maeneo.

Maofisa wa serikali wamesema kupungua kwa viwango vya chanjo kunatokana na kutokuwa na habari kuhusu chanjo hiyo ya ugonjwa wa surua pamoja na dhana potovu kwamba inasababisha ugonjwa wa tawahudi.

Ugonjwa huu hatari wa Suruwa husababisha upofu, kuharibika kwa ubongo na hata kifo.

Waziri wa Afya nchini Ujerumani, Jens Spahn, amependekeza sheria kuruhusu wazazi wa watoto ambao hawajapata chanjo kutozwa faini ya hadi Euro 2500 ama Dola 2,800, huku baadhi ya visa 170 vikiripotiwa nchini Ujerumani katika miezi ya Januari na Februari.

DW

INATOKA UK.16

# Chuo cha Ualimu Vikindu katika mahafali y

**USHIRIKIANO**

Anasema chuo kimepata mafanikio makubwa kwa ushirikiano wa karibu sana na bodi ya chuo pamoja na wazazi wa wanachuo.

"Kila mzazi mwenye mtoto chuoni anachangia kiasi cha fedha kwa ajili ya maendeleo ya chuo ambapo michango hutumika kununua magodoro na vifaa vya kufanyia usafi wa mazingira," anasema na kuongeza:

"Lakini pia kuboresha mazingira ya chuo, kufanya ukarabati mdogo mdogo wa majengo, madawati, viti, milango na vitanda."

Amina anasema wanaipongeza wizara katika kuchangia maendeleo ya chuo kwa kulipa fedha za chakula kwa wanachuo na kutoa fedha za kukamilisha Jengo la Mwinyi.

"Lakini pia kulipa mishahara ya wafanyakazi, fedha kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, kuongeza kompyuta 30 na kutoa miongozo mbalimbali ya uendeshaji."

**CHANGAMOTO**

Amina naye anaungana na mwenyekiti wa bodi kuzungumzia uchakavu wa miundombinu mbalimbali chuoni hapo.

**RAIS WA CHUO**

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu, rais mstaafu wa wanachuo, Kuwa Mohamed anasema pamoja na mafanikio katika masomo yao, lakini walikabiliwa na changamoto mbalimbali.

"Takribani zote zimetajwa na mwe-

## JE, WAJUA?

# Mambo matano yanayodhihirisha dunia 'si ya wanawake'

WAKATI safari ya wanawake watupu kwenda anga za juu ilipokatizwa katika dakika za mwisho kutokana na kubadilishwa mavazi, mjadala mkali umezuka kuhusu namna wanawake wanavyojizatiti kuwapo katika dunia inayoonekana imebuniwa kwa ajili ya wanaume.

Caroline Criado Perez, mwandishi wa makala inayoangazia takwimu zinazodhihirisha upendeleo na dunia iliyobuniwa wanaume, anasema hakushangazwa kuhusu mjadala huo wa mavazi ya wanawake kwenda anga za juu.

"Ndicho kinachofanyika kila uchao linapokuja suala la tunachokibuni...tumezoea kuwafikiria wanaume kila mara tunapokuwa katika ubunifu, na wanawake hufikiriwa tu katika misingi ya aina tofauti ya watu," anasema.

Yafuatayo ni mambo matano yanayodhihirisha jinsi ambavyo dunia haikubuniwa wanawake.



Mavazi ya kijeshi kama yanavyoonekana kwa mwanajeshi huyu, bado yametengenezwa maalumu kwa ajili ya wanaume. . **PICHA: MTANDAO**

**MAVAZI YA ANGA ZA JUU**

Shirika la Anga za Juu (Nasa) lilikabiliwa na shutuma kali katika mtandao wa Twitter, lilipotangaza kwamba huenda safari ya wanawake watupu kwenda anga za juu ikasitishwa kutokana na ukubwa wa mavazi hayo.

Limefafanua kwamba mwanaanga za juu Anne McClain aligundua dakika za mwisho kuwa ukubwa wa mavazi aliyopewa awali ni bora kuliko aliyotarajiwa kusafiri nayo ambayo yalikuwa makubwa mno, na kwa hivyo safari hiyo ikasitishwa kwa sababu za kiusalama.

**ZANA ZA KIJESHI**

Mwaka 2016, Jeshi la Marekani lilianza kuwasajili wanawake kupigana vita katika vitengo vilivyokuwa vya wanaume pekee kwenye Jeshi la Nchi Kavu, Jeshi la Maji na la Anga, lakini zana nyingi zilikuwa zimeundwa kwa ajili ya wanaume.

Jeshi liliongeza saizi nane ndogo za ziada za wanawake mwaka huo, lakini mavazi kama viatu, kofia za jeshi bado hazijageuzwa ukubwa.

Baadhi ya wanawake wameiambia Buzzfeed News mwaka huu kwamba wakati wakiwa jeshini, walilazimika kukarabati na kuvaa mavazi ya kinga yaliyobuniwa wanaume dhidi ya mashambulio, katika kuhakikisha kwamba mavazi hayo yanawasaidia kuwakinga kama inavyotakiwa.

Wanawake walilazimika kutumia nguo zilizostahili katika jeshi. Katika vita vya pili duniani, inaarifiwa wanawake hawakutarajiwa kufanya kazi zisizo za ofisini.

Ndio sababu jeshi halikutayarisha sare za kazi nyingine kama fundi wa magari.

**SANAMU LA AJALI ZA MAGARI**

Kwa miaka mingi, Marekani haikufanya majaribio ya kutosha ya ajali ya gari kwa kutumia sanamu la mwanamke aliyefungwa mshipi, mpaka ilipofika mwaka 2012, sanamu hilo la majaribio lilitumika kwa mfano wa mwanamume.

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2011 wa Chuo Kikuu cha Virginia Center for Applied Biomechanics, madereva wanawake waliohusika katika ajali za magari walikuwa na uwezekano wa asilimia 47 kupata majeraha mabaya wakilinganishwa na wanaume.

Na si Marekani pekee, hali hiyo imedhihirika pia katika mataifa ya Umoja wa Ulaya (EU).

"Katika majaribio matano kisheria yanayofanyika EU, kuna moja tu linalofafanua kwamba ni lazima utumie sanamu la kike na pia nalo huwekwa kwenye kiti cha abiria," anasema Criado Perez.

Criado anasema sekta hiyo inafahamu wazi kuwa ni lazima ishughulikie suala la wanawake.

"Lakini hawajalifanya hilo kwa namna yoyote ya maana inayodhihirisha kwamba wanawake ni asilimia 50 ya idadi jumla ya watu waliopo."

**SIMU ZA KISASA**

Kuanzia programu tumishi mpaka ukubwa wa simu, kuna ubunifu tofauti katika simu za kisasa uliowafanya wanawake kusema kwamba wanaume ndio waliolengwa katika ubunifu wa simu hizo.

Mikono ya wanawake kwa wastani ni midogo kwa angalau inchi moja kuliko ile ya wanaume, jambo linalozusha tatizo kila kunapoundwa simu zenye uso mkubwa.

Kutuma ujumbe katika simu yenye uso wenye ukubwa wa inchi 4.7 au kubwa zaidi huenda ikawa tatizo au kufanya kuwa vigumu kwa wanawake wengi na (baadhi ya wanaume walio na mikono midogo).

**BBC**

## UTAFITI:

# Mitandao ya kijamii huathiri vijana rika la kubalehe

ATHARI za matumizi ya mitandao ya kijamii kwa manufaa ya kuishi maisha yanayowaridhisha vijana ni chache na hasa kwa 'walio katika kipindi cha kubalehe,'

Utafiti uliowahusisha vijana wa Uingereza walio katika umri wa kubalehe 12,000 unabainisha.

Familia, marafiki na maisha ya shule kwa pamoja huwa na athari bora katika kuboresha maisha, inasema timu ya watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Oxford.

Na watafiti hao wamezitaka kampuni kutangaza taarifa juu ya namna watu wanavyotumia mitandao ya habari ya kijamii kuelewa zaidi juu ya athari za teknolojia hizo katika maisha ya vijana walio katika umri wa kubalehe.

Utafiti huo uliochapishwa katika jarida la PNAS ulilenga kujibu swali la ikiwa vijana walio katika umri wa kubalehe wanaotumia mitandao ya kijamii zaidi ya wastani wanaishi maisha ya kuridhika kwa kiwango cha chini au ikiwa vijana wenye umri huo ambao hawajaridhika kimaisha hutumia zaidi mitandao ya habari ya kijamii.

Tafiti za awali zilihusu uhusiano kati ya matumizi ya vifaa vya teknolojia ya mawasiliano, teknolojia yenyewe na afya ya akili ya watoto.

YALIYOJITOKEZA

Profesa Andrew Przybylski na Amy Orben, kutoka taasisi ya Intaneti katika Chuo Kikuu cha Oxford, wanasema mara nyingi ushahidi unaotumiwa hautoshi na hivyo kutoa picha ambayo haijakamilika.

Utafiti wao ulibaini kuwa uhusiano kati ya kuridhika kimaisha na mitandao ya kijamii 'hayana thamani,' faida yake ikiwa ni chini ya asilimia moja katika kuboresha maisha ya vijana wenye umri wa kubalehe na kwamba athari za mitandao ya kijamii ya habari 'hutoa taarifa kwa njia tofauti.'

Profesa Przybylski, ambaye ndio mkurugenzi wa utafiti huo katika taasisi hiyo anasema:

"Asilimia 99.75 ya kiwango cha kuridhika maishani haihusiani na matumizi yoyote ya mitandao ya kijamii."

Utafiti huo uliofanyika kati ya mwaka 2009 na 2017, uliwahusisha vijana wenye umri kati ya miaka 10 na 15 wakiulizwa waeleze ni muda kiasi gani wanaoutumia katika mitandao ya habari ya kijamii katika siku ya kawaida ya shule na pia kiwango cha jinsi muda huo ulivyowasaidia kwenye nyanja mbalimbali za maisha yao.

Walibainisha kuwa muda ambao wasichana waliutumia katika mitandao ya kijamii uliwaathiri zaidi miongoni mwao, lakini athari ilikuwa ni ndogo kuliko ilivyokuwa kwa wanaume.



Mabinti 'wakichati' kwa kuwezeshwa na teknolojia ya habari na mawasiliano ambapo sasa mitandao ya kijamii inachukua muda katika maisha na hasa ya vijana. **PICHA: MTANDAO**

# ya 18 ya kutoa walimu

nyekiti wa bodi na mkuu wa chuo...ninaomba serikali isaidie kuzitatua zilizobaki kwa ufanisi wa taaluma inayotolewa chuoni hapa," anasema.

**MGENI RASMI**

Akijibu hotuba na risala zilizotolewa katika mahafali hayo, mgeni rasmi Chinguwile anaanza kwa kusema kuwa ualimu ni wito, hivyo walimu wanatakiwa kuwa wabunifu katika kazi nzima ya ufundishaji.

"Wahitimu wote mtumie maarifa na mbinu mlizopata chuoni, kuwafundisha wanafunzi huko muendapo ili waweze kuyafahamu kwa ufasaha masomo yao," anasema.

Anawaasa walimu kuwa wazalendo kwa kuwafundisha watoto na kuhakikisha wanaelewa... na si kuchukuwa fimbo na kuwatandika wanafunzi.

"Mwalimu anatakiwa afundishe mwanafunzi amuelewe... hakuna sehemu inayosema sera ya elimu ni kuchapa wanafunzi," anasema.

**CHANGAMOTO**

Akizungumzia changamoto za chuo zilizoelezwa katika mahafali hayo, naibu katibu mkuu huyo anasema serikali inazifahamu changamoto hizo.

"Na ndiyo maana baadhi imeshazitatua na mwaka huu wa fedha, bajeti imetengwa kwa ajili ya kutatua baadhi ya changamoto zilizosalia, pia kuongeza idadi ya kompyuta," anasema.

Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Paulina Ndigeza, anawapongeza wadau wote wa Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano katika kuhakikisha sekta ya elimu inapaa kwa kazi.

Anasema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri kati ya serikali, walimu, wazazi na walezi pamoja na wadau ambao wanashiriki shughuli mbalimbali za kielimu.

## SAIKOLOJIA

**NA MICHAEL ENEZA**

# Yasiyomalizika kuhusu ubaya katika uhusiano, mantiki yake kisaikolojia



Uhusiano kama huu unahitaji kujitoa kama saikolojia inavyofundisha ili uwe imara. . **PICHA: MTANDAO**

MOJA ya maeneo ya majadiliano ya kijamii katika redio hasa za FM ni ukweli au undani wa uhusiano kati ya wanawake na wanaume, nani anayeharibu uhusiano au tuseme nani wa kulaumiwa kuhusu kuporomoka kwa mahusiano, ndoa kuvunjika au kuyumba wakati wote.

Siyo rahisi kusema kuwa kuna majawabu yoyote yanayojitokeza katika mijadala hiyo, ambayo kwa njia nyingine inakuwa ni burudani ya mvutano kati ya wanawake na wanaume kutupiana mzigo wa kuharibu uhusiano huo, bila jitihada ya dhati ya kutafuta majawabu.

Ni kujifurahisha kwa kutoa hoja za kulaumiana na kujitahidi zisifikie kikomo, kwani ikifikia mahali watu wanaelewana, kunapooza.

Hiyo haina maana kuwa inawezekana kabisa watu wakaelewana kuhusu jambo hilo, kwani katika kila suala linalogusa hisia, na siyo la ufahamu wa kawaida, siyo rahisi kuunganisha mawazo kwani kuacha kusisitiza umuhimu wa hoja au kipengele hiki au kile katika hoja.

Itakuwa sawa na kuwa tayari kuumiza nafsi, ambayo inatilia maanani kwa nguvu kile kinachozungumzwa.

Kila nafsi na kwa maana hiyo kila mshiriki katika mjadala kama huo anatazamia kuwa anachosema ndicho kitaeleweka, kuwa yaliyobaki yanakosa uelewa wa kina, yaani wa hisia chanya, kuhusu suala hilo.

Mijadala ya aina hiyo ndiyo inaitwa kwa Kiingereza 'the dialogue of the deaf,' yaani majadiliano kati ya viziwi, kwani kila mmoja anaisikia sauti yake tu au labda na sauti za wenye hoja kama ya kwake, na kuamini alichosema, au labda na wachangiaji wa mlengo kama huo.

Hiyo hata hivyo haina maana kuwa mjadala kama huo kweli ni wa 'viziwi,' kwani kwa maumbile yake, binadamu anachomwa na maneno pamoja na hisia zinazoambatana na maneno au hisia hizo.

Sababu ni kuwa katika maisha hakuna uhakika wa lolote lile, mfano wa mnyama akiwa porini; hatari ipo kokote.

Kinachofanya hoja inaleta mabishano makali ni ujumuisho wake kihisia, kwani mwanaume akisema 'wanawake wako hivi,' anajumuisha wote (ambao hawezi kuwafahamu kwa kiasi hicho) lakini anaweza kuwa na uhakika kuwa mumewe au mshirika wake kimahusiano yuko hivyo.

> Kujua jinsi binadamu walivyo kupitia kwa mtu mmoja ni busara na siyo sayansi,,,

Ndiyo hapo linazuka suala la mantiki kuhusu uwezo wa kujumuisha umati (wanaume wote) kwa kile kilichoonekana kwa mwanaume mmoja, au kilichotokea mara kadhaa kwa huyo mwanamke.

Kujua jinsi binadamu walivyo kupitia kwa mtu mmoja ni busara na siyo sayansi, ila sayansi pia haiwezi kuikanusha busara hiyo kwa kuwa haina uwezo wa kufanya utafiti kujua wangapi wanahusika.

Tofauti kati ya majadiliano ya kawaida na kufuatilia hoja hizo kimantiki ni kuwa pale ambapo mhusika, akizungumzia anachokifahamu au kilichomkuta katika maisha anasema 'wanaume wako hivi' au 'wanawake wako hivi,' mjadala wa kimantiki utalenga kuainisha uwezekano kuwa katika hali ya aina moja au nyingine, uelekeo wa hulka kuelekea njia hiyo ni mkubwa.

Hapo ingekuwa rahisi zaidi washirika kueleza wanachofahamu kama ni kiasi gani kwa mfano ndoa inaweza kuwa hatarini kutokana na tukio la aina moja au nyingine.

Mjadala kama huo ungeanza kufafanua ni wapi ndoa inakuwa hatarini na wapi inakuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kusimama, n.k.

Ukifuatilia kukua kwa fani tofauti za kisayansi zinazogusa maisha ya binadamu au uhusiano wa kijamii kwa jumla, unakuta kuwa mazungumzo ya kawaida kuhusu uhusiano yanaendana na fikra za zamani au za awali za falsafa, ambako wachangiaji na wabunifu walikuwa wanatafuta majawabu ya jumla. Inaonekana kuwa kinachotokea ni michepuo ya fikra za aina tofauti, na kila moja huwa inajenga kasri yake na shule zake (ndiyo hizi 'academies' au 'madrasa' zilizoanzishwa na Wayunani kwa sehemu kubwa).

Mzazi akichukia mwelekeo wa kihisia na tafsiri ya maadili au uhusiano unaofuatwa katika 'academy' fulani, anamtoa mwanae huko anampeleka kwingine, 'asiharibiwe.'

Ina maana kuwa hakuna mkondo wa kihisia au tafsiri ya jumla ya maadili au mahusiano ambayo inawezekana katika mazingira hayo, na kwa njia hiyo kujenga himaya yenye umoja kihisia au kimaadili inakuwa kazi ngumu.

Tawala za wakati huo hasa zilikuwa katika mfumo wa 'mijikenda' ambao umekuwapo maeneo mengi duniani, ikiwepo miongoni mwa makabila - kuwa koo tofauti zilikuwa zinajitawala, zikiwasiliana na kuhusiana na koo zingine kwa masuala kadhaa, hasa ulinzi.

Hata hivyo, udhaifu ulikuwa mkubwa kwani wakivamiwa kutoka nje wasingeweza kujilinda kwa pamoja bila ugomvi mkubwa nani kiongozi, kodi iwe kiasi gani - ndiyo ugomvi Somalia, Libya....

Himaya zilizuka ili kuondoa uhuru huo na migogoro isiyoisha wakati watu wanataka njia za biashara zifunguliwe, sheria iwe moja na mifumo ya maadili iunganishwe.

Ndiyo mifumo ya awali ikaanza kuanguka kwa kukosa malisho, kwani mijikenda ilipoanguka na 'academies' zikakwama pia, kukosa mazingira chanya ya kupata sifa, kupelekwa wanafunzi na wazazi kuwa tayari kuwalipa, n.k.

Fikra ya utawala mpya uliochukua nafasi ya mijikenda kwa silaha inaanza kutawala, ikiwa ni pamoja na kubadili mifumo ya ibada iendane na mizimu (inaitwa miungu) ya kabila au ukoo ulioko madarakani, au kama ni jeshi la maharamia, miungu ya alikotoka kamanda wa jeshi hilo.

Ndiyo mwanzo wa kuondoka katika mijadala ya kawaida ya wanaume wako hivi na wanawake wako hivi na kuweka mifumo ya maadili na sheria, ikiwa imefuatana na watoa sheria ambao kimsingi ni wachache katika historia, kama Solon wa Uyunani, Musa na Sulemani kwa Waisraeli wa kale na wa baadaye kidogo, Buddha wa India na Confucius wa China, na huku kukiwepo michepuo mingine ya sheria ikitawala jumuiya tanzu za mifumo hiyo mikuu, kwa mfano ilivyo katika madhehebu ya dini.

Kutatuliwa kwa ubishi wa wema na ubaya ni kuwekwa sheria moja, hivyo tatizo likitokea inaangaliwa nani alivunja sheria, siyo nani alisababisha yeye avunje sheria!

Ina maana kuwa tatizo la sasa hivi, au tuseme mazingira yaliyopo katika uhusiano nchini, na yanavyoonekana katika redio za FM ni upana wa uhuru wa kimaisha na jinsi jitihada za kuunda na kusimamia familia zinazodumu zilivyo ngumu, katika ulimwengu wa mashindano kimaisha.

Mazingira haya hayatabiriki matokeo yake kijamii au kwa mtu binafsi ni nini, hivyo pale nyumba au unyumba unaundwa katika mazingira fulani halafu yanabadilika, mahusiano nayo yataathirika.

Ndiyo hapo ubishi unaingia nani kasababisha hiki, wakati suala la msingi ni fursa za kipato na hivyo kihaiba au kimapenzi kupanuka kwa mmojawapo kati yao, na mwingine kuwa duni kwake.

Kanuni moja ambayo labda haijazungumziwa ipasavyo katika majadiliano hayo ni ile ya ushindani wa kihisia ndani ya mahusiano, ambayo ni tofauti na kanuni za maadili za kuishi kwa kupendana na kusaidiana.

Maadili hayo yapo na yanafanya kazi lakini mkondo wa ushindani hauko mbali na ndiyo msingi wa kanuni ya 'kuishi nao kwa akili,' au kuvumiliana, lakini matokeo ya mikondo hiyo ya ushindani wa kihisia kupata 'kilicho bora zaidi' ina matokeo tofauti.

Katika kila uhusiano upo upana wa udhaifu wa kibinadamu unaohitaji moyo ili kuulinda, na kwa kanuni ya mpauko wa kila aina ya uhusiano na hata maisha yenyewe (kuzeeka ni mpauko wa mwili kujisitiri, kujilinda) kuna uwezekano watu kushindwana.

Sasa ni aina gani ya uhusiano itakwama na ipi itafaulu kupita hizo changamoto ni suala la kisanyansi kwa kiasi fulani, la kitatifi, wakati katika majadiliano ni hisia chanya za kile kinachofanywa na mojawapo katika makundi ya jinsia ndicho kinachosikika zaidi.

*Dk. Raymond Nusura Mgeni. Anapatikana kupitia anwani raymondpoet@yahoo.com*
*+255 676 559 211*

## SAUTI ZA WADAU



**SABATO KASIKA**

WASHIRIKI wa warsha ya kujadili mbinu za kumaliza ukatili kwa watoto shuleni iliyofanyika Temeke hivi karibuni, wanadai vibanda vya picha za video vinaharibu wanafunzi kimaadili. Wadau wanasemaje?



**STANLEY CHARO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MTOTO kushuhudia picha za ngono ni sawa na kumlisha chakula ambacho hajafikia umri wa kukila. Hili suala la kuwapo kwa vibanda vya kuonyesha video mitaani siyo geni na baadhi ya wamiliki wa vibanda hivyo wamelalamikiwa sana kwa kuonyesha picha ambazo zinakwenda kinyume na maadili na tena mchana kweupe. Kibaya zaidi ni kwamba wanawaonyesha watoto wadogo. Jambo hili halina afya katika maadili. Kwa maoni yangu ni kwamba vibanda vyote vifutiliwe mbali na utafutwe utaratibu mwingine wa kuvisajili na kuwekewa masharti ambayo wahusika wakiyakiuka wanachukuliwa hatua kali za kisheria. Kwanza hata filamu za mapigano na ujambazi nazo hazifai kwa watoto, lakini wamekuwa wakionyeshwa. Katika mazingira hayo mtoto anajifunza nini cha kumsaidia katika maisha yake ya baadaye? Ingekuwa ni filamu za kawaida zinazoelimisha na hata mechi ya mpira wa miguu, sina tatizo, lakini wahusika wanapopitiliza hadi kuwaonyesha watoto vitu ambavyo vina athari kwa maisha yao ya baadaye, ni muhimu hatua za kisheria zichukuliwe haraka. Watoto hawajui lolote wanaposhuhudia picha au video mbaya, wao wanaona ni jambo la kawaida na inadaiwa kuwa baadhi yao wanaweza kuomba wazazi fedha wakisema wanakwenda kununua daftari au kalamu, lakini kumbe lengo ni kupata pesa ya kulipa kiingilio cha kushuhudia video zisizofaa. Watoto wajengwe katika maadili mema.



**ROSEMARY MMASI (MWALIMU S/MSINGI KEKO MWANGA, DAR ES SALAAM)**

HILI halina ubishi, ni kweli baadhi ya wanafunzi wanaingia katika vibanda hivyo na kujifunza mambo ya ovyo na kwenda kufanyia majaribio na mwisho wa siku wanajikuta wakifanyiwa ukatili.

Siyo sahihi vibanda hivyo kuwaonyesha watoto video za ngono, ambazo hazilingani na umri wao na matokeo yake wanakwenda kujaribiana katika maeneo mbalimbali ikiwamo vyoo vya shule. Inauma na inakera kama mtoto anapewa nauli kwenda shule au anatembea kwenda shule, huku wazazi wakijua kwamba yupo shuleni na kumbe anaishia katika vibanda vya video ambazo hazilingani na umri wake.

Ushauri wangu ni kwamba wazazi wawe na tabia ya kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, wanaweza kubaini mambo mengi kuliko kuwaamini moja kwa moja na mwisho wake ni kujiingiza katika mazingira ya kufanyiwa ukatili. Wanafunzi wenye tabia hiyo hata maendeleo yao shuleni huwa siyo mazuri. Hivyo suala la uangalizi tusiachiwe sisi walimu tu bali tushirikiane. Hilo likifanyika kikamilifu, tutapata kizazi bora cha baadaye kuliko kuwaacha wafanye wanavyotaka na kujikuta wakiwa katika hatari ya kushuka kitaaluma.



**BRIDGETER PILLA (HAKIMU MFAWIDHI WA MAHAKAMA YA MWANZO TEMEKE, DAR)**

TATIZO la aina hii linaanzia katika malezi. Wazazi wanatakiwa kusimamia vyema malezi bora kwa watoto wao ili kusaidia kutokomeza vitendo hivyo vikiwamo na vingine ambavyo vinagusa ukatili, ambao baadhi ya watoto wamekuwa wakifanyiwa hata na ndugu wa karibu.

Mzazi anatakiwa kufuatilia mwenendo wa mtoto wake kila anapokwenda na pia kuwa naye karibu, kumfanya awe rafiki ili kujua mambo mbalimbali anayokabiliana nayo. Ili kufanikisha hilo, mzazi hatakiwi kuwa mkali kupita kiasi, anaweza kukosa mengi yakiwamo hayo ya kuingia katika vibanda vya kuonyesha video chafu.

Kimsingi kila mzazi azingitie kaulimbiu ya mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Mama Salma Kikwete isemayo, 'mtoto wa mwenzio ni wako.' Hilo likifanyika itakuwa ni rahisi wazazi kupeana taarifa wanapoona nyendo za watoto wao siyo sawa. Kwa sasa mzazi anaweza kumuona mtoto wa mwenzake anafanya jambo fulani baya na ananyamaza kimya. Lakini tukizingatia kauli mbiu ya Mama Salma Kikwete, tukiona watoto wanaingia katika vibanda hivyo tutapeana taarifa kwa ajili ya kukomesha tabia hiyo na pia tutakomesha vitendo vya ukatili dhidi yao.



**HASSAN MPAKO (MKAZI WA LIWALE MKOANI LINDI)**

TUSIPOCHUKUA hatua, basi tunaandaa kizazi cha ajabu. Umakini wa wazazi na walezi ni wa muhimu katika hili, kwasababu video zinazoonyeshwa katika vibanda hivyo ni hatari kwa maadili. Mara nyingi huwa kuna picha za ujambazi, utekaji nyara, ukatili, lakini inaendelea mpaka kwenye picha chafu za ngono, halafu watoto wadogo wanaangalia. Hata kama siyo picha hizo, siyo sawa mtoto wa shule kuacha vipindi darasani na kwenda katika vibanda hivyo. Matokeo yake ni kwamba badala ya kukazania masomo, akili yake yote ataelekeza huko. Sioni umuhimu wa kuwapo kwa vibanda hivyo mitaani, kwani vina mchango mkubwa wa kutuharibia watoto wetu. Bila mamlaka husika kuchukua hatua, tutakuwa tunajenga jamii ya ajabu sana. Huko baadaye tutakuwa na watoto wahuni, makatili, majambazi, ambao mambo ya ngono kwao ni jambo la kawaida. Inawezekana wapo baadhi ya wazazi wanaona ni jambo la kawaida kuwaruhusu watoto wao kwenda katika vibanda hivyo na kuangalia picha zinazochochea ngono, lakini wajue kuwa wanachangia watoto wao kuanza uhusiano wa kimapenzi mapema na kuwa kwenye hatari ya kupata magonjwa ya zinaa, ukiwamo Ukimwi.



**SULEIMAN MATHEW (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MATUMIZI hasi ya teknolojia ya mawasiliano ikiwamo kuwapo kwa vibanda hivyo mitaani ni moja ya changamoto inayokwamisha jitihada za kulinda maadili ndani ya jamii na pia mapambano dhidi ya Ukimwi ambazo zimekuwa zikifanywa na mashirika mbalimbali pamoja na serikali. Vibanda hivyo pia vinasababisha wanafunzi wanatoroka shule, wanaiba pesa nyumbani na ni maarufu sana kwa kuonyesha picha za ngono...naomba kila mahali serikali ya mtaa iwe makini na vibanda hivi na ikibidi hata vipigwe marufuku. Vilevile niseme kwamba hatuwezi kufanikiwa katika vita hii iwapo mzazi hajaona umuhimu kwamba mtoto wa mzazi mwenzake ni wake. Ni vizuri mzazi akimuona mtoto wa mwenzake anaingia kwenye vibanda vya video aumie na ikiwezekana amzuie na kumtaarifu mzazi wake. Ingawa sina takwimu, lakini ninaamini vibanda hivyo vinachangia asilimia kadhaa kufeli kwa watoto katika masomo shuleni na vinawaathiri kisaikolojia kulingana na video chafu wanazoziona. Kiujumla ni kwamba vibanda hivyo vinawapoteza watoto wetu kielimu, wanaweza kuwa hawafiki shuleni wanaishia katika vibanda hivyo na vinawafanya wakose maadili mema. Wito wangu ni kwamba wazazi tusiachie vibanda hivyo vitulelee watoto, mwisho wa siku watakuja kuwa wasiofaa katika jamii. Kila mmoja wetu atimize wajibu wa malezi bora kwa mtoto wake, huo mtindo wa kwenda kuangalia picha chafu utafutika.



## Wafanyabiashara wa mpunga watahadharishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imewatahadharisha wafanyabiashara wa mpunga wanaotumia vipimo visivyokuwa rasmi kununua zao hilo na kuwanyonya wakulima kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu msimu mpya wa biashara ya mpunga ambao ndio unaanza katika wilaya yake. Alisema muda wowote wataanza operesheni maalumu ya kuwasaka wanyonyaji wote wanaotumia vipimo visivyoruhusiwa ikiwamo magunia ambayo hayatakiwi pamoja na mizani isiyoruhusiwa kutumika kwenye biashara.

Mfune alisema mtu yeyote atakayenaswa akitekeleza unyonyaji huo, hatafumbiwa macho na kwa sasa wanaendelea pia kutoa elimu kwa wananchi, ili wasikubali kuuza mpunga wao kwa wafanyabiashara wanaotumia vipimo feki.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha wakulima wa nchi hii wananufaika na shughuli zao za kilimo, sasa haiwezekani mwananchi anahangaika na kilimo karibu mwaka mzima halafu mtu mwingine anakuja kunufaika kwa kumwibia, hatutakubali," alisema Mfune.

Alisema ukaguzi wa vipimo vinavyotumika kwenye ununuzi wa mpunga vitakaguliwa kabla ya kuanza kutumika na kwamba ukaguzi utaendelea wa siri ili kushughulika na wanaochezea vipimo hivyo. Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Vipimo wa Mkoa wa Mbeya, Richard Mbonambucha alisema kwa sasa wanaendelea na ukaguzi wa vipimo vinavyotumika kwenye ununuzi wa mazao mbalimbali ikiwamo mpunga.

Alisema watahakikisha wanatokomeza vipimo vyote feki vinavyotumika kuwanyonya wakulima ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wanunuzi wa mazao wanaotumia vipimo visivyotakiwa kwenye shughuli hizo. Aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali wanaofanya biashara ya mazao kuhakikisha wanatumia vipimo ambavyo ni rasmi ikiwamo mizani katika kuuza mazao badala ya kutumia vipimo vya makisio.

"Sisi tunahakiki vipimo vyote ikiwamo mizani ili wananchi wauze mazao yao kwa usahihi na asiibiwe mtu, kuna baadhi ya wafanyabiashara wanakuja na mizani ambayo ikikaguliwa inaonekana iko sahihi, lakini baada ya hapo wanaichezea tena, tutashughulika nao," alisema Mbonambucha.

Nao baadhi ya wakulima wa maeneo mbalimbali wilayani Mbarali walisema kwa muda mrefu wamekuwa wakinyonywa na wafanyabiashara kupitia vipimo hali ambayo inawafanya wasipate tija kwenye kilimo chao.

Mmoja wa wakulima hao, John Kayuni alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakichezesha mizani kwa mbinu wanazozijua wao na hivyo gunia lenye kilo 100 linaanza kuonekana lina kilo 90 mpaka 95.

Alisema awali walikuwa wanawaibia kwa kutumia vipimo vingine vidogo ikiwamo matumizi ya ndoo za lita 20, lakini baada ya serikali kupiga marufuku vipimo hivyo, wafanyabiashara wanawanyonya kwa kutumia mizani.

# Ajitolea kujenga vyoo baada ya utata mil.10/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MDAU wa Maendeleo Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela ameamua kuendeleza ujenzi wa vyoo vya wanafunzi katika shule za msingi Nero na Mapambano zilizopo katika Kata ya Iyela, jijini Mbeya baada ya kutokea sintofahamu kwenye matumizi ya Sh. milioni 10 za Mfuko wa Jimbo zilizotolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.

Alifanya uamuzi huo jana wakati wa kikao cha kamati za shule hizo kilichokuwa kimeandaliwa kwa ajili ya kupokea taarifa ya matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo kutoka kwa Ofisa Mtendaji na Diwani wa Kata hiyo taarifa ambayo haikupokelewa kutokana na viongozi hao kutohudhuria.

Kikao hicho kiliitishwa kufuatia kile kilichofanyika mwishoni mwa wiki na wajumbe wakaonyesha wasiwasi ya matumizi ya fedha hizo za mfuko wa jimbo wakidai mradi umekwama, huku fedha zikiwa hazijulikani zilipo.

Mwaselela alisema kutokana na sintofahamu hiyo, yeye anaendeleza ujenzi wa vyoo hivyo na atahakikisha vinakamilika ifikapo mwezi Julai mwaka huu, ili kuwaondolea adha wanafunzi wa shule hizo ambao wako hatarini kupata magonjwa ya mlipuko.

**Sisi tunachotaka ni watoto wetu kuanza kutumia vyoo hivi, tunamshukuru mdau wetu kwa kuamua kumalizia vyoo, lakini sisi tutahakikisha fedha hizo za mfuko wa jimbo zinapatikana.**

"Tulikubaliana hapa kuwa diwani aende akamwambie mtendaji atuletee taarifa hapa, lakini kama mnavyoona diwani mwenyewe hajaja na mtendaji hayupo, sasa wao waendelee na migomo ila mimi kwa sababu nilianza mwenyewe mradi huu nitaumaliza," alisema Mwaselela.

Alisema endapo watakuwa wamezitafuna fedha hizo watajuana na viongozi wao akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya kwa madai kuwa fedha hizo zilitolewa na serikali kwa kusainiwa na Rais John Magufuli.

Baadhi ya wajumbe wa kikao hicho walidai kuwa watahakikisha fedha hizo zilizotolewa na serikali kwa ajili ya mradi huo zinapatikana na kufanya shughuli za maendeleo.

Mmoja wa wajumbe hao, Asheli Mpetele alisema baadhi ya watumishi wa serikali katika kata hiyo wameigeuza kata hiyo kuwa shamba la bibi kwa kufuja mali za umma ikiwamo fedha za miradi ya shule.

Alisema kabla ya wadau kujitokeza kuanza kujenga vyoo hivyo wananchi waliwahi kuchangishwa fedha kwa kila mwanafunzi kutozwa Sh. 4,000, lakini mpaka sasa fedha hizo hazijulikani zilifanya kazi gani na sasa fedha za mfuko wa jimbo nazo zinaanza kutoeleweka.

"Sisi tunachotaka ni watoto wetu kuanza kutumia vyoo hivi, tunamshukuru mdau wetu kwa kuamua kumalizia vyoo, lakini sisi tutahakikisha fedha hizo za mfuko wa jimbo zinapatikana," alisema Mpetele.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyela, Anna Spalika, alikataa kutoa ufafanuzi wa matumizi ya fedha hizo kwa madai kuwa taarifa anatakiwa kutoa kwa mwajiri wake ambaye ni mkurugenzi na sio kwenye vyombo vya habari.

Alisema kilichopo katika kata hiyo ni mgogoro ambao hata hivyo hakufafanua unatokana na nini, huku akidai kuwa yeye yupo chini ya mkurugenzi na kwamba mkurugenzi anajua kila kinachofanyika.



Mchuuzi wa kofia akisaka wateja katika moja ya mitaa ya Jiji la Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## H/shauri Rungwe yatoa 10% kwa wanawake

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imetoa Sh. milioni 250 zinazotokana na asilimia 10 ambayo inatengwa kutokana na makusanyo ya ndani kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi fedha hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, alisema halmashauri hiyo imetumia mapato yake ya ndani kutekeleza agizo la serikali kuviinua vikundi vya wajasiriamali. Loema alisema katika halmashauri hiyo walianza kwa kuvikopesha vikundi 35 ambavyo ni vya vijana, wanawake na Saccos, lakini hadi sasa ni vikundi 60 vimekwisha nufaika na mikopo hiyo.

"Kwa sasa tumesaidia vikundi 60 ili kutekeleza agizo la serikali la kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani na kuhakikisha fedha hizo zinatolewa bila riba, lengo likiwa ni kuendeleza shughuli za uchumi kwa wananchi," alisema Peter.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Ezekiel Mwakota, akikabidhi hundi hiyo alisema wananchi walionufaika na mikopo hiyo wanatakiwa kuwaamini na kuirejesha kwa muda fedha hizo.

Alisema fedha hizo zimetolewa kwa baadhi ya vikundi, lakini kuna watu wakishachukua wanaziingiza katika matumizi mabaya ya kuanza kunywea pombe na kutoona manufaa yake kama serikali ilivyokuwa imekusudia.

"Hizi fedha zikirudishwa kwa muda mwafaka itakuwa ni njia moja wapo ya kutoa fursa kwa watu wengine pia hata vikundi hivyo vitabakiwa na faida ya asilimia 10 ambazo zitaendelea kuwaendeleza," alisema Mwakota.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Rungwe, Deodatus Nenze, alisema maombi ya vikundi ni mengi na kwamba wataendelea kutoa mikopo hiyo kwa vikundi vilivyokidhi vigezo kwa kuwa sasa haina riba.

Alisema halmashauri kwa sasa inaendelea kukusanya mapato mengine ambayo yatachukuliwa asilimia 10 na kukopesha katika vikundi vingine ili kuhakikisha wananchi wilayani humo wananufaika na mikopo hiyo.



# Operesheni ondoa mizinga ya miti yaja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii inatarajia kuanza operesheni ya kuondoa matumizi ya mizinga ya kufugia nyuki ya kienyeji inayotumia magome ya miti na kuwataka wananchi kutumia ya kisasa ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

**Tumekuja na mpango wa kugawa mizinga hiyo 50,000 kwa wananchi na watatakiwa kuchangia kiasi kidogo cha fedha.**

Akizungumza jijini Dodoma juzi katika kuelekea kilele cha Siku ya Nyuki Duniani, Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kutoka wizarani, Ezekiel Mwakalukwa, alisema operesheni hiyo itafanyika kufuatia mkakati wa usambazaji wa mizinga ya kisasa 50,000 ili kuzuia ukataji miti.

Alisema wizara inamikakati mbalimbali ya kutunza misitu ambayo imekuwa ikiharibiwa kutokana na ufugaji nyuki na kwamba kwa sasa mikakati hiyo itawezesha kulinda misitu iliyopo nchini.

"Zipo sababu mbalimbali zinazofanya kupungua kwa nyuki, moja wapo ni ukataji wa miti au kukoboa kwa ajili ya kutengenezea mizinga kwa njia ya kienyeji, huku wakijua kuwa maua ya miti hiyo ndiyo yanayotumika katika uzalishaji wa asali," alisema.

"Tumekuja na mpango wa kugawa mizinga hiyo 50,000 kwa wananchi na watatakiwa kuchangia kiasi kidogo cha fedha," alisema Mwakalukwa.

Akiwasilisha mada katika mdahalo unaohusu sekta ya nyuki, mkufunzi kutoka Chuo cha Mafunzo ya Nyuki Tabora, Mohamed Wawa, alisema kwa mujibu utafiti mbalimbali uliofanywa na wataalamu, moja ya changamoto inayoathiri ufugaji wa nyuki ni matumizi ya viuatilifu.

Hata hivyo, aliwataka watumiaji wa viuatilifu kuwathamini nyuki kwa kupuliza dawa kwenye mimea wakati wa jioni kwa kuwa muda huo wanakuwa wamepumzika kwenye mizinga.

Aidha, aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu ili kuboresha ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la wafuga nyuki nchini, Rudia Issa, alisema ili kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya hiyo, kuna kila sababu ya kuandaa kongamano la kitaifa litakalohusisha wizara zote ili kuweka ushirikiano katika kulinda rasilimali za nyuki.



Wakulima wakipima uzito wa mazao ya ufuta kabla ya kuuza katika eneo la Mjini Kati, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Baadhi ya wanunuzi wasiowaaminifu wamekuwa wakinunua mazao hayo, bila kupima na kuwadhulumu wakulima. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanaoharibu mizani kuchukulia hatua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa serikali wa vipimo mkoani Dodoma umewaonya wafanyabiashara wenye tabia ya kuharibu mizani yao kwa madhumuni ya kuwaibia wateja kuwa watawachukulia hatua za kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Kaimu Meneja Wakala wa Vipimo Mkoa wa Dodoma, Joachim Dotto, alisema kumekuwa na uelewa mdogo kwa baadhi ya wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kuhakiki vipimo vyao.

Dotto, alisema wengi wanakwepa upimaji wa kutumia mizani bila kuelewa umuhimu wake wakihisi kufanya hivyo kutamfanya ampunje mteja na kusahau kuwa wanaweza kujipunja wenyewe.

"Ukitumia vipimo unakuwa na uhakika na viwango vya kile ulichokipima, wengine hawatumii vipimo pengine kwa kukosa elimu, lakini wengine wanafanya hivyo makusudi au kuchezesha mizani ili tu kumuibia mteja bila kutambua kuwa wanapoteza wateja, na kwenda kinyume cha sheria za nchi yetu," alisema Dotto.

Hata hivyo, alisema kwa muda wa wiki moja walifanya shughuli mbalimbali lengo likiwa ni kutoa elimu kwa jamii ili kujua umuhimu wa kutumia vipimo ambavyo ni sahihi.

Naye Ofisa vipimo, Zaidat Gharib, alisema kwa wateja au wanunuzi wa bidhaa wanapohisi kuwa wanafanyiwa wizi kwenye duka au bucha watoe taarifa mapema ili kudhibiti tabia hiyo kabla haijakithiri.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kufuata sheria na taratibu za serikali hasa biashara zao ili waweze kuepuka faini ama vifungo.

Aliwataka wateja kutambua kuwa ili kuepuka kuibiwa ni lazima kuangalia stika ya mzani uliohakikiwa na wakala wa vipimo.

# BMH kufanya upasuaji kwa njia ya matundu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH), inatarajia kuendesha kambi ya wiki mbili ya upasuaji na uchunguzi kwa kutumia upasuaji wa matundu madogo (Endoscopic Surgery) kwa magonjwa mbalimbali ikiwamo ya uzazi.

Akizungumza jana kuhusu kambi hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa huduma za upasuaji na Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi katika Hospitali hiyo, Dk. Januarius Hinju, alisema kambi hiyo itaanza Juni 7-21, mwaka huu.

Alisema kambi hiyo itaendeshwa kwa ushirikiano kati ya madaktari bingwa wa BMH na wenzao kutoka Marekani.

"Upasuaji huo utakuwa wa magonjwa yote hata wenye matatizo ya uzazi, kutokushika mimba, ngiri (hernia), waje BMH kuanzia sasa kwa ajili ya uchunguzi ili watakaokutwa na matatizo wapangiwe huduma hiyo ya upasuaji wakati wa kambi hiyo," alisema Dk. Hinju.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Dodoma na mikoa jirani kujitokeza kuanza kufanyiwa uchunguzi ili wale watakaogundulika na matatizo waweze kufanyiwa upasuaji.

Dk. Hinju alisema upasuaji wa matundu madogo ni wa kisasa ambao una faida kubwa kwa mgonjwa kulinganisha na upasuaji wa kawaida.

Alitaja baadhi ya faida hizo kuwa ni pamoja na muda mchache anaotumia mgonjwa kupona baada ya upasuaji, maumivu kidogo pamoja na mgonjwa kutotokwa na damu nyingi wakati wa upasuaji.

"Kambi hii inalenga kuimarisha huduma za kibingwa kwa mwaka wa pili mfululizo katika hospitali hii na kambi ya kwanza ilifanyika Julai, mwaka jana," alisema.





NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said (kushoto); Mwakilishi wa Chakechake, Suleiman Sarahan (kulia) na Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Yahya Ahmada Abdulwakili (katikati) wakibadilishana mawazo nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mabadiliko sheria kuboresha ZSSF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, amesema marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yamelenga kuboresha mfuko huo, kuuwezesha kutekeleza majukumu yake ya kulipa mafao kwa wastaafu.

Aliyasema hayo wakati akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) pamoja na marekebisho yake.

Alisema marekebisho hayo yamefanyika kutokana na utafiti mbalimbali ambao ulionyesha kwamba mfuko huo unahitaji marekebisho ya sheria ili kuufanya kuwa bora zaidi.

Alikanusha taarifa za baadhi ya watumishi wa serikali wastaafu wanaodai kwamba mafao yamepungua kwa asilimia 60.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba hakuna mafao yaliyopungua kwa watumishi wastaafu. Sisi tumeboresha mafao na kuwa miongoni mwa mifuko inayoongoza kwa maslahi bora ya mafao kwa watumishi nchini," alisema Balozi Ramia.

Ramia alisema mfuko huo umelipa mafao ya watumishi wastaafu viinua mgongo yenye jumla ya zaidi ya Sh. bilioni 3.7 kati ya Januari na Machi, mwaka huu.

Aidha, alisema mfuko una Sh. 2,461,565,428 ikiwa ni fedha za pensheni kwa wastaafu 266.

# Waziri asema ajira hazizingatii ubaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Issa Haji Gavu, amesema ajira serikalini hazizingatii jinsia.

Akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, alisema ajira katika utumishi wa umma Zanzibar zinazingatia sifa na uwezo wa mtu na si jinsia.

Gavu alitoa ufafanuzi huo jana alipokuwa anajibu hoja za baadhi ya wajumbe wa baraza hilo waliohoji kwa nini serikalini hakuna madereva wanawake na badala yake nafasi hizo zimeshikiliwa na wanaume.

**Si kweli kwamba ajira zinazotolewa serikali zinatumika kwa msingi wa rushwa.**

Alisema hakuna dereva mwanamke aliyeajiriwa serikalini na si kwamba serikali inaajiri watu kwa kuzingatia jinsia bali hakuna mwanamke aliyeomba ajira kupitia nafasi ya udereva.

"Madereva wanawake wapo lakini hawajaajiriwa serikalini kwa misingi kwamba ni madereva na suala la msingi serikali hauzingatii jinsia bali sifa za elimu zinazostahili," alisema.

Alisema kama wako wanawake wenye sifa wanaweza kuomba nafasi hiyo na kwamba hakuna ubaguzi wa kijinsia katika kada hiyo ya ajira.

Pia alisema si kweli kwamba ajira zinazotolewa serikali zinatumika kwa msingi wa rushwa na yeyote mwenye ushahidi juu ya hilo anapaswa kutoa taarifa katika vyombo husika ili hatua zichukuliwe.

Kuhusu bima ya afya, alisema Sera ya Afya ya Zanzibar imekataa watumishi wa umma kuwa na bima ya afya kwa kutambua jitihada zinazofanywa na serikali katika kuboresha huduma za afya na huduma hiyo inatolewa bila malipo.

# Apigia debe mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara, Viwanda na Masoko imewataka wakulima wa Zanzibar kujikita zaidi katika kilimo cha biashara cha mazao ya viungo ambacho soko lake ni la uhakika.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Khamis Hassan Hafidh, aliyasema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa mikakati ya wizara katika kuendeleza kilimo cha mazao ya biashara katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Hafidh alisema mazao ya biashara yamebainika kuwa mkombozi kwa wakulima kutokana na soko lake kuwa la uhakika nje ya nchi.

Aliyataja mazao ambayo soko na bei yake ni nzuri ni vanila, pilipili manga, pilipili hoho na uzile.

"Serikali inawataka wakulima wa mazao ya biashara sasa kujikita katika kuendeleza mazao ya viungo ikiwamo pilipili manga, pilipili hoho na vanila," alisema.

Naibu Waziri alisema wizara imeanza kuwashajihisha wakulima kupanda miti aina ya mikaratusi ambayo mafuta yake soko lake liko kubwa katika nchi za Asia.

Alisema Wizara ya Biashara imetiliana saini na kampuni ya Huashu kutoka China kwa ajili ya kununua mafuta ya mkaratusi, huku kampuni hiyo ikikifanyia ukarabati mkubwa kiwanda cha Makonyo kilichoko Pemba.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumetiliana saini na kampuni ya Huashu kutoka China kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya makonyo na mkaratusi ambayo soko lake lipo kubwa nchini humo," alisema.

# Kanisa lawapa neema wananchi

**Na George Tarimo,** KIDAMALI

KILIO cha wananchi wa Kijiji cha Kidamali wilayani Iringa cha kukosa huduma ya afya kimepata ufumbuzi, baada ya Kanisa la Orthodoks kujenga zahanati kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 100 ambayo itatoa huduma kwa wananchi hao bure.

Zena Dembe, alisema zahanati hiyo itapunguza changamoto ya kusafiri umbali mrefu, wengine kufia njiani bila kufika kituoni, kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

**wananchi wamepokea mradi huo vizuri kwa sababu utapunguza msongamano katika Kituo cha Afya Nzihi.**

Wanakijiji wengine Anna Pugiri na Daima Luvanda walisema uwapo wa zahanati hiyo ni fursa nzuri kwa sababu itapunguza gharama za kiuchumi kutembea umbali mrefu, pia itasaidia wananchi wa uchumi duni kwa kuwa huduma za matibabu zinatolewa bure.

Luvanda alisema kanisa hilo limekuwa likiwachangia kwa mambo mbalimbali ikiwamo ujenzi wa shule za msingi na sekondari akitolea mfano sekondari za Kidamali na Magubike.

Padri Dimitrios Nziku, Makamu wa Askofu na Katibu wa Askofu wa kanisa hilo Jimbo la Arusha na Tanzania ya Kati, alisema ujenzi huo ni moja ya miradi ya kanisa ambayo lengo lake ni kusaidia jamii bila kujali dini, kabila wala rangi, huku akibainisha huduma hiyo itatolewa bure kila siku tofauti na awali ambapo walikuwa wakitoa kwa siku mbili tu kwa mwezi.

Aliongeza kuwa wananchi wamepokea mradi huo vizuri kwa sababu utapunguza msongamano katika Kituo cha Afya Nzihi.

Alisema wametoa huduma ya kuchimba visima vya maji kwa ajili ya kuhudumia jamii ambavyo ni Kitapilimwa, Sasamambo, Mangalali, Kibebe, Ipwasi na Ibogo na kuunga mkono juhudi za serikali katika masuala ya elimu kwa kujenga shule za msingi Ipwasi na kuweka samani zote Ibogo, Ilalasimba pamoja na huduma zingine nyingi.

Zahanati hiyo ilizinduliwa na Kiongozi wa Kanisa la Orthodoks Afrika, Mwenyeheri Papa Patiriaka Theodoros II wa Aleksandria, huku Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Steven Muhapa licha ya kushukuru kanisa hilo kujenga zahanati pamoja na vifaa tiba, dawa ameomba serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kujenga chumba cha kuhifadhia maiti kwenye zahanati hiyo ili kupunguza adha kwa wananchi kusafiri hadi katika Hospitali ya Ipamba au Iringa kuhifadhi maiti.



Meneja wa Kiwanda cha Sierra kinachozalishaji mafuta ya msandali, Ashish Upadhaye (kulia), akizungumza jambo juu ya matumizi ya mti wa msandali katika kuzalisha bidhaa na Mkurugenzi wa Utafiti wa Mazingira na Usimamizi wa Mfumo Ikolojia wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Joseph Kombe (kushoto), walipotembelea kiwanda hicho Babati mkoani Manyara. Watatu kulia ni Mwenyekiti wa Bodi (NEMC), Prof. Esnat Chaggu na watatu kushoto ni Mjumbe wa Bodi hiyo, Dk. Neduvoto Mollel. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kituo afya chakwamisha wajawazito

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

WAJAWAZITO na watoto, ambao wana umri wa kuhudhuria kliniki waishio katika Kijiji cha Kimanzichana Magharibi, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wameshindwa kuhudhuria kliniki kutokana na kijiji hicho kukosa kituo cha huduma za afya takribani miaka 44 sasa.

Hayo yalisemwa kwa nyakati tofauti na wakazi wa kijiji hicho walipokuwa wakizungumza na Nipashe.

Sabina Kizaza, alisema wajawazito na watoto wanashindwa kuhudhuria kliniki kutokana na kijiji kutokuwa na kituo cha afya, hivyo kuifuata huduma hiyo vijiji vya mbali.

"Ukiwa mjamzito unaweza kwenda kijiji kingine kupata huduma za ujauzito, inatakiwa kila mwezi ufike kliniki, lakini tunashindwa kufika kutokana na umbali pamoja na gharama za usafiri na matibabu zipo juu," alisema.

Aliongeza kuwa gharama za kliniki kila mwezi ni Sh. 6,000, kujifungua kwa njia ya kawaida Sh. 30,000 ukijifungua kwa upasuaji Sh. 300,000.

Aliongeza kuwa pamoja na gharama hizo, kufika katika kituo cha afya ni usafiri wa bodaboda kwenda Sh. 10,000 na kurudi Sh. 10,000, wakati wananchi hawana uwezo huo.

Aliongeza kuwa wajawazito wakifikia siku ya kujifungua baadhi wanaenda vituo vya afya na wengine huwatumia wakunga ambao huwalipa chochote baada ya ukijifungua.

Juma Baksri, aliiomba halmashauri kuwapatia fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa kituo chao cha afya.

Diwani wa Kata ya Kimanzichana, Ally Ndipitipi, alisema kijiji kilianzishwa mwaka 1975, lakini hakina kituo cha huduma za afya. Alisema zahanati ambayo ipo katika kijiji hicho haijakamilika na inajengwa na nguvu za wanakijiji.

Alieleza kuwa hata eneo la zahanati walipewa na msamaria mwema ili paweze kujengwa zahanati ambayo itawasaidia wanakijiji kuacha kuingia gharama kubwa kwenda kutafuta huduma vijiji vya mbali.

# Tanzania yauza tani 600 za chai mnada Mombasa

**Na Mwandishi wetu**

WIKI iliyopita Tanzania iliuza kwa wanunuzi wa nje tani 600 za chai au kilo 600,000 katika mnada wa chai wa Mombasa safari hii kwa kutumia ghala lake la Dar es Salaam.

Njia iliyotumika ni kupeleka sampuli ambayo imewavutia wanunuzi mashuhuri kutoka ng'ambo. Ofisa Mtendaji Mkuu wa DL Group, Stephen Bett, alisema ndoto ya kampuni yake kuifanya Tanzania kuwa kiini cha biashara na ulimaji wa chai barani Afrika inawezekana.

"Jambo hili linawezekana kabisa. Jumatatu iliyopita peke yake tumeuza tani 600 kwa wanunuzi wa nje.

"Ghala hili litawasaidia sana wakulima au wazalishaji wa chai kupitia mnada wa kimataifa wa Mombasa," alisema Bett na kuongeza kuwa pia watapata fursa ya kuuza chai yao katika bei nzuri na yenye ushindaji sokoni.

Bett alisema ghala hilo lililoanzishwa Dar es Salaam kwa ajili kuonjea 'tasting' chai, litatumika kama sehemu ya kuhakikisha ubora, viwango na kuwajengea uwezo zaidi wakulima kuhusu zao la chai. Bett alisema kampuni yake ilituma sampuli za chai Mombasa kutoka ghala la Dar es Salaam ambapo wanunuzi wakubwa wa chai wakaithibitisha na kuifagilia ubora wa chai kutoka Tanzania.

Alisema soko la chai kwa kampuni hiyo lipo Uingereza, Urusi, Mashariki ya Kati, Misri, Afrika Kusini na Sudan kwa uchache wake.

Kampuni ya DL Group kupitia Mwenyekiti wake Mtendaji, Dk. David Langat, alitangaza hivi karibuni kwamba kampuni yake imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa kiini cha uzalishaji na ununuzi wa chai barani Afrika na ili kutekeleza dhamira hiyo imejenga ghala kubwa la kisasa.

Serikali ya Tanzania imelifanya zao la chai kuwa kati ya mazao mkakati saba ya biashara.

ITV

JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA EVELINE MHETO MJASILIAMALI KUTOKA BOKO JIJINI DAR ES SALAAM AKIELEZEA JUU YA USINDIKAJI WA VIUNGO MBALI MBALI KAMA TANGAWIZI NA VITUNGUU SAUMU PAMOJA NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA.

HABARI KIMATAIFA

## Congo yazizima Katumbi akirejea nyumbani

**KINSHASA,** Congo

KIONGOZI wa upinzani wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Moise Katumbi, amelakiwa na maelfu ya wafuasi mjini Lubumbashi baada ya kuishi uhamishoni kwa takriban miaka mitatu.

Katumbi alipokelewa jana na maelfu ya wafuasi waliojawa na furaha na shangwe katika Uwanja wa Ndege wa Luano nchini Congo.

Kiongozi huyo wa upinzani amekuwa akiishi uhamishoni kwa miaka zaidi ya miwili iliyopita baada ya kushtakiwa na serikali ya Rais wa zamani wa nchi hiyo, Joseph Kabila kwa makosa kadhaa ya uhalifu ikiwamo udanganyifu, kuajiri maamluki na kujipatia uraia wa pili kinyume cha sheria. Umati wa watu ulionekana ukimsindikiza Moise Katumbi kuelekea katika uwanja wa michezo wa TP Mazembe.

Katika mahojiano na televisheni ya France 24, Katumbi alisema kwamba anapanga kurudi nyumbani Mei 20, ikiwa ni takribani miaka mitatu tangu aondoke nchini humo.

"Ni hakika kwamba Mei 20, nitakuwa Lubumbashi," alisema Katumbi wakati alipofanya mahojiano Mei 6, mwaka huu.

Alieleza kwamba baada ya kurudi Lubumbashi atapanga ziara ya kitaifa kwa lengo la kuwaliwaza raia wa Congo, hususani familia zilizoteswa, wanaoishi katika taabu.

Mwaka 2016, Katumbi, alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela kwa kununua nyumba kinyume cha sheria kwenye mji ulio mashariki mwa nchi wa Lubumbashi, pia kutuhumiwa kwa kuwaajiri mamluki wa kigeni ili kupanga njama dhidi ya serikali.

Wakati wa kuapishwa kwake, Rais mpya wa Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Felix Tshisekedi, aliahidi kuwaachilia huru wafungwa wote wa kisiasa wakiwamo watu wote waliofungwa wakati wa maandamano yaliyofanyika kabla ya uchaguzi wa mkuu wa mwezi wa Desemba mwaka jana. Mashtaka dhidi ya Katumbi yametupiliwa mbali na Rais Tshisekedi na kutoa fursa kwa Katumbi kurudi.

Hata hivyo, Katumbi ameeleza kwamba uamuzi wa mahakama kubatilisha hukumu ya miaka mitatu dhidi yake sio kutokana na makubaliano na Rais Tshisekedi, bali ni mfumo wa sheria ambao kwa sasa hauingiliwi kisiasa. **BBC**

# Rais Trump: Tutaichakaza Iran, haitaonekana tena

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameionya Iran kwamba isithubutu kuanzisha vita baina yake kwani itaharibiwa vibaya iwapo vita vitazuka.

"Iwapo Iran inataka kupigana na Marekani huo ndio utakuwa mwisho rasmi wa taifa hilo, msijaribu kuitikisa Marekani," alisema Trump katika ujumbe wake wa akaunti ya Twitter.

Marekani imepeleka meli zaidi za kivita na ndege katika eneo la mashariki ya kati katika siku za hivi karibuni.

Ujumbe wa Rais Trump kwenye akaunti hiyo unaadhimisha kubadilika kwa msimamo baada ya jaribio la hivi karibuni la kuficha uwezekano wa vita kati ya mataifa hayo mawili.

Siku chache zilizopita, Rais Trump aliwaambia washauri wake kwamba hapendelei shinikizo la Marekani dhidi ya Iran kubadilika na kuwa vita.

Na alipoulizwa na waandishi wa habari siku ya Alhamisi iliopita iwapo Marekani ilikuwa ikijiandaa kivita, Rais Trump alijibu: 'Sidhani'.

**Siku chache zilizopita, Rais Trump aliwaambia washauri wake kwamba hapendelei shinikizo la Marekani dhidi ya Iran kubadilika na kuwa vita.**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Javad Zarif, alisema kuwa Iran haitaki kupigana na Marekani.

"Hakutakuwa na vita kwa kuwa hatutaki vita na hakuna mtu ambaye anafikiria kuivamia Iran katika eneo hili," alisema Zarif.

Msuguano kati ya nchi hizo unajiri baada ya Iran kusitisha kwa muda majukumu yake na kuonya kuendelea kuzalisha madini ya Uranium ambayo hutumika kutengeza mafuta na silaha za kinyuklia.

Mpango huo ulilenga kusitisha vikwazo dhidi ya Iran na badala yake ilitakiwa kusitisha mpango wake wa kinyuklia, lakini Marekani ilijiondoa katika makubaliano hayo mwaka uliopita.

Rais Trump aliyataka makubaliano hayo kuwa mabaya, hivyo aliiwekea vikwazo Iran.

Tehran imedaiwa kubeba silaha katika boti kwenye eneo hilo la mashariki ya kati, wachunguzi wa Marekani wanaamini kwamba taifa hilo lilishambulia meli nne za mafuta katika pwani ya Falme za Kiarabu, madai ambayo Iran imekana.

Katika siku za hivi karibuni, Marekani imepeleka meli ya kivita inayobeba ndege kwa jina la USS Abraham Lincoln katika eneo hilo na imedaiwa kuwa kuna mpango wa kuwatuma wanajeshi 120,000 katika eneo hilo.

Marekani imeshawaondoa raia wake wanaofanya kazi Iraq na jeshi la Marekani limetangaza hali ya tahadhari katika eneo hilo kutokana na ujasusi kuhusu vikosi vinavyoungwa mkono na Iran.

Wanajeshi wa Uholanzi na Ujerumani wamesitisha mazoezi yao ya kijeshi katika taifa hilo.

Siku ya Jumapili, jeshi la Iraq lilisema kuwa roketi ilirushwa katika eneo linalolindwa sana katika mji wa Baghdad ambalo kuna nyumba za serikali na balozi za kigeni. **BBC**



Raia wa Sudan wakiwa wamekusanyika nje ya makao makuu ya jeshi la nchi hiyo. **PICHA: AFP**

# Wanajeshi, waandamanaji warudi tena mezani

**KHARTOUM,** Sudan

VIONGOZI wa kijeshi na wakuu wa vuguvugu la maandamano ya umma nchini Sudan watarejea katika meza ya majadiliano kukamilisha muundo wa baraza tawala la mpito, baada ya majadiliano hayo kushindwa kuleta tija hapo awali.

Kwa mujibu wa msemaji wa baraza la kijeshi la mpito, Jenerali Shamseddine Kabbashi, mazungumzo hayo yataendelea kukiwa na matumaini makubwa ya kufikia makubaliano.

"Hatuna pupa ya kufikia ushindi muhimu, matokeo yoyote yatakayopatikana yatamaanisha hatua moja mbele, mazungumzo ya leo usiku yanahusiana na "madaraka ya utawala wa mpito," ilieleza taarifa kwenye mtandao wa Twitter iliyotolewa na wasomi wa Sudan ambao ndiyo waanzilishi wa vuguvugu la malalamiko

Viongozi wa vuguvugu la malalamiko wanataka kiongozi wa baraza hilo la mpito awe raia, baada ya wito wa jumuiya ya kimataifa kutaka majadiliano yamalizike kwa kuundwa kipindi cha mpito kitakachoongozwa na raia.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mazungumzo hayo yangejikita katika suala la kugawana viti vya baraza la mpito kati ya wanajeshi na raia pamoja na kumteua atakayeliongoza baraza hilo.

Wanajeshi na wanaharakati wanaopigania mageuzi walikubaliana kuhusu mada kadhaa kabla ya kusitisha mazungumzo yao, ikiwa ni pamoja na kipindi cha mpito cha miaka mitatu, kuundwa bunge la watu 300, ambalo theluthi mbili ni wawakilishi wa muungano kwa ajili ya uhuru na mageuzi.

Majadiliano kati ya pande hizo mbili yalisitishwa Jumatano iliyopita na baraza la kijeshi linaloongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhane aliyetwaa madaraka baada ya kupinduliwa kwa Rais Omar al Bashir, Aprili 11, mwaka huu.

Kabla ya mazungumzo kuanza, kwa mara ya kwanza tangu Omar al Bashir alipopinduliwa mamia ya wafuasi wa itikadi kali waliandamana Jumamosi iliyopita mbele ya kasri la rais wakipinga aina yoyote ya utawala wa kiraia ambao hautaitumia sheria ya dini ya kiislam kuwa ndio mwongozo wa sheria nchini Sudan.

Sheria ya Kiislamu inatumika nchini Sudan tangu mapinduzi yaliyomleta madarakani Omar al Bashir aliyekuwa akiungwa mkono na wafuasi wa itikadi kali mwaka 1989. **DW**

# Wateja Halopesa kufanya malipo ya simu kwa visa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI za Halotel Tanzania na Visa zimesaini mkataba wa kimkakati ambao utawawezesha watumiaji wa Halopesa kufanya malipo kwa njia ya visa kupitia simu zao.

Naibu Mkurugenzi wa Halotel, Nguyen Tien Dung, alisema jana wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa ushirikiano kati ya kampuni hizo utawezesha watumiaji wa Halopesa kutumia huduma ya visa kwenye simu zao kwa kufanya malipo ya bidhaa na kuweka pesa na kutoa kwa mawakala wa huduma ya visa.

Dung alisema takwimu kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), iliyotoa mwaka 2018 inasema kuwa Halopesa ni huduma ya malipo kwa njia ya simu inayokua kwa kasi nchini na idadi ya wateja waliojisajili kwa huduma ya Halopesa imeongezeka kwa asilimia 71.76 katika kipindi cha mwaka 2018. Kampuni ilifunga mwaka 2017 ikiwa na watumiaji 780,000. Idadi hiyo imeongezeka kwa hadi kufikia milioni 1.3 mwishoni mwa mwaka 2018.

"Kwa ukuaji mkubwa wa idadi ya wateja wa Halotel na kuwa ni mtandao wa simu unaokua kwa haraka hapa Tanzania tangu tuanze kutoa huduma hapa nchini, tuna imani kwamba idadi ya watumiaji wa Halopesa pia itaendelea kuongezeka," alisema Dung.

Alisema kwa sasa Halopesa ina zaidi ya mawakala 40,000 na nguvu ya huduma ya visa inaipa Halopesa thamani na uwezo zaidi wa kuwezesha wateja kufanya manunuzi kwa njia ya visa kupitia simu zao.

Mkurugenzi wa visa nchini, Olive Njoroge, ameelezea kuwa ushirikiano huo unalenga zaidi katika kuunganisha Watanzania kwenye huduma ya visa na kuleta usalama wa fedha zao kufanya malipo fanisi kwa huduma na bidhaa.

## Mwanaharakati Chadema aweka msimamo

INATOKA UK.8

mamo yake ambayo imekuwa ikilenga kukosoa mambo mbalimbali.

"Kwa kuwathibitishia zaidi kwamba tukio langu ni la kisiasa ni maneno ya watekaji. Ilikuwa tarehe 4 (Jumamosi), siku moja baada ya Rais John Magufuli kumaliza ziara mkoa wa Mbeya. Kwangu ilikuwa siku ya kwanza kuonekana hadharani kwa sababu sikuwapo muda, nilitembelea ofisini kwangu asubuhi," alisema.

Kuhusu kubadili msimamo wa kisiasa alisema: "Kazi ya sikio haiwezi kufanywa na pua, pua itafanya kazi yake na sikio kazi yake. Siwezi kubadili msimamo wangu na mkae mkijua ujasiri ni asili ya mtu," alisema.

"Nimezaliwa hivi hivi kama kuna maiti au umauti unanitafuta ni mara mia kwenye maisha, ni bora kifo huwa kina tisha sana lakini kifo ni kizuri kama unakufa ukiwa unawapigania wanyonge na watu ambao hawawezi kusema, kifo ni kibaya kama unakufa unawadhulumu wanyonge," aliongeza.

Mdude (pichani) aliwashukuru viongozi wa dini waliofanya kazi ya kupiga kelele baada ya tukio hilo na kuwaomba waendeleze kwa wengine ambao hawajapatikana hadi sasa.





Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Barclays Tanzania, Abdi Mohamed (kushoto), katika hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa wateja wao jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mkurugenzi wa Habari katika Ofisi ya Shekhe wa Mkoa, Tabu Kawambwa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Korosho moto bungeni

INATOKA UK.8

kamati ya watu wachache waende wakague kwenye maghala. Nataka nikwambie kuwa korosho imeoza kwa asilimia 30. Weka watu wakakague maana tukiendelea kuzubaa hata zilizopo zitaoza, tutapata hasara zaidi."

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akichangia mjadala huo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, alisema ataunga mkono kufanyika kwa uchunguzi wa ununuzi wa korosho ikiwa utajikita katika upatikanaji wa malighafi za kutosha viwandani na wakulima kulipwa vizuri.

Kakunda alisema unahitajika uchambuzi wa kina utakaofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuweka mfumo wa kuhakikisha viwanda vinapata malighafi ya kutosha.

"Ushindani wa bei umekuwa mkubwa kiasi kwamba viwanda vyetu vinapata shida kushindana na kampuni nyinginе," Kakunda alisema.

Alibainisha kuwa katika miaka 10, viwanda vingi vya korosho nchini vimekufa kwa sababu ya ushindani uliko katika soko.

Kuhusu baadhi ya wabunge kutaka viongozi kuwajibika kwa uhujumu wa zao la korosho, Kakunda alisema uhujumu uchumi ni suala la kisheria ambalo lina utaratibu wake ikiwa ni pamoja na kukamilisha uchunguzi wa kutosha dhidi ya mashtaka husika.

"Wakati tunamwachia Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika jambo hilo, tunatambua kabla ya Rais hajachukua hatua ya kumkomboa mkulima kwa kumlipa Sh. 3,300 kwa kila kilo (ya korosho), hakuna kampuni hata moja ambayo ilikuwa imefikia ofa hiyo," Kakunda alisema.

Aliongeza kuwa baada ya serikali kutangaza kununua korosho, zilijitokeza kampuni na kusema zinaweza kulipa kwa bei hiyo au zaidi.

**SIKU 40**

Kakunda alisema serikali itahakikisha inawalipa wakulima wote walioiuzia korosho na taarifa za mauzo hayo zitawasilishwa bungeni kabla ya kumalizika kwa mkutano huu wa Bunge la Bajeti, yaani ndani ya siku 40 kuanzia jana.

Akihitimisha mjadala huo, Waziri wa Kilimo (Hasunga) alisema serikali itawalipa wakulima wote wa korosho hata kama itachelewa kuuza korosho ilizozikusanya kutoka kwao. Alisema itawalipa wakulima hao ikibidi hata kwa kukopa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

02-04- 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe 23/5/2019 kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka NAMANGA kuelekea SONGEA. Magari hayo yenye namba za usajili:

T 116 DCG / T 901 CZT
Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.50 |
| Upana- | mita | 2.90 | |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

**T 339 DEC / T 364 DCF**
Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.50 |
| Upana- | mita | 2.90 | |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

2. Njia itakayotumika: **NAMANGA mpaka SONGEA kupitia MOROGORO,** Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215239102

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## MCHANGANYIKO

**KIWANJA KINAUZWA,** KIWANJA KUNAUZWA PLOT NO. 97 BLOCK M, MEDIUM SIZE KILWA MASOKO MTAA MIINA OPOSITE UWANJA WA NDEGE BEI MAELEWANO. TEL. 0712 566677, 0753 907281.

**SALES LADY ANAHITAJIKA**
SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACE BOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33.

**MONKAL I INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu kwa waliogua muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,vidonda vya tumbo kuunguruma na kujaa gesi n.k kama umehangaika huku na kule bila mafanikio njoo nikusaidie acha kuteseka:0713293988/0758078288

NIPASHE

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**TAXATION CAUSE NO.8 OF 2019**
**RAJESHI KUMAR SHIVJI AGGARWAL ............DEGREE HOLDER**
**VERSUS**
**JOSEPH SERAFIN MOSHA..................JUDGEMENT DEBTOR**

TO:
JOSEPH SERAFIN MOSHA,
WHEREVER YOU ARE.

**NOTICE FOR HEARING,**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for hearing in the High Court of Tanzania at Moshi on 11th June, 2019 at 09:00 am before Honourable F.H. Mahimbali -Deputy Registrar.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 10th day of May, 2019

215238702

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**

**MAOMBI MADOGO YA ARDHI NAMBA 150 YA MWAKA 2018**
**NEEMA MUNUO ULASA...........MWOMBAJI**
**MUSA BISIMWA PAULO................MJIBU MAOMBI**

KWA:
MUSA BISIMWA PAULO
POPOTE ULIPO

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 19/06/2019, kuja kusikiliza shauri la maombi madogo ya ardhi iliyofunguliwa na mwombaji dhidi yako.

Unatahadharishwa kuwa endapo hautofika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 13/05/2019.

115238602

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DENNIS CHARLES** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya TVS STAR yenye namba za usajili MC662 CCE. Chassis namba MD625AF74J1LA0452.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/819/2018.**

115238402

## KUFUNGA KAMPUNI

**NYAKATO FOODS LIMITED**
**Reg No. 63507**
Bodi ya Wakurugenzi kwa pamoja na wamiliki wa Kampuni ya **NYAKATO FOODS LIMITED** wameamua kufunga Kampuni yao baada ya kuendeshwa kwa hasara. Bodi hiyo pia imemchagua Bwana **CUTHBERT SUNG'ARE KIVUYO** kuwa msimamizi wa zoezi la ufungaji wa Kampuni hiyo.
Kwa yeyote mwenye madai na Kampuni hii awasiliane na Bwana **CUTHBERT SUNG'ARE KIVUYO.**

215238002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA
Usimamizi wa Mirathi NAMBA 67/2019


Ombi la SHABANI ELIAS KIBOMA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu HABIBA SALIMU

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 7/6/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 06/5/2019

115237302

KWA MATANGAZO MADOGO MADOGO TUPIGIE
**0767 223311**

## VYETI VIMEPOTEA



**CHARLES NG'WANZALIMA ELIAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa na MAGU Secondary School mwaka 2009 chenye **Index no. S0539 - 0083**, cheti cha KIDATO CHA SITA cheny no. S.0798/0898, cheti cha Uwalimu no. **505/0393 VILIVYOTOLEWA NA CHUO CHA UALIMU KOROGWE** mwaka 2018. Pamoja na cheti cha kuzaliwa .

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**taarifa ya polisi: PMB/RB/1410/2019.**

115238102

## CHETI KIMEPOTEA




**IRENE MSOLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S515/009 kilichotolewa na ILULA SEKONDARI mwaka 1993. Cheti kilipotelea Iringa.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: IR/RB/4690/2014.**

115237902

## CHETI KIMEPOTEA



**RAPHAEL AFRICANUS BURA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0168-0543 kilichotolewa na SANU SEMINARY May 2016.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**SD REF: 51/02/05/2018.**

115237802

## CHETI KIMEPOTEA



**GIDAY GIDAHAMIT B.** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.110/41** kilichotolewa na **ILBORU SEKONDARI** mwaka 1981. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.152/559** kilichotolewa na SHINYANGA SEKONDARI mwaka 1984.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KJN/RB/4747/2018.**


# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Pathfinder INTERNATIONAL
Sexual and reproductive health without fear or boundary

# PRE-QUALIFICATION TENDER FOR SUPPLY/ PROVISION OF GOODS, SERVICES AND WORKS FOR THE FINANCIAL YEARS 2019 & 2021

**Preface**
Shortlisting is a pre-tender process that provides a shortlist of providers from which providers are obtained to bid. Shortlisting is used where requirements are of a routine nature or bidding is for a group of similar contracts. Shortlisting shall be open to all providers and providers shall be invited using a shortlist notice.

This is a shortlisting application solicitation document for potential providers for the years 2019 & 2021

The Application Form is divided into:

- Part I: General Part
- Part II: Instructions to Bidders
- Part III: Preparation of Applications
- Part IV: Submission of Applications
- Part V: Opening and Evaluation of Applications
- Part VI: Shortlisting

**PART I: GENERAL**
1.1 Scope of Application
1.1.1 PI TANZANIA invites applications for the shortlist of providers for the requirements described in ANNEX A.
1.1.2 Through out this document:
(a) The "Applicant" means the bidder submitting an application; and
(b) "Application" means a bid or submission to be short-listed.

**PART II: INSTRUCTIONS TO PROVIDERS**

**2.1 Introduction**
PI TANZANIA will evaluate and shortlist all eligible companies for the provision of various requirements for the years 2019 and 2021. Once a firm has been shortlisted, it will automatically qualify to submit a bid(s) for the provision of some or all the requirements. Bidders are advised that at the discretion of PI TANZANIA, framework contracts may result from this process for some items. In such cases, firms shall be informed about the arrangement at the time of solicitation. PI TANZANIA reserves the right to add similar types of requirements to the list in this document.

**2.2 Objectives**
PI TANZANIA invites sealed Applications from reputable providers for provision of various requirements for years 2019 and 2021 as mentioned in Annex A.

**2.3 Cost of Applying**
The Applicant shall bear all costs associated with the preparation and submission of its Application and PI TANZANIA will in no case be responsible or liable for those costs, regardless of the conduct or outcome of the shortlisting process. Application will be free of cost.

2.4 Clarification of Application Forms
A prospective Applicant requiring any clarification of the Application Forms may notify PI TANZANIA by e-mail (highly recommended), telephone or though the client's address indicated below. PI TANZANIA will respond prior the set deadline.

For clarification purposes, only, the Entity's address is:

To: Pathfinder International Tanzania
Street Address: Chato Street, Plot No 260, Off New Bagamoyo Road, Regent Estate,
Town/City: Dar es Salaam
Postal Code/P. O. Box No: P.O.Box 77991, Dar es Salaam.
Country: Tanzania
E-mail: Procurement-TZ@pathfinder.org

**2.5 Amendment of Application Forms**
2.5.1 At any time prior to the deadline for submission of applications, PI Tanzania may amend the Application Forms by issuing an addendum.
2.5.2 Any addendum issued shall be part of the Application Forms and shall be communicated electronically to all who have obtained the Application Forms from PI Tanzania.
2.5.3 To give prospective Applicants reasonable time to take an addendum into account in preparing their applications, PI Tanzania may at its discretion, extend the deadline for the submission of applications.

**PART III: PREPARATION OF APPLICATIONS**
3.1 Language of Application
The Application shall be written in English language.

3.2 Documents Establishing Applicant's Eligibility and Qualifications

The Applicant shall provide as part of its Application, documentary evidence of the Applicant's legal status, financial, technical and production capability to provide the services if a contract is awarded in the format provided in the Application Submission Sheet. Failure to provide the required information may result in disqualification.

3.3 Format and Signing of Applications

3.3.1 The Applicant is requested to submit its Application Forms in one envelope marked:

"Application for Supplier Prequalification [Insert Lot number] for supply/provision of (Description) Pathfinder International TANZANIA for the years 2019 & 2021."

In addition, Applicants should indicate on top of the envelope the category/area of procurement for which they are applying. The envelope shall contain one (1) original and no copies.

Where an applicant wishes to be shortlisted in more than one category, they shall provide different application forms for required categories and submit separate applications as above.

3.3.2 The Application shall be typed or written in indelible ink and shall be signed by the Applicant or a person or persons duly authorized to sign the Application Forms. All pages of the Application shall be initialed by the person or persons signing the Application and each page numbered.

3.3.3 Any alterations, erasures, or overwriting shall be valid only if they are initialed by the person or persons signing the Application.

3.3.4 All Pages of the application MUST be numbered sequentially starting with page number one (1) being the cover page.

PART IV: SUBMISSION OF APPLICATIONS

4.1 Sealing and Labelling of Applications

4.1.1 The Application Form shall be composed of one envelope marked as stated above.

4.1.2 For application submission purposes only, please address;
To: Pathfinder International Tanzania
Street Address:
Chato Street, Plot No 260, Off New Bagamoyo Road,
Regent Estate,
Town/City: Dar es Salaam
Postal Code/P. O. Box No: P.O. Box P.O.Box 77991, Dar es Salaam
Country: Tanzania
E-mail: Procurement-TZ@pathfinder.org

Please deliver your application to Pathfinder International Tanzania reception desk.

The application start date is: May 21, 2019

4.1.4 Unsealed and not properly addressed envelopes will be rejected by Pathfinder international-Tanzania.
Note: only sticker seals are accepted.

**4.2 Deadline for Submission of Applications**
Applications must be received by Pathfinder International Tanzania at the address specified above not later than June 18, 2019 at 2.00pm.

**4.3 Late Applications**
Any Application received after the deadline for submission will be rejected.

**PART V: OPENING AND EVALUATION OF APPLICATIONS**

5.1 Opening of Applications by Pathfinder International TANZANIA.
5.1.1 PI TANZANIA shall open the applications internally. The Applicants or the Applicants' representatives who submit applications shall sign a register as evidence for their submission.

5.2 Evaluation of Applications: PI TANZANIA will carry out the evaluation of proposals as referenced in annex B.

5.3 Clarification of Applications

5.3.1 During evaluation of the Applications, PI TANZANIA may, at its discretion, ask the Applicant for clarification of its Application. A request for clarification shall be sent to a bidder by the evaluation committee and all requests for clarifications shall be noted in the evaluation report.

5.3.2 A bidder shall be instructed to reply for clarifications within a specified time, addressing their responses to the Procurement Committee/Departments through
E-mail:Procurement-TZ@pathfinder.org.

5.3.3 Failure of a bidder to respond to a request for clarification may result in a rejection of its bid.

5.4 Contacting PI TANZANIA

5.4.1 No Applicant shall contact PI TANZANIA on any matter relating to its Application from the time of Application opening to shortlisting of Applicants.

5.4.2 Any effort by the Applicant to influence PI TANZANIA in its decisions on the Application evaluation may result in rejection of its Application.

5.5 Confidentiality

5.5.1 Information relating to the evaluation of applications and recommendation for shortlisting shall not be disclosed to Applicants or any other persons not officially concerned with such process until the notification of shortlisting is made to all Applicants.

5.5.2 From the deadline of submission of applications to the time of notification of the results of the shortlisting, any Applicant that wishes to contact PI TANZANIA on any matter related to the shortlisting process may do so but only by e-mail.

**PART VI: SHORTLISTING**

6.1 Notification to the Shortlisted Applicants

PI TANZANIA will notify all Applicants in writing via their registered e-mail addresses that they have been shortlisted to provide particular requirements for the Financial Years 2019 & 2021.

6.2 Inspection

PI TANZANIA reserves the right to conduct a physical inspection of the premises of the Applicant at its own cost and discretion. If, after the inspection, it is deemed that the physical structure and quality of service equipment is unsatisfactory, then the Application will be rejected. PI TANZANIA reserves the right to verify all information submitted.

6.3 Currency

All monetary/financial information furnished, must be quoted in Tanzania Shillings.

6.4 Changes in Qualifications of Applicants

6.4.1 Applicants and those subsequently shortlisted or conditionally shortlisted shall inform PI TANZANIA of any material change of information that might affect their qualification status. Providers may be required to update key shortlisting information at the time of bidding.

6.4.2 Prior to contract award, the best evaluated bidder may be required to confirm its continued qualified status in a post-qualification review process.

**FORM I: APPLICATION SUBMISSION SHEET**

**To: PI TANZANIA**
**Date:**
We, the undersigned declare that:

(a) We have examined and have no reservations to the Application Forms, including Addenda No:…….., [insert the number and issuing date of each Addenda];

(b) We hereby apply to be shortlisted for the following requirement:

**LOT Number** **Description of Requirement**

(c) It must be noted that PI general payment terms is within thirty (30) working days after successful/acceptance of delivery of products/service together with the Invoice and E.F.D receipt.

| Accepted | Not Accepted |
|---|---|
| | |

(d) We, including any subcontractors or providers for any part of the contract or contracts resulting from this shortlisting process do not have any conflict of interest, and are not associated, nor have been associated in the past, directly or indirectly, with any one that has prepared the solicitation document;

| Accepted | Not Accepted |
|---|---|
| | |

(e) We understand that you may amend the scope and value of any contracts to bid for or cancel the shortlisting process at any time and that you are neither bound to accept any application that you may receive nor to invite the shortlisted applicants to bid for the contract or contracts, which are the subject of this shortlisting, without incurring any liability to the Applicants;

| Accepted | Not Accepted |
|---|---|
| | |

(f) We understand that qualification information may be subject to verification through a post-qualification process prior to any award of contract;

| Accepted | Not Accepted |
|---|---|
| | |

(g) We hereby authorise you and your authorised representatives, to conduct any enquiries or investigations to verify the statements, documents and information submitted in connection with this application and to seek clarification from our bankers and clients regarding any financial and technical aspects. This Application Submission Sheet will also serve as authorisation to any individual or authorised representative of any institution referred to in the supporting information to provide such information deemed necessary and as requested by you to verify statements and information provided in this application.

Signed: …………………………………………………………..

Name: ………………………………………………………………
Dated on ___________ day of _________________, _______

**FORM II: APPLICANT INFORMATION SHEET**

**GEOGRAPHICAL LOCATION STRUCTURE AND ORGANIZATION**

i. Name of Company*:
[insert full legal name]

Contact Person:

Physical address*:
[insert street/ number/ town or city/ country]

Postal address*:

Telephone number*:

Email*:
* Must be stated

ii. Description of the Company's activities:

iii. Number of years of experience in the provision of the requirement under reference

iv. Please indicate here or attach an organization chart showing the company structure including key personnel.

**FORM III: RESOURCES: PERSONNEL**

**1. Number of staff**

- Management staff:
- Technical staff:
- Support staff:

Please list the present key personnel and management staff.

| Name of the Staff | Years of relevant experience |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

1.0 Please indicate reference of the NGOs have worked with for the supply of Medical Equipment

| Name of the NGO | Years of relevant experience |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

## HABARI MICHEZO

**FORM IV: RESOURCES: PROVIDERS EQUIPMENT AND FACILITIES**

On the basis of the information provided in the Application Forms, please indicate equipment and facilities considered by your firm to be necessary for providing the requirement and whether this is already in the company's ownership or will be purchased.

| | FORM V: LEGAL STATUS |
|---|---|
| 1 | Enclose a copy of the Power of Attorney to the signatory of the Application Forms registered by the Registrar of Companies or written authorization to submit the application |
| 2 | Enclose a copy of the Memorandum and Articles of Association or its equivalent. A separate list of Directors/Partners/Proprietors should be attached. A joint venture agreement should be attached where applicable |
| 3 | Enclose valid business certificates from relevant authorities such as; |
| a | Valid VAT Registration Certificate (Where applicable) |
| b | TIN registration certificate |
| c | Valid Business License |
| d | Certificate of incorporation/registration |
| e | Tax Clearance Certificate |
| f | Electronic Fiscal Device user Identification Number registration certificate (EFD) |
| g | Any other specific license / registration for professional bodies e.g. Contractors, engineers etc. (Where applicable) |
| h | Industry required certification or permits i.e. OSHA, Sumatra, EWURA, TCRA (Where applicable) |
| i | Certified Copy of Certificate of Title or Lease Agreements (to determine physical location) |
| j | Please enclose a copy of your firm's ISO or other quality assurance certificate, if any. |
| k | Any other relevant document |

ANNEX A: STATEMENT OF REQUIREMENTS

*List of requirements to be provided include but are not restricted to the following:*

**A: Common Goods, Services and Consultancy.**

| LOT NUMBERS | DESCRIPTION OF SERVICES |
|---|---|
| A | Printing Services: supply and printing of business cards, letter head, fliers, brochures, posters, branded stationery items, envelopes, t-shirts, manuals, various reports, designing and printing of staff ID cards, signboards, certificates, caps and the related services. |
| B | Supply of office sundries/general merchandise (i.e. sugar, milk powder, tea leaves, milo, coffee and the related items) and cleaning materials |
| C | Supply of general office stationery, cartridges and tonners |
| D | Supply, repair, servicing of fire extinguishers and equipment |
| E | Supply of tires and tubes for motor vehicles and motor cycles preferably importers, dealers and distributors |
| F | Supply of Medical equipment and consumables |
| G | Supply of drinking water for the dispensers |
| H | Provision of computers service, repair and maintenance |
| I | Provision of hotel accommodation and conference services |
| J | Provision of catering services for meetings, training and conferences and hiring of venue |
| K | Provision of motor vehicle service, repairs and maintenance |
| L | Provision of transport services specifically vehicle hire; saloon cars, pick-ups double cabin, station wagon, minibuses and trucks. |
| M | Provision of Sanitary Services |
| N | Provision of General Cleanness and Fumigation |
| O | Provision of security services |
| P | Provision of Furniture |
| Q | Provision of Air ticketing services |
| R | Provision of Plumbing and Electrical works services |

***Note 1: In case of any discrepancy between this document and the pre-qualification notice, this document shall prevail.***

***Note 2: Only ONE copy (Original) of the application document shall be required for every category applied for.***

***Note 3: Applicants must indicate on the outer envelope the category applied for***

***Note 4: No samples shall be required for this exercise***

***Note 5: Applicants shall submit and register a different document for each category applied for***

***Note 6: To obtain the full tender document, please contact:*** Procurement-TZ@pathfinder.org

**DONDO SOKA**
**MAGA ULAYA**




# MBAPPE AIITA REAL, ATANGAZA KUSEPA

## ●●● Nimegundua mengi hapa na ninahisi kuwa na majukumu zaidi...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amefunguka kuwa anazingatia mustakabali wake wa baadaye Paris Saint-Germain, huku akikiri kuwa anafungua milango kwa "mradi mpya".

**Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia, Jumapili usiku alitangazwa kuwa mchezaji bora wa Ufaransa , akitwaa tuzo zote ya Mchezaji Bora wa Mwaka na ile ya Kinda Bora wa Mwaka.**

Lakini baada ya kupokea tuzo hizo kutoka kwa Didier Drogba, mshambuliaji huyo alisema: "Ni kipindi muhimu sana kwangu, kimekuja kwa mabadiliko yangu kikazi.

"Nimegundua mengi hapa, na ninahisi labda ni wakati wa kuwa na majukumu zaidi.

"Ninatumai kwamba pengine inaweza kuwa hapa Paris Saint-Germain, hiyo itakuwa furaha kubwa ama pengine sehemu nyingine na mradi mpya."

Mbappe amefunga mabao 32 wakati akiibebesha PSG ubingwa wa Ligue 1, lakini klabu kwa mara nyingine ilishindwa tena kufurukuta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo ni malengo ya mabilionea wa Qatar, wanaomiliki klabu hiyo.

PSG ilishindwa kulinda ushindi wao wa mabao mawili walioupata ugenini kwenye mechi ya mkondo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-Bora dhidi ya Manchester United na kujikuta ikisinzia na kuwaruhusu miamba hiyo ya Old Trafford kupindua matokeo mechi ya marudiano.

Mbappe alisimamia maoni yake baada ya sherehe hizo, na kuongeza: "Nilisema kile nilichopaswa kusema.

"Unapokuwa katika tukio hilo unaweza kutuma ujumbe, nadhani nimetuma wangu. "Kama nitazungumza zaidi itatia fora na huo si ujumbe niliotaka kutuma."

Mapema mwaka huu, Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, alidai kuwa Zinedine Zidane anaweza kutumia Ufaransa wake kuipata huduma ya Mbappe katika klabu hiyo majira haya ya joto.

"Zidane ni Mfaransa, hivyo na Mbappe anaweza kufanya kitu fulani," alisema Perez.

Pep Guardiola tayari alishakana taarifa kwamba Manchester City inaweza kumsajili Mbappe Oktoba mwaka jana.

"Manchester City haina, na haitakwenda kutumia fedha ambazo pengine Mbappe anastahili, ama PSG inazostahili," alisema.

## HABARI MICHEZO

# Said ajitosa urais ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MBIO za kuwania nafasi za uongozi katika Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), zimeanza kwa Katibu Msaidizi wa Kamati ya Maridhiano, Khamis Abdalla Said, kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya urais wa shirikisho hilo.

ZFF zamani ZFA, imetangaza kuwa itafanya uchaguzi wake mkuu ifikapo Juni 2, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Said alisema kwa sasa bado muda wa kampeni haujaanza ili kutangaza sera zake, lakini yeye kilichomsukuma zaidi kugombea nafasi hiyo ni kutaka kulibadilisha soka la Zanzibar ikiwamo kuleta hamasa katika soka.

Said alisema soka la Zanzibar linahitaji viongozi wenye uelewa na maono ya juu zaidi katika kuliendesha kwake ili liweze kuwa na hamasa kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

Mgombea huyo alisema kikubwa kitakacholibadilisha soka hilo ni kufuata katiba mpya ambayo imeanza kufanya kazi hivi karibuni pamoja na kuwa na ushirikiano wa karibu na serikali sambamba na vyama vyote vya michezo.

"Kikubwa zaidi nikipata nafasi ya kuwa rais nitasimamia Katiba ya ZFF ambayo ndio mwongozo kamili wa kuhakikisha soka letu linasonga mbele kama ilivyokuwa wakati wa uongozi wa marehemu mzee Fereji (Ali Tamim Fereji), licha ya changamoto zilizokuwapo kwa wakati huo," alisema.

Aliongeza kuwa pia atahakikisha anaboresha ushirikiano na vyama vingine vya soka pamoja na kuendelea na jitihada za kuusaka uanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf) pamoja na Fifa ambao umekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wadau wa soka wa visiwani hapa.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 35 | 28 | 4 | 3 | 74 | 14 | 88 |
| 2. Yanga | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5. Mtibwa Sugar | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7. Mbeya City | 36 | 13 | 8 | 15 | 38 | 38 | 47 |
| 8. Ndanda | 36 | 12 | 11 | 13 | 23 | 33 | 47 |
| 9. Singida United | 36 | 11 | 12 | 13 | 30 | 37 | 45 |
| 10. Stand United | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 11. Alliance | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 12. Coastal Union | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13. Mbao | 36 | 11 | 11 | 14 | 26 | 38 | 44 |
| 14. TZ Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15. Kagera Sugar | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 16. Ruvu Shooting | 36 | 10 | 12 | 14 | 33 | 41 | 42 |
| 17. JKT Tanzania | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 18. Biashara United | 35 | 10 | 10 | 15 | 27 | 33 | 40 |
| 19. Mwadui | 36 | 10 | 8 | 18 | 41 | 51 | 38 |
| 20. African Lyon | 36 | 4 | 11 | 21 | 23 | 49 | 23 |

# KAMPIRA AITABIRIA YANGA MAKUBWA

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa zamani wa Yanga, wamesema wanaamini kuwa kikosi chao kitakachoshiriki Ligi Kuu Bara msimu ujao kitakuwa na timu imara na kitafanya vema kwenye mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

**Kauli hiyo imetolewa siku chache baada ya Mwenyekiti mpya wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla, kutangaza kuwashirikisha nyota hao katika mchakato wa kusajili wachezaji.**

Msolla alisema ili kuwa na kikosi imara, uongozi wa klabu hiyo utampa jukumu la usajili Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera pamoja na nyota hao wa zamani ili kukamilisha mchakato huo kwa kuwakabidhi fedha za usajili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Umoja wa Wachezaji wa zamani wa Yanga, Ramadhani Kampira, alisema uamuzi huo umewafurahisha na anaamini utaifanya timu yao kuwa bora na itakayoshinda mataji mbalimbali katika msimu ujao.

Kampira alisema wao wanawafahamu wachezaji wenye uwezo wa hapa nchini na vile vile kiufundi watamsaidia Zahera kusajili wachezaji watakaokuwa na msaada kwa Yanga na si wale watakaokuja kujaribu "bahati".

"Tunafurahi kupata nafasi hii, miaka ya nyuma wachezaji walikuwa wanasajiliwa kwa kubahatisha, tunaamini kwa ushirikiano huu, mambo yatakuwa mazuri na Yanga itakuwa tishio," alisema Kampira.

Aliongeza kuwa kwa uamuzi huo, wala Yanga haitatumia kiasi kikubwa cha fedha ili kukamilisha mchakato huo na badala yake kamati hiyo mpya itasajili kwa kuzingatia viwango.

Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambayo inaombea Simba ipoteze mechi zake zilizosalia na yenyewe kushinda michezo yake miwili iliyobakia, itashiriki Kombe la FA, Kombe la Mapinduzi na Kombe la SportPesa.



Cristiano Ronaldo, akiwa amepozi nyuma ya kombe la ubingwa wa Serie A pamoja na mama yake, Dolores (kulia) na mpenzi wake, Georgina Rodriguez, kufuatia timu yake ya Juventus kukabidhiwa rasmi kombe hilo baada ya mechi ya funga msimu dhidi ya Atalanta iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Allianz juzi. **PICHA: MTANDAO**

# *Shabiki Madrid Ifakara ashinda mil. 208/-*

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa timu ya Real Madrid na mkazi wa Ifakara, mkoani Morogoro, Gadi Mwajeka ameibuka mshindi wa zawadi ya Sh. milioni 208. 5 baada ya kubashiri kwa usahihi mchezo wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi yenye thamani hiyo, Mwajeka alisema hakuamini mara baada ya kupigiwa simu kuambiwa yeye ndiye mshindi wa zawadi hiyo ya fedha.

Mwajeka ambaye ni mfanyabiashara wa rangi za mkeka katika eneo la Ifakara mjini, alisema ushindi huo ni faraja kubwa sana kwake na anaamini utamsaidia kuboresha biashara yake na vile vile kaunzisha nyingine mpya.

Sikuamini kama nimeshinda kiasi kikubwa cha fedha, nimetumia kiasi cha Sh. 1,000 tu kubashiri na kuingiza kiasi kikubwa cha fedha. Nimefarijika sana, alisema Mwajeka. Alisema ameshiriki kubashiri kwa muda wa miaka mitatu na mwaka huu ndio amebahatika kuibuka kinara wa kiasi hicho kikubwa cha fedha.

"Mke wangu ni nesi, nilikuwa nachukua madaftari yake kuandika timu na kuanza kuzipigia mahesabu. Nitatumia fedha hizi kwa ushauri wa wazazi wangu kuona ninafanya biashara gani," alisema.

Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet, Allen Mushi, alisema Mwajeka ni mshindi wao wa tano kushinda zawadi hiyo nono, tangu walipoanza shindano hilo mapema mwaka huu.

Mushi alisema M-Bet itaendelea kuwa nyumba ya mabingwa na kuwaomba mashabiki wa soka kubashiri na kampuni yao ili kuweza kubadili maisha yao.

M-Bet ni nyumba za mabingwa na mabingwa wote wanapatikana kupitia michezo ya kubahatisha ya kampuni yetu, kujitajirisha vilevile kuichangia nchi yao kwani asilimia 20 ya fedha hukatwa kama kodi ya kusaidia maendeleo ya nchi katika sekta mbalimbali, aliongeza Mushi.

# Michezo

Jumanne Mei 21, 2019

Nipashe




Mbappe aiita Madrid, atangaza kusepa UK.30



Mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta (mwenye kombe), akisherehekea ubingwa wa Ubelgiji pamoja na wachezaji wenzake wa KRC Genk, baada ya mechi ya funga msimu dhidi ya Standard Liege kumalizika kwa sare tasa katika Uwanja wa Luminus Arena mwishoni mwa wiki. **PICHA: MTANDAO**

# Aussems: Simba anzeni sherehe

## ●●● Rekodi ya kubebea ubingwa Singida yanukia kujirudia leo, awataka mashabiki kuufanya...

**Na Somoe Ng'itu**

HESABU zitatimia? Wakati swali hilo likitikisa kichwani kwa mashabiki wa Simba kuelekea mechi yao ya leo ugenini dhidi ya Singida United, Kocha Mkuu wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Mbelgiji Patrick Aussems, amewataka kujiandaa kuufanya mji wa Singida kuwa maalum kwao kwa ajili ya kusherehekea ubingwa wa Ligi Kuu 2018/19.

**Katika mechi hiyo itakayochezwa Uwanja wa Namfua mkoani Singida leo, Simba yenye pointi 88, inahitaji ushindi ambao utaiwezesha kufikisha alama 91 ambazo haziwezi kufikiwa na klabu yoyote kwenye msimamo wa ligi hiyo msimu huu.**

Hata hivyo, Yanga inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, endapo itashinda michezo yake miwili iliyosalia itafikisha alama 89, wakati huu Simba ikiwa na mechi tatu mkononi pamoja na mechi hiyo ya leo.

Mabingwa hao watetezi, msimu uliopita pia walitwaa ubingwa wa ligi hiyo wakiwa Singida, tena siku moja kabla ya mchezo baada ya watani zao, Yanga kutoka sare dhidi ya Tanzania Prisons.

Aussems, aliliambia Nipashe jana kuwa, timu yake inahitaji kushinda mechi zote tatu za ligi hiyo zilizobaki na si mchezo mmoja wa leo kama ambavyo inaonekana.

Aussems alisema kuwa nguvu waliyotumia wakati wanaanza msimu huu ndiyo wataendelea nayo mpaka katika mchezo wa mwisho ambao utakuwa ni dhidi ya Mtibwa Sugar utakaochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

"Mashabiki wa Simba tuifanye Singida kuwa mji wetu wa kusherehekea kikombe cha ubingwa," alisema kwa kifupi kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kilifika salama Singida jana mchana kwa kutumia usafiri wa ndege kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na baadaye kutumia basi maalumu la kukodi kwenda mkoani humo.

Rweyemamu aliwataja wachezaji watakaokosekana katika mchezo wa leo ambao wamebaki jijini Dar es Salaam kuwa ni pamoja Zana Coulibaly, Said Ndemla na Mohammed Ibrahim "Mo".

Singida United itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare zinazofanana za mabao 2-2 mara mbili mfululizo, dhidi ya Stand United na JKT Tanzania, wakati Simba imeshinda michezo yake dhidi ya Mtibwa Sugar na Ndanda FC.

# Sevilla kuleta neema Dar leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa wa kihistoria wa michuano ya Europa League, Sevilla ya Hispania ambao wamemaliza msimu huu wa La Liga wakiwa nafasi ya sita, wakitarajiwa kuwasili nchini leo kwa ajili ya mechi ya kirafiki iliyoandaliwa na Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni ya SportPesa kwa ushirikiano na La Liga, neema kibao zinatarajiwa kupatikana katika ziara ya klabu hiyo.

Sevilla ambayo inatarajiwa kushuka Uwanja wa Taifa keshokutwa Alhamisi kuvaana na Simba kwenye mechi ya kirafiki, kabla ya mchezo huo itafanya shughuli mbalimbali za kuinua sekta ya michezo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema SportPesa inakwenda kuweka historia kwa mara nyingine tena nchini kwenye sekta ya mpira wa miguu kwa kuileta timu ya Sevilla.

"Kupitia ujio wao timu ya Sevilla watafanya shughuli mbalimbali zenye lengo la kuinua sekta ya michezo nchini kwa vijana na mpira wa miguu kwa ujumla.

"Watatoa mafunzo ambayo yatahudhuriwa na timu ya vijana ya Bom Bom FC katika Uwanja wa Uhuru bila kusahau semina elekezi itakayotolewa na maofisa wa klabu ya Sevilla kwa viongozi wa klabu za hapa nchini, TFF na washirika wake ili wapate kuimarika kitaaluma na kupata uelewa jinsi ya kuongeza mapato ya klabu zao.

Naye Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi aliwatangaza waamuzi watakaochezesha mechi hiyo kuwa ni mwamuzi wa kati, Elly Sasii akisaidiwa na Mohammed Mkono kutoka jijini Tanga na Soud Lila wa Dar es Salaam wakati Jonesia Rukyaa wa Kagera atakuwa mwamuzi wa akiba.

"Waamuzi wanaochezesha mchezo huu wote ni waamuzi wenye beji za Fifa, mchezo huu mbali ya kujitangaza kama nchi, lakini pia ni sehemu ya kutangaza vitu vyetu mbalimbali wakiwamo wachezaji na waamuzi," alisema Madadi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >